Nipashe
Jumanne Oktoba 15, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580049
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
witter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## RC, DC waingia kanisani, mitaani kuhamasisha uandikishaji kura

UKURASA 4


Kaskazini
Jumatatu Oktoba 15, 2019.
Nipashe
KILIMANJARO, ARUSHA, MANYARA, TANGA
Ukurasa iii
Takukuru yapiga 'mkwara' uchaguzi serikali za mitaa
Ukurasa iv
UANDIKISHAJI wa uchaguzi mitaa wasuasua Arumeru
Wenye viwanda vya chumvi walalamika
Ukurasa ii
Kanda ya Kaskazini inavyotafuta suluhu ya maji
Baadhi ya wanafunzi wa sekondari katika Mkoa wa Kilimanjaro wakifua karibu na chanzo cha maji, kutokana na tatizo la maji. PICHA: MAKTABA
Ukurasa II.

# Wastaafu waelezea upekee wa Nyerere

• **Wajukuu**, wapishi nao watoa ya moyoni, JPM asema miradi inayoendelea ni kumuenzi kwa vitendo... *Endelea ukurasa 2 & 3*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5
**HESLB YAWATAKA WAOMBAJI MIKOPO KUKAMILISHA NYARAKA**
BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imewataka wanafunzi 4,794 ambao wamekwama...

UKURASA WA 7
**SERIKALI YAAGIZA MRADI WA STAR CITY UPEWE HATI**
WIZARA ya Viwanda na Biashara imeagiza kutolewa hati kwa eneo la mradi mkubwa wa Star City kwenye...

## Necta yapata dawa vyeti feki

UKURASA 4




UKURASA 2

Rais John Magufuli akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge mwaka huu, Mzee Mkongea Ally, katika sherehe za kilele cha Mbio za Mwenge, Wiki ya Vijana na Kumbukizi ya Miaka 20 ya Kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, mjini Lindi jana. **PICHA: IKULU**



## Ripoti madudu Mwenge yatua rasmi Takukuru

MICHEZO SABABU IAAF KUIKATAA REKODI YA KIPCHOGE UK.31
MAONI, KATUNI UK.6

# Wastaafu, viongozi waelezea upekee wa Mwalimu Nyerere

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wa serikali, wastaafu, wajukuu na wapishi, kwa nyakati tofauti wamemwelezea Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kuwa alipenda watu waadilifu na utajiri alioutaka ni wa kuondoa matatizo ya Watanzania.

Hayo yalisemwa jana Butiama mkoani Mara wakati wa Kongamano la Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere ambalo lilihudhuriwa na viongozi wa serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM), wastaafu, wazee wa mila na wageni ambao walifanya kazi naye enzi za uhai wake.

Mwalimu Nyerere alizaliwa katika Kijiji cha Mwitongo, Butiama mkoani Mara Aprili 13, 1922 na alifariki dunia Oktoba 14, 1999 jijini London, Uingereza alikokwenda kwa matibabu.

Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara), Philip Mangula, alisema Nyerere alikuwa mtu wa kawaida na aliamini mtu akifanya kosa, si lake bali la yule aliyemteua.

Alisema Mwalimu Nyerere katika kujenga utaifa, alianzisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na aliamini kwamba wote ni sawa na rushwa ni adui wa haki.

Mwanasiasa mkongwe, Stephen Wassira, ambaye ameshika nyadhifa mbalimbali katika serikali tangu awamu ya kwanza hadi ya nne, alisema alimfahamu Mwalimu Nyerere akiwa na umri wa miaka 13 kwa kumsikiliza hotuba zake kwenye redio wakati huo akipinga ukoloni na kusema kutawaliwa ni fedheha.

Alisema siku moja alikwenda nyumbani kwa Mwalimu Nyerere katika mazungumzo na kwa sababu alimweleza mambo ambayo hakuyapenda, alinyanyuka na kuchukua jembe na kwenda shambani kulima nyuma ya nyumba yake.

"Nikawauliza walinzi wake, mwalimu amekwenda wapi wakaniambia kulima. Nikamwambia nipeni jembe Rais hawezi kulima peke yake, tukalima akiwa amenyamaza. Baada ya kuona nalima sisemi, akaniambia mheshimiwa mbunge yale mambo yamekwisha tulime.

"Mwalimu alikuwa hashikilii hasira wala hakuwa na chuki, lakini ukijenga hoja anakuelewa. Hata asipoitekeleza hoja yako siku hiyo hiyo, ataitekeleza baadaye. Alikuja kutekeleza akagawa Wilaya ya Bunda.

Wassira alisema mwaka 1973, Mwalimu Nyerere alimteua kuwa Waziri Mdogo (Naibu

INAENDELEA UK 8



Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Joseph Warioba (kulia), Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Phillip Mangula (wa pili kulia), Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (wa pili kushoto), familia pamoja na viongozi wengine wakiwa mbele ya kaburi la Hayati Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere katika maadhimisho ya miaka 20 ya kifo chake, katika kijiji cha Mwitongo, Butiama mkoani Mara jana. **PICHA: WANMM**

# Ripoti miradi ya Mwenge yatua Takukuru

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kufanya uchambuzi wa ripoti ya miradi ya maendeleo iliyoshindwa kufunguliwa na viongozi wa Mbio za Mwenge, kuwafikisha mahakamani viongozi wote waliohusika katika ubadhirifu.

Amemtaka Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo, kuichambua ripoti hiyo kila nukta, kila ukurasa na kufanyika uchunguzi wa kina na kuwafikisha mahakamani wahusika wote.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo jana kwenye Uwanja vya Ilulu, Lindi, wakati wa maadhimisho ya kilele cha Mbio za Mwenge na kumbukizi ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere muda mfupi baada ya kupokea ripoti.

"Mtu wa Takukuru uko wapi? Njoo hapa mbele nikukabidhi ripoti hii. Naikabidhi hii ripoti kwa Takukuru ukaikague, uiangalie wale wanaotakiwa kupelekwa mahakamani, na wale ambao unaona huwawezi niletee ripoti zao. Nataka Tanzania inyooke," alisema Rais Magufuli.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, wakati akisoma hotuba kwenye maadhimisho hayo, miradi ya maendeleo 107 yenye thamani ya Sh. bilioni 90.2 kwenye halmashauri 82 nchini ilibainika na kasoro.

Mhagama alisema katika mbio za Mwenge zilibainika kasoro katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa ya maji, elimu, barabara na ujenzi wa majengo ya umma.

Alisema miradi hiyo haikuzinduliwa au kuwekwa mawe ya msingi na viongozi wa mbio za Mwenge kutokana na kasoro hizo zisizoendana na matumizi ya fedha katika miradi husika, kujengwa kinyume cha mikataba na makadirio yaliyopitishwa na wataalamu, makandarasi kushindwa kufuata na kusimamia kanuni za ujenzi.

Kwa mujibu wa Mhagama,

INAENDELEA UK 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
05-10-2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe 13-10-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka Dar es salaam kuelekea Chang'ombe, gari hizo zenye namba za usajili:

   **T 636 DFA / T 887 DJB**
   **T212 BTE/T 574 BZB**
   **T653 DFA/T 900 BAZ**
   **T195 BTE/T837 DJB**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 27 |
| **Upana** | - | mita | 4.0 |
| **Kimo** | - | mita | 5.1 |

3. Njia itakayotumika: Dar es salaam Port hadi Chang'ombe kupitia Mandela road, Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215454002


## Magufuli asisitiza kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa vitendo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amesema serikali anayoiongoza itaendelea kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kwa kuheshimu tunu za taifa ukiwamo Mwenge wa Uhuru pamoja na kuwathamini vijana kwa kuwateua kuwa viongozi.

Akizungumza jana wakati wa kilele cha Mbio za Mwenge na Kumbukumbu ya Miaka 20 ya Kifo cha Baba wa Taifa, kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi. Mwalimu Nyerere alifariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, London nchini Uingereza alikokuwa akipata matibabu.

Alisema serikali ya awamu ya tano inamuenzi Mwalimu Nyerere kwa kuanzisha balozi mbalimbali ikiwamo ubalozi wa Korea, Cuba na kwamba imemuenzi kwa kuhamisha makao makuu ya nchi kuwa Dodoma.

"Nampongeza Rais mstaafu wa awamu ya nne Jakaya Kikwete kwa kuendeleza utaratibu wa kumkumbuka Baba wa Taifa, katika miaka 10 ya utawala wake. Serikali ninayoiongoza tumejitahidi kumuenzi kupitia kukemea rushwa na kutoa elimu ya msingi bila malipo," alisema.

Rais alisema Baba wa Taifa aliamini kulinda uchumi na kulinda uhuru wa kisiasa ni kuwa na taifa la kujitegemea, ndiyo maana alianzisha Azimio la Arusha na kwamba bado lina msingi kwenye taifa.

Aidha, Rais Magufuli aliwataka Watanzania kusimamia miiko ya Azimio la Arusha, kumtanguliza Mungu, kuwa na umoja pasipo kubaguana na kujitayarisha kwa kufanya mambo mazuri.

Aliwataka Watanzania kuendelea kumuenzi kwa kutekeleza kwa vitendo misingi ya Uhuru na Azimio la Arusha ambalo linahimiza watu kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa, elimu kwa wote hasa elimu ya ufundi, kupiga vita umasikini na ukosefu waa jira, kujenga miundombinu, uzalendo na nidhamu kwa watumishi wa umma.

Rais magufuli alisisitiza kuwa serikali ya awamu ya tano itajitahidi kwa kadri iwezavyo kumuenzi Baba wa Taifa kwa vitendo klama ambavyo inafanya sasa.

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Viongozi wa dini wasisitiza amani

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wa dini mbalimbali wameiombea Tanzania amani, upendo na utulivu na kumwombea kwa Mungu Rais John Magufuli, ampe uadilifu zaidi na uwezo wa kuona mambo ya heri zaidi pamoja na viongozi wengine.

Maombi hayo yalifanyika jana katika uwanja wa Ilulu mkoani Lindi wakati wa maadhimisho ya kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, kumbukizi ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na Wiki ya Vijana Kitaifa.

Wakitoa dua na sala katika maadhimisho hayo, viongozi hao walimshukuru Mungu kwa kuendelea kuifanya Tanzania kuwa na amani na kuwa nchi ya mfano Afrika Mashariki. Sheikh wa Mkoa wa Lindi, Mohamed Mshangani, kwa niaba ya Baraza Kuu la Waislam Tanzania (Bakwata) alimwomba Mungu aendelee kuilinda amani iliyopo.

"Utujalie nchi yetu hii pamoja na viongozi wetu wakiongozwa na Jemedari Mkuu, Rais Magufuli, Mungu akupe uadilifu zaidi na uono wa kuona mambo ya kheri zaidi wewe pamoja na jopo la viongozi wa juu wa taifa hadi wa chini, tunaomba utujalie heri na salama.

"Nchi iwe na heri kubwa, iliyoongozwa na Nyerere alifanya kazi kubwa na kwa kazi ya uadilifu leo unatuona tupo mbele yako tunakuomba uendelee kutujalia amani," alisema.

Sheikh Mshangani alisema Mwalimu Nyerere alikuwa na huruma na uadilifu, hivyo kutokana na uadilifu huo wanamwombea Rais na watendaji wake awaondolee balaa na waongoze bila kutishwa.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Lindi, Bruno Ngonyani, akiliwakilisha Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC), alisema kwa miaka mingi Watanzania wameishi kwa amani na upendo.

"Tumeishi kwa uelewano na upendo, siyo kwamba upendo umekuwa mkamilifu la hasha, upendano tunaweza kuuongeza ziadi na zaidi na mshikamano tunaweza kuuongeza lakini tukilinganisha na nchi nyingine za jirani tunaona sisi umetupenda kwa namna ya pekee.

"Tunataka tudumishe umoja huo, mshikamano huo na upendo huo ambao Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alikuwa ametuanzishia," alisema.

Aidha, Askofu Ngonyani alimwomba Mungu kwa ustawi wa nchi na kwa maendeleo ya kila mmoja awaangalie vijana wakiwamo waliokimbiza Mwenge wa Uhuru kwa yale wanayoyatamani wayapate kwa kushughulika kwa kutumia nguvu zao kwa ajili ya kujijenga wao, taifa na ulimwengu.

Mchungaji Patrick Simwinga, kwa niaba ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), alimwombea kwa Mungu Rais Magufuli ili aendelee kumpa hekima, afya njema pamoja na viongozi waliopo madarakani waongoze katika haki ili nchi iishi kwa amani na utulivu.

Pia aliwaomba wananchi wajitokeze kwenye uandikishaji wa daftari la kudumu la mpiga kura katika hatua hiyo ya kwanza ambayo ndiyo itawezesha kupiga kura na kuchagua viongozi.

# Vijana wafundwa kuyaishi mazuri ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere

**Na Munir Shemweta, BUTIAMA**

**"Niwaombe vijana kutumia hazina ya wazee wetu na kuwa chachu ya kuishi kwa vitendo. Mwalimu alikuwa kielelezo cha uongozi bora na maisha yenye maadili, hivyo hatuna budi kuyaisha yale mazuri aliyoyafanya," alisema.**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka vijana kujifunza maisha ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kwa vitendo ili matendo ya kiongozi huyo wa kwanza wa Tanzania yaendelee kukumbukwa.

Dk. Mabula alisema hayo jana kwenye maadhimisho ya miaka 20 ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere katika Kanisa Katoliki la Bikira Maria Jimbo la Musoma, Parokia ya Butiama mkoani Mara.

Alisema ni vyema vijana wa kitanzania wakatumia hazina ya wazee kama Mwalimu Nyerere kuwa chachu ya kuishi kwa vitendo.

"Niwaombe vijana kutumia hazina ya wazee wetu na kuwa chachu ya kuishi kwa vitendo. Mwalimu alikuwa kielelezo cha uongozi bora na maisha yenye maadili, hivyo hatuna budi kuyaisha yale mazuri aliyoyafanya," alisema.

Dk. Mabula ambaye alikuwa Mkuu wa Kwanza wa Wilaya ya Butiama, alihitimisha salamu zake kwa kuwataka wananchi kuishi pia kwa kumcha Mungu kwa kuwa wakati wa uhai wake, Baba wa Taifa aliishi kwa kumcha Mungu.

Naye Waziri Mkuu mstaafu, Joseph Warioba alisema Mwalimu Nyerere alikuwa ni mtu wa maisha ya kumcha Mungu na mtu aliyejitahidi kujenga umoja na mshikamano kwa Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Phillip Mangula, alimwelezea Mwalimu Nyerere kuwa mtu aliyepigania haki na aliyesisitiza kuwa binadamu wote ni ndugu na Afrika ni moja.

Maadhimisho ya miaka 20 ya kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere katika Kanisa Katoliki Parokia ya Butiama yalihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima; Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Stephen Wasira; Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo na Chifu Joseph Wanzagi.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

KODI YA MAJENGO

Viwango sasa ni rafiki, unaweza kulipa kwa simu yako!
Wahi ukalipe sasa ili kuepuka usumbufu!



Tshs.10,000/=
Jengo la kawaida

Tshs. 20,000/=
Ghorofa zima katika Halmashauri ya Wilaya

Tshs. 50,000/=
Kila sakafu ya ghorofa katika Majiji,Miji na Manispaa

Wahi ukalipe sasa!

"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

Piga simu bure: 0800-750075 au 0800-780078
Barua pepe: huduma@tra.go.tz
WhatsApp Namba: 0744-233-333

215460602



Enabel

PUBLIC TENDER Ref: TAN 133

Constructions of KALALANGABO FISHING LAND SITE

Enabel, The Belgian Development Agency, works in partnership with the ministry of Natural Resources and Tourism in implementation of Natural Resources and Management Project in Kigoma Region **(NRM LED)** is now inviting suitable and Qualified Constructors to apply for the public tender for works for the constructions of Kalalangabo fishing site in kigoma region.

Details for this tender which include Tender documents and all relevant details are available in enabel webite at: **www.enabel.be** and **https://btctanzania.wordpress.com**/

All local companies and all Contractors are invited to visits the website and apply:

215456202

## HABARI KITAIFA

# Necta yapata dawa ya waghushi vyeti

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Mitihani (Necta) limesema kutokana na mabadiliko makubwa liliyoyafanya, limeanza kutoa vyeti vya kisasa ambavyo hakuna mtu mwenye uwezo wa kughushi kama zamani.

Katibu Mtendaji wa Necta, Dk. Charles Msonde, alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye mahafali ya 15 ya shule ya msingi Tusiime, Tabata jijini Dar es Salaam.

Dk. Msonde alisema Necta imefanyakazi kubwa kuweka mifumo mizuri ya kudhibiti watu wanaopenda kughushi vyeti vyake na kwamba atakayefanya hivyo kwa sasa atatambulika kwa haraka kutokana na mifumo thabiti iliyowekwa.

"Ukija Necta utaona kazi kubwa inayofanywa pale, kuna mambo makubwa sana yamefanyika na hivi vyeti kuanzia vya darasa la saba vimewekwa alama nyingi maalum ambazo katika hali ya kawaida huwezi kuziona ila sisi tukiweka kwenye mashine zetu tunaona kwa haraka," alisema Dk. Msonde.

Alisema wataalamu wa Necta wamekuwa wabunifu kwa kuweka mifumo mbalimbali ambayo inarahisisha kubaini vyeti ambavyo vitakuwa vimeghushiwa na kwamba hiyo ilisaidia pia kuwabaini watumishi waliokuwa na vyeti vya aina hiyo.= "Vyeti tunavyotoa hivi sasa ni vya kisasa na ninaweza kuhakiki cheti cha mtu kama ni halali au kaghushi hapa hapa kwa kutumia simu yangu. Naandika namba yake inaniletea jina lake, picha yake na shule aliyosoma na picha. Kwa hiyo kama ameghushi nambaini haraka nikiwa hapa hapa," alisema.

Dk. Msonde alisema ubunifu mkubwa wa watumishi wa Necta ndio umeiwezesha taasisi yake kuchaguliwa kuwa baraza bora la mitihani Afrika na ndiyo sababu imepewa jukumu la kuongoza taasisi kama hizo Afrika Mashariki.

Alisema katika kurahisisha usajili wa wanafunzi wa shule za msingi kwa ajili ya mitihani, baraza hilo limeamua kuwapa majukumu hayo walimu wakuu wa shule zote ambao ndio wanajua idadi na majina sahihi ya wanafunzi walio nao. Alisema Necta ilianzisha mfumo uitwao 'Primary School Education Management (PREM)' na kuwapa jukumu la kusimamia usajili wa walimu wakuu ili kuondoa matatizo ya kukosewa majina ya wanafunzi yaliyokuwa yakijitokeza awali.

"Tuna zaidi ya shule za msingi 18,000 na sasa tumeona tukiruhusu kila mtu aje Necta itakuwa vurugu. Kwa hiyo walimu wakuu hakikisheni mnasajili wanafunzi wenu kwa ufasaha msikosee majina maana mkifanya hivyo inaleta shida baadaye," alisema

"Unasajili jina la mwanafunzi leo anafika darasa la nne anafanya mitihani tunatoa matokeo unakuja kwetu unasema jina limekosewa. Sasa aliyekosea ni nani? Baraza au wewe?" alihoji Dk. Msonde

Alitoa mfano kuwa mwanafunzi anapofika darasa la saba na kutaka kusajiliwa kwa ajili ya mitihani, mwalimu mkuu anapaswa kuweka namba aliyotumia kujisajili alipokuwa darasa la nne kwa kuwa italeta jina sahihi alilojiandikisha nalo wakati huo.








Mwendesha mkokoteni akiwa ameusheheni madumu matupu ya plastiki katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC Dom atinga kanisani kuhamasisha uandikishaji

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAKATI muda wa uandikishaji wa daftari la orodha ya wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa ukiongezwa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameingia kanisani kuhamasisha wananchi kujiandikisha.

Huku Dk. Mahenge akifanya hivyo, viongozi wenzake ngazi ya wilaya waliingia mitaani kwa ajili ya kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwenye mchakato huo.

Mkuu huyo wa Mkoa alifanya hivyo Jumamosi iliyopita alipoingia kwenye Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA) Dodoma Kati. Licha ya kuhamasisha watu kujiandikisha, pia aliwataka kujitokeza kwa wingi kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Alisema mkoa wa Dodoma unakadiria kuwa na watu milioni 2.3 na wanaotarajiwa kujiandikisha ni milioni 1.2 kwa ajili ya uchaguzi huo.

"Mpaka sasa tumeandikisha watu 468,000 hivyo tuko chini ya nusu. Katika wilaya zote wilaya iliyofanya vizuri ni ya Kongwa, nimeona niwakumbushe badala ya kukaa mitaani na kupata kiongozi ambaye hatukumtaka. Tunayo nafasi sasa ya kwenda kujiandikisha na kwenda kupiga kura," alisema.

Aliwataka wasiwaachie watu wengine kuwafanyia uamuzi wa kuchagua viongozi bali waende wenyewe kuchagua wanaowataka.

"Uongozi bora si jambo dogo unaweza kuwa na Rais bora, lakini kiongozi wa chini akiwa si bora. Nawaomba mkajiandikishe mshiriki uchaguzi kwani kujiandikisha hakuchukui hata dakika mbili," alisema.

Mbali na Dk. Mahenge, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alitembea mtaa kwa mtaa kuhamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha katika daftari hilo.

Shekimweri aliwahimiza wananchi kutumia siku tatu zilizoongezwa ili kila mtu ashiriki na kwamba maendeleo yoyote yanaanzia ngazi ya kijiji, hivyo ni wajibu wa wananchi kujiandikisha ili wapate fursa ya kuchagua viongozi waadilifu na wenye kasi kama ya Rais John Magufuli.

Juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alitangaza kuongeza siku tatu kwa ajili ya uandikishaji hadi keshokutwa.

**DAR MAMBO MOTO**

Wakati hali ikiwa hivyo mkoani Dodoma, jijini Dar es Salaam mambo yalipamba moto kuanzia juzi kwa magari kupita mitaani kuhamasisha wananchi kujitokeza ili kujiandikisha.

Magari hayo yalipita katika mitaa mbalimbali tangu asubuhi hadi usiku huku matangazo yakisisitiza wananchi wafike katika vituo vya kujiandikisha.

Mbali na kuhamasisha kwa njia za matangazo mbalimbali kupitia magari, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alitangaza kuwa jana maduka yasifunguliwe hadi saa 5:00 asubuhi ili kupisha mchakato huo.

Dar es Salaam ni moja ya mikoa ambayo ilitangazwa wiki iliyopita na Jafo kwamba uko nyuma katika uandikishaji ukiwa na asilimia nane tu, hatua ambayo waziri huyo alisema mikoa itakayofanya vibaya katika mchakato huo, atawasilisha dokezo kwa Rais kwa ajili ya kuchukua hatua.

**NDIKILO AKEMEA UBAGUZI**

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amewataka wananchi kuishi kwa upendo na kuacha kubaguana kwa misingi ya ukabila na udini.

Ndikilo alisema hayo jana wilayani Rufiji katika kata za Muhoro na Ikwiriri wakati akihamasisha wananchi kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi huo.

Alifikia hatua hiyo baada ya kujitokeza changamoto ya ubaguzi katika uandikishaji kwenye baadhi ya wilaya za mkoa huo baada ya baadhi ya watu kuwakataa watu wa jamii ya wafugaji kujiandikisha kwa madai kuwa ni wageni wahamiaji, hivyo hawastahili kujiandikisha licha ya kuwepo kwenye maeneo hayo kwa muda mrefu.

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# HESLB yawataka waombaji mikopo kukamilisha nyaraka

**Na Mary Geofrey**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imewataka wanafunzi 4,794 ambao wamekwama kukamilisha maombi yao kuendelea kwa kuambatisha nyaraka muhimu mtandaoni kabla ya kutangaza rasmi majina ya wanufaika wote keshokutwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema wametangaza hatua hiyo baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa maombi ya mikopo ya wanafunzi 55,444 ambao wamepata udahili katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu nchini.

Badru alisema wanafunzi watakaopangiwa mikopo watapata taarifa zao kupitia akaunti zao kwenye mtandao wa taasisi hiyo.

"Tulitoa siku sita ambazo zinakamilika kesho (leo), lakini bado kuna hao ambao tunawaona katika mfumo kuwa bado hawajakamilisha. Inawezekana wako ambao hawahitaji tena mkopo, lakini inawezekana wako wahitaji wa kweli kwa hiyo tumeamua hatutafunga mfumo wetu na wanaweza kuendelea kukamilisha," alisema Badru.

**"Tulitoa siku sita ambazo zinakamilika kesho (leo), lakini bado kuna hao ambao tunawaona katika mfumo kuwa bado hawajakamilisha. Inawezekana wako ambao hawahitaji tena mkopo, lakini inawezekana wako wahitaji wa kweli kwa hiyo tumeamua hatutafunga mfumo wetu na wanaweza kuendelea kukamilisha," alisema Badru.**

"Wanaweza kuingia katika akaunti zao na kukamilisha lakini kwa wale ambao watafika vyuoni wakiwa bado hawajakamilisha, tunakutana na maofisa mikopo Ijumaa mjini Morogoro na wawahudumie wanafunzi hawa wakiwa vyuoni kwa kupokea nyaraka zinazokosekana na kuziwasilisha kwetu ili wote wenye uhitaji wapangiwe mkopo," aliongeza.

Kwa mujibu wa Badru, utoaji wa mikopo pia huzingatia makundi maalum kama yatima waliowasilisha nakala za vyeti vya vifo vya wazazi, wenye ulemavu walioambatisha barua kutoka kwa wanganga wakuu wa wilaya au mkoa na waombaji mkopo ambao kutokana na hali duni ya kiuchumi, walifadhiliwa katika masomo yao ya sekondari au stashahada.

Kuhusu malengo ya mwaka huu, Badru alisema serikali imetenga Sh. bilioni 450 ambazo zitawanufaisha wanafunzi 128,285.

Alisema kati ya hao, zaidi ya wanafunzi 45,000 watakuwa wa mwaka wa kwanza na wengine 83,285 ni wanufaika wa mikopo wanaoendelea na masomo.

Alisema bajeti ya mwaka wa masomo 2018/19 ilikuwa Sh. bilioni 427.5 na iliwanufaisha wanafunzi 123,329.



Baadhi ya wataalamu kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Ofisi ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Musoma, wakipima eneo litakapowekwa bomba la maji kutoka Ziwa Victoria, mkoani Mara, na kusambazwa katika baadhi ya vijiji vya Musoma, kupitia mradi wa maji wa maziwa makuu ulioanza wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ahamasisha urasimishaji ardhi

**Na Munir Shemweta, ILEMELA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (pichani), amewataka wananchi kuchangamkia urasmishaji unaoendelea nchini ili kuwa na umiliki halali wa ardhi, hivyo kuitumia kujiletea maendeleo.

**"Wananchi walijenga kwa nguvu zao na serikali haikuwa makini katika kupanga maeneo ili watu wakae katika mpangilio mzuri, hivyo Rais aliagiza wananchi warasmishiwe ili wawezeshwe kiuchumi na kutumia ardhi yao na majengo kuendelea katika shughuli za uchumi na kuweka dhamana. Kazi hii ya urasmishaji inafanyika kwa miaka 10 na kumalizika mwaka 2023," alisema.**



Dk. Mabula, ambaye ni Mbunge wa Ilemela mkoani Mwanza, alisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita alipozungumza na wananchi wa jimbo hilo katika Mtaa wa Kabanganya, akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika Kanda ya Ziwa.

Alisema Rais John Magufuli ameelekeza maeneo yote yaliyokuwa katika ujenzi holela yarasmishwe kwa kupimwa ili wananchi wawe na umiliki halali kwa kuwa walitumia nguvu nyingi wakati wa kuyaendeleza.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, kupimiwa pekee katika maeneo yaliyorasmishwa hakutoshi na kushauri wananchi kuhakikisha wanapata hati za umiliki ili kuzitumia katika kujipatia mikopo na shughuli zingine za maendeleo.

"Wananchi walijenga kwa nguvu zao na serikali haikuwa makini katika kupanga maeneo ili watu wakae katika mpangilio mzuri, hivyo Rais aliagiza wananchi warasmishiwe ili wawezeshwe kiuchumi na kutumia ardhi yao na majengo kuendelea katika shughuli za uchumi na kuweka dhamana. Kazi hii ya urasmishaji inafanyika kwa miaka 10 na kumalizika mwaka 2023," alisema.

Akizungumzia shughuli za maendeleo katika jimbo la Ilemela, Dk. Mabula alisema tangu achaguliwe kuwa Mbunge, amefanya mambo makubwa katika sekta ya elimu kwa kuwezesha ujenzi wa shule za msingi na sekondari sambamba na kuongeza vyumba vya madarasa kwa baadhi ya shule hizo tofauti na miaka ya nyuma.

Dk. Mabula pia aliwaambia wananchi wa Mtaa wa Kabangaja kuwa hivi sasa jitihada zinafanyika kuondoa tatizo la maji katika mtaa huo na mitaa mingine ya jimbo hilo. Alisema tayari timu ya wataalamu iko katika mtaa huo kuhakikisha inakamilisha uwekaji miundombinu ya maji.

Baadhi ya wananchi wa mtaa wa Kabangaja, walimweleza Dk. Mabula kuwa wanakabiliwa na tatizo la maji katika maeneo yao ingawa mtaa wao ndio chanzo cha maji kwenda maeneo mengine.

Mkazi wa Kabangaja, Aziz Said, alimweleza Naibu Waziri kuwa pamoja na uwapo wa upimaji shirikishi katika eneo hilo, hadi sasa bado hawajapatiwa hati za umiliki wa maeneo yao jambo lililofafanuliwa na Ofisa Mipango Miji na Ardhi kutoka Manispaa ya Ilemela, William Magoha, kuwa limesababishwa na baadhi ya wananchi kushindwa kukamilisha fedha za upimaji.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## TENDER INVITATION

Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) invites tenders from eligible, reputable and competent tenderers for **DUST CONTAINER HANDLING SERVICES**

**TENDER INSTRUCTIONS AND CONDITIONS**

1. Tender documents in English language shall be collected from Procurement Offices from 9AM to 4PM, between 18th October 2019 and 22th October 2019. Tender documents are issued free of charge.

   Or Request tender through Saphiness.kikwesha@heidelbergcement.com, Telephone number 0785 670 641 and dickson.malinzi@twigacement.com Telephone number 0785 670 646
2. TPCPLC is not responsible for any costs related to printing of the bids to be submitted by the tenderers.
3. Tenderers must submit well printed bids in a properly sealed envelope by hand and presented in ONE COPY addressed to:

   **Head of Procurement Cluster III,**
   **Tanzania Portland Cement Company Limited,**
   **P.O. Box 1950,**
   **Dar es Salaam.**
4. Deadline for tender submission shall be 29Th October 2019 before 4PM. late bids shall not be accepted.
5. Tender envelopes must be clearly marked with the relevant tender.
6. Bids MUST be in Tanzania Shillings.
7. Bids should be valid for a period of 90 working days from the date of submission deadline.
8. TPCPLC in not bound to accept the lowest bid or any bid.
9. Sites visits are MANDATORY for all interested tenderers.
10. Documents to be submitted with tender documents include;
    i. Copies of Certificate of Incorporation/Registration/TIN/VRN and valid Business License.
    ii. Copy of tax clearance certificate from Tanzania Revenue Authority
    iii. Letters of recommendation from 3 current major clients.
    iv. Certified bank statement for the month of April 2019 (1st to 31st May 2019)
    v. Safety compliance documents
    vi. Only short listed Companies will be contacted

215459602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni miaka 20 kuendelea kutomwona Mwalimu

**VONGOZI** mashuhuri kama Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kazi, maono na fikra zao haziwezi kufa, bali wanaendelea kuishi. Ndiyo maana shujaa Nyerere aliyevuta pumzi yake ya mwisho Oktoba 14, 1999, hata leo anaishi.

Viongozi kama hawa japo wamefariki dunia kile walichofanya kwa ajili ya mataifa yao kinaendelea kuimarika na kuwa bora kila siku na kila wakati.

Nyerere anaendelea kuishi kwa kuwa kazi zake alizozifanya kila wakati zinang'ara na kuimarika siku hadi siku licha ya kwamba hayupo tena.

Mathalani, vyuo vikuu alivyojenga kuanzia Dar es Salaam na Sokoine, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro na Dar es Salaam, Bandari za Dar na Tanga. Kazi hizo chache ni miongoni mwa mamia ya mambo aliyofanya Mwalimu Nyerere ambayo kila siku yanazidi kung'ara na kuwa mapya kila uchao.

Ndiyo maana tunasema kiongozi huyu mashuhuri na watendaji aliyefanyakazi zilizotukuka kama Nyerere na aliyekuwa anajiamini hafi na wala hasahauliki.

Kwa hiyo tutaendelea kusema Nyerere ni kiongozi mahiri, mwenye weledi, jasiri, rafiki wa Watanzania na Waafrika wote, imara na aliyeongoza kimkakati.

Kama taifa, tutaendelea kumwenzi Nyerere kwa kuwa ameyaongezea thamani maisha ya Watanzania kuanzia mwaka 1961 hadi 1999 akiwa mstari wa mbele kujenga shule, kulinda rasilimali, kuanzisha viwanda, kilimo cha kisasa, kujenga hospitali, barabara, kuanzisha miradi ya umeme na mashirika ya umma ili kuwahudumia Watanzania.

Yote hayo yameongeza thamani katika maisha ya kila mmoja ndiyo leo tunamwita shujaa na mpiganiaji maarufu wa haki za wananchi, amani, usawa na maendeleo.

Licha ya kwamba shujaa huyu alivuta pumzi yake ya mwisho Oktoba 1999 , hadi leo anaishi na ametuachia ujumbe unaotuhamasisha sisi na viongozi wote wa Afrika kumuiga kwa mambo mema na makuu aliyolifanyia taifa.

Watanzania licha ya kifo kututenganisha naye, hatuna kinachotufanya tusikitike kwani tuna hazina ya kazi zake na mambo makubwa aliyoyafanya yanayotufanya tutembee kifua mbele na kuringa kuwa kama taifa tuna zawadi kubwa ya kiongozi ambaye amezaliwa na kukulia katika ardhi yetu.

Nyerere ametuachia urithi (legacy) kwa taifa zima na Afrika. Tunajivunia Watanzania tunaye baba anayeheshimika kwa kazi kubwa za ndani na nje ya mipaka yetu.

Tunajivunia kuwa na kiongozi mwenye nidhamu ya hali ya juu aliyefanyakazi kwa bidii zote, asiyechoka kuwahudumia Watanzania na Afrika nzima.

Tunaposherehekea maisha yake tunaendelea kumuona Nyerere aliyekuwa na maadili na utaratibu wa kipekee katika kujenga nchi kwa misingi ya amani, uzalendo heshima na upendo ambavyo hadi sasa vinaendelea kuonekana na kusimamia kazi zake.

Tutaendelea kumuenzi Baba wa Taifa, kwa kuwa ndiye mbunifu na mchora ramani ya taifa letu tena ndiye sababu wa ushindi na mafanikio yote yanayoonekana Tanzania leo.


Tunamheshimu kwani ndiye aliyeweka misingi ambayo viongozi wengine wameisimamia na kuliwezesha taifa kusimama na kuendelea kuimba wimbo wa ushindi na maendeleo.


Tunapokumbuka kifo chake na kukumbuka maisha aliyoishi tunaendelea kumpongeza Nyerere kuwa alikuwa shujaa na kamanda mwaminifu ambaye hata siku moja hakukimbia mapambano ya kisiasa.

Alipigania kuwe na hali bora ya uchumi duniani, akigombana na mabeberu na wanyonyaji bila kuwajali au kuwaogopa pale alipoona wamekwenda kinyume na kuikandamiza Afrika. Ushujaa wake ndiyo tunaoutumia hadi sasa kuwa na misimamo ya kulinda na kutetea rasilimali zetu kama gesi, madini ardhi ili zitunufaishe na si kuwatajirisha mabeberu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni wakati sasa kilimo kiwe na asilimia 10 ya bajeti

Na Raphael Kibiriti

**WAKULIMA** hasa wadogo nchini ni moja ya kundi linaloonekana kuwa na watetezi wengi.

Si watu binafsi, taasisi au mashirika tu, lakini majukwaa mbalimbali, kama vile Jukwaa la Asasi za Kilimo (ANSAF) na Shirika la Mapinduzi ya Kijani kwa nchi za Afrika (AGRA).

Haya yote yanalenga kuwasemea, kuwatetea na kuwapigania wakulima kutoka pande zote ili maisha yao yastawi kutokana na kazi hiyo muhimu wanayoifanya kwa maslahi ya taifa.

Lakini ukiachana na mashirika hayo yenye lengo la kuwa na sera, sheria na kanuni zinazomnufaisha mkulima, pia kuna kundi la wanasiasa.

Kundi ambalo linawajumuisha madiwani, wabunge, mawaziri na watendaji wengine wa serikali kama vile makatibu tarafa, wakuu wa wilaya na wa mikoa, bila kusahau viongozi wa kitaifa kwa maana ya rais na wasaidizi wake wakuu.

Kundi hili nalo limo miongoni mwa makundi yanayoonekana 'kuwapigania' wakulima.

Lakini pengine swali ni kwa nini wanafanya hivyo?

Kwa mashirika na asasi mbalimbali, wanafanya hivyo katika kutimiza malengo yao ya kuona wakulima wanastawi kimaisha.

Lakini kwa upande wa wanasiasa, Muungwana anaona wana sababu mbalimbali, lakini kubwa zaidi ni ile ya kutimiza malengo ya kisiasa vilevile.

Hii ni kwa sababu kilimo kinabaki kuwa sekta muhimu katika kuchagiza uchumi na maendeleo ya taifa kwa ujumla wake.

Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, kilimo kinatoa ajira kwa takribani asilimia 75 ya Watanzania, huku kikichangia zaidi ya asilimia 100 ya chakula kinachozalishwa nchini.

Hivyo, hatua ya wanasiasa kuwatetea wakulima inaweza ikawa ni katika kukidhi malengo ya kisiasa, kwa msingi kuwa ndiyo sekta iliyoajiri sehemu kubwa ya Watanzania.

Kwamba asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima, wengi wao wakiwa wadogo wadogo, ni mtaji mkubwa kwa wanasiasa.

Ni kundi kubwa la wapigakura ambalo linaweza likamweka na kumtoa madarakani mwanasiasa yeyote yule na ndiyo maana haiwi ajabu kuona karibu kila mwanasiasa anajaribu kulionyesha kuwa bado analipigania.

Ni katika muktadha huo ndipo Muungwana anapoibuka kulonga, sana sana akielekeza mtazamo wake kwa wanasiasa hawa hawa ambao wawapo majukwaani ama kwenye kumbi zao za udiwani ama bungeni, hujipambanua kuwa watetezi wa kundi hili.

Tena wakati mwingine wakionyesha kuwa na hasira pale inapoonekana wakulima 'wao' wanapuuzwa.

Sasa Muungwana anawauliza wanasiasa hawa kuwa, kama wako tayari hata kukamata shilingi ya Waziri wawapo bungeni, ama kupiga kura ya kufukuza watendaji wa halmashauri za wilaya, miji, manispaa ama za jiji, iweje hadi leo hii, bado bajeti inayotengwa kwa ajili ya kilimo si kwa kiwango cha kuridhisha?

Tena wakati wao wakiwa ndio wahusika wa bajeti ya serikali?

Ikumbukwe kuwa Umoja wa Afrika kupitia NEPAD, waliasisi Programu ya Kuendeleza Kilimo mwaka 2003 (CAADP), kwenye mkutano uliofanyika jijini Maputo nchini Msumbiji.

> **Ni kundi kubwa la wapigakura ambalo linaweza likamweka na kumtoa madarakani mwanasiasa yeyote yule na ndiyo maana haiwi ajabu kuona karibu kila mwanasiasa anajaribu kulionyesha kuwa bado analipigania.**

Katika mkutano huo, viongozi hao walikubaliana kutenga asilimia 10 ya bajeti za nchi zao kwenye sekta ya kilimo na maendeleo vijijini.

Muungwana alitegemea basi wanasiasa waonyeshe kweli kuwa ni watetezi wa kundi hili kubwa la Watanzania, kwa kupigania bajeti ya kilimo ifikie hiyo asilimia 10 iliyokubaliwa kwa ajili ya kilimo.

Hivyo ni rai ya Muungwana kwa wanasiasa na watendaji wengine wa serikali kuwapigania wakulima na hasa wadogo wadogo kidhati, kwa kuhakikisha bajeti ya kilimo inakuwa ni asilimia 10 ya bajeti yote ya serikali.

Hilo likifanyika, wakulima wataondokana na mazonge yanayowakwamisha, kama yale ya tija ndogo katika uzalishaji, utegemezi wa mvua, huduma za ughani zisizoridhisha, miundombinu hafifu, ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao, uzalishaji na teknolojia hafifu ya kilimo.

Hilo likifanyika wakulima hawatahangaikia masoko ya mazao yao kama ilivyo kadhia inayoendelea ya baadhi ya wakulima wa pamba kutolipwa fedha zao hadi sasa.

# Serikali yaagiza mradi wa Star City upewe hati

Na Mwandishi Wetu

WIZARA ya Viwanda na Biasahara imeagiza kutolewa hati kwa eneo la mradi mkubwa wa Star City kwenye Manispaa ya Morogoro uliokwama kuanza uwekezaji kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo hatimiliki.

Mradi huo ulisajiliwa mwaka 2016 na Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA) kwa ajili ya kupokea wawekezaji katika viwanda na miradi mingine, lakini ilishindikana kutokana na kukosa hati.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Prof. Joseph Buchweishaija, alitoa agizo hilo katika kikao kazi kilichofanyika mjini hapa ambacho kilihudhuriwa pia na makatibu wakuu wa wizara nyingine, uongozi wa Mkoa wa Morogoro na mamlaka ya EPZA.

"Hatupo tayari kuona mradi huu unacheleweshwa tena na mtu au taasisi kwa sababu yoyote ile. Kila mmoja hapa ni lazima atimize wajibu wake ili kuufanya mradi huu uanze kazi haraka kabla ya mwisho wa mwaka," alisema.

Prof Buchweishaija aliiagiza Manispaa ya Morogoro kukamilisha upimaji wa eneo hilo lenye ukubwa wa hekta 4314 (ekari 10,661) ndani ya wiki tatu na pia kupatikana kwa hati ya eneo hili.

Katika kikao hicho, maofisa mbalimbali wa serikali waliowakilisha taasisi za Mamlaka ya Majisafi na majitaka ya Mkoa wa Morogoro (Moruwasa), Shirika la Umeme nchini (Tanesco) na Wakala wa Barabara Vijijini (Tarura), kuhakikisha wanatengeneza mpango maalum kwa haraka na kuwa tayari mwanzoni mwa mwezi ujao utakaowezesha kuweka miundombinu wezeshi katika eneo hilo la Ukanda Maalum ya kiuchumi ya Star City.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Kanali mstaafu Joseph Simbakalia, alisema ardhi ni kiungo muhimu sana katika kuvutia uwekezaji hasa kwenye viwanda na hivyo ucheleweshaji wa hati katika eneo la Star City imekuwa kikwazo kikubwa katika kuendeleza eneo hilo.

Eneo hilo la Ukanda maalum ya Kiuchumi la Star City linamilikiwa na kampuni ya kitanzania ya Dominion Plantation Limited (DPL) kwa hisa 51 na kampuni ya Hyflux Limited kutoka Singapore kwa asilimia 49.

Simbakalia alisema EPZA ni mkono wa serikali ambao unashiriki kwa karibu kuandaa mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji katika viwanda.

Alisema pia kuwa mradi wa treni ya umeme ya Standard Gauge, ambao utapita katikati ya mradi utaunganisha bandari kavu itakayojengwa katika eneo hilo la ukubwa wa ekari 500.

Alisema bado mazungumzo yanaendelea na wawekezaji wa viwanda vingine vitatu ili kuwekeza katika eneo hilo.

Meneja Mkuu wa mradi wa The Star City, Annath Bhat alisema wamepokea maombi mengi kutoka kwa wawekezaji wakitaka kuwekeza katika eneo hilo maalum, lakini ucheleweshaji wa hati umekuwa kikwazo.

"Tunaiomba serikali ikamilishe utoaji wa hatimiliki ili mradi huu uweze kuanza mapema na kuleta wawekezaji wengi zaidi," alisema.



Mkazi wa Mtaa wa Somanda, Anastazia Magesa (katikati), akijiandikisha katika daftari la mpiga kura katika kituo cha uandikishaji cha mtaa huo, mjini Bariadi, mkoani Simiyu jana. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

## Serikali yataka watumishi wakapigwe msasa TPSC

Na Mwandishi Wetu, TANGA

SERIKALI imewataka waajiri wote nchini kukitumia Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) kuwaendeleza watumishi wao katika maeneo ya mafunzo msasa na mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya ili kuongeza ufanisi sehemu za kazi.

Akizungumza jijini hapa mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 31 ya TPSC, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Francis Michael, alisema mafunzo hayo ni muhimu sana katika kuwawezesha watumishi wa umma kufanya kazi zao kwa weledi.

Alisema iwapo watumishi wa umma watapitia katika chuo hicho, watapata mafunzo ya kujiandaa kustaafu, mafunzo ya usimamizi wa ofisi, mafunzo ya usimamizi wa nyaraka kwa njia ya Tehama, mafunzo ya OPRAS na mafunzo ya maadili na huduma bora kwa wateja.

Alisema ni muhimu chuo kuunga mkono juhudi za serikali za ujenzi wa uchumi wa viwanda na Tanzania yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 kwa kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu wenye lengo la kutatua changamoto mbalimbali nchini.

"Ni matumaini yangu kuwa aina ya mafunzo na ushauri wa kitaalamu mnaoutoa unaenda sambamba na maboresho katika sekta ya umma na kuwawezesha watumishi wa umma na watarajiwa kukabiliana na changamoto mbalimbali," alisema.

Mkuu wa chuo hicho, Dk. Emmanuel Shindika, alibainisha kuwa katika mahafali hayo, jumla ya wahitimu 6,151 walitunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali.

Dk. Shindika alisema kwa mwaka 2018/2019, watumishi wa umma 4,116 walihudhuria mafunzo mbalimbali chuoni hapo na kwamba matarajio ya mwaka huu, watumishi 6,060 watapatiwa mafunzo.

Alisema chuo kinaendesha mafunzo ya ngazi ya shahada ya kwanza katika fani za menejimenti ya kumbukumbu na uhazili katika kampasi ya Dar es Salaam.

Alisema mwaka 2018/2019, wanafunzi 238 walidahiliwa na kusajiliwa wakati mwaka huu wanatarajia kudahili wanafunzi 438.

"Tunaimarisha miundombinu na kuhisha mitaala iendane na kasi ya mabadiliko ya sasa ya ukuaji wa uchumi na uendelezaji wa viwanda," alisema.

Aliongeza kuwa wanakusudia kukamilisha ujenzi wa kituo cha mafunzo kwa watumishi wa umma Dodoma na kuendelea na ujenzi wa jengo ghorofa tatu katika Kampasi ya Tabora.

Chuo kina matawi sita ambayo ni Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Mbeya na Tanga.

## Wastaafu washauriwa kufuga samaki

Na Dotto Mwaibale, SINGIDA

WASTAAFU wameshauriwa kufuga samaki ili kupata chakula chenye lishe bora na kuinuka kiuchumi badala ya kutegemea fedha za kiinua mgongo pekee.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Juma Mkhofoi, mfugaji mkubwa wa samaki mkoani Singida, alipozungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani ambayo kitaifa yanafanyika Uwanja wa Bombadia mjini hapa.

"Niwaombe wastaafu wenzangu wasikae bure na kutegemea kiinua mgongo pekee kuendesha maisha yao bali wafuge samaki kwani watapata kitoweo chenye lishe bora na fedha za kujikimu," alisema.

Mkhofoi alisema gharama za ufugaji wa samaki ni ndogo na soko lake ni kubwa tofauti na kilimo ambacho kinahitaji mambo mengi.

Aliongeza kuwa mabwawa ya samaki yanaweza kuchimbwa eneo lolote na chakula chao ni pumba ya mpunga na mahindi ambayo haizidi Sh. 5,000 kwa gunia na udavi ni Sh. 250,000 na kwamba samaki kwa bwawa moja kwa siku wanakula kilo moja tu.

Mstaafu huyo alisema baada ya kustaafu Wizara ya Maji na Umwagiliaji aliamua kuchimba mabwawa 67 kwa ajili ya kufuga samaki na kila bwawa alitumia Sh. milioni moja na sasa anafurahia ufugaji huo.

Alisema mabwawa hayo aliyachimba mwaka jana na sasa ameanza kupata matunda ya ufugaji huo kwa kuwa kuanzia mwaka jana mwishoni hadi mwaka huu mwanzoni, amepata zaidi ya Sh. milioni sita baada ya kuvua samaki na kuwauza.

"Nimeanza kupata pesa kwa kuwauza samaki aina ya sato ninaowafuga pamoja na kitoweo chenye lishe ambacho kinakubalika kwa afya tofauti na nyama zingine," alisema Mkhofoi.

Kwa mujibu wa Mkhofoi, lengo lake ni kuwa na zaidi ya mabwawa 80 na kila wiki awe anazalisha kilo 1,000 hadi 2,000 na kuwa soko lake kubwa litakuwa hapa hapa mkoani Singida na hapendi kuwauzia wafanyabiashara kwa kuwa wanaenda kuwalangua walaji ambao watashindwa kupata chakula chenye lishe bora.

**"Nimeanza kupata pesa kwa kuwauza samaki aina ya sato ninaowafuga pamoja na kitoweo chenye lishe ambacho kinakubalika kwa afya tofauti na nyama zingine," alisema Mkhofoi.**

# Wastaafu, viongozi waelezea upekee wa Mwalimu Nyerere

INATOKA UK 2

Waziri) wa Kilimo chini ya Joseph Mungai na kwamba baada ya uteuzi huo, Mungai alimtania kuwa amepata unaibu waziri kutoka shambani.

Alisema mwaka 1975 Mwalimu alimwita Ikulu akamweleza kuwa ameshauriwa na Waziri wa Mambo ya Nje, John Malecela, kuwa amteue kuwa balozi wa Zambia ingawa uteuzi huo alikataa na kumweleza sababu kuwa anapenda maendeleo vijijini.

"Mwaka huo huo, akaniita tena akaniambia uliniambia unapenda maendeleo vijijini, baada ya muda akiwa Butiama akatangaza kuwa niwe Mkuu wa Mkoa wa Mara ili kumsaidia Chifu wa wakati huo. "Hiki ndicho kipindi nilichojifunza kuhusu maisha ya Mwalimu ni hicho cha miaka saba na nusu, alikuwa anakuja sikukuu ya Pasaka na Krismasi anakaa sana. Nilijifunza alikuwa binadamu na binadamu wanazaliwa na vipaji alipewa vipaji vingi.

Unaweza ukapewa vipaji usivitumie vizuri, lakini Mwalimu alitumia vipaji vyake vizuri. Aliamini binadamu wote ni sawa, aliamini kila binadamu anastahili heshima. Alitafsiri imani hiyo katika nyanja zote na alichukia umaskini ndiyo maana aliutangaza kuwa adui," alisema.

Alisema Mwalimu Nyerere hakutaka utajiri yeye mwenyewe bali aliutaka wa kuondoa matatizo ya watu wote.

"Angekuwa anataka utajiri, angekuwa tajiri mkubwa Afrika pengine na dunia, maana migodi ipo hapa na dhahabu ipo kila mahali angechimba. Alisimamia maendeleo ya watu wote, aliamini watu wote hawawezi kuwa matajiri lakini alitaka wawe na nyumba ya kuishi, wapate chakula, elimu na matibabu," alisema. Mjukuu wa Mwalimu, Sophia Nyerere, akizungumza kwa niaba ya wajukuu wenzake, alisema babu yao aliwapenda na kuwafanya kuwa wamoja.

"Wakati babu alipokuwa hai nadhani wale wapishi waliotoka hapa wameeleza hii nyumba ilikuwa inapikwa saa 24. Sasa hivi tumekuja kwenye kumbukizi zake, hii nyumba haikai watu sana.

"Ninachokuomba Chifu wetu (Japhet Wanzagi) jaribu kuwaeleza wana ukoo na ndugu wengine warudi nyumbani, tunataka tushirikiane kumuenzi yule mzee kwa vitendo. Kwa maana hiyo tuwe tunakutana kila baada ya miezi sita," alisema.

**WAIOMBA CCM IWALEE**

Akiwasilisha ujumbe wa wajukuu wote wa Mwalimu Nyerere kwa Makamu Mwenyekiti wa CCM, Mangula, Sophia alisema wanaomba walelewe.

"Babu yetu alikuwa mwasisi wa CCM, tunaomba mtulee. Hatuwezi kumuenzi Mwalimu kwa vitendo kama ninyi wazee hamtachukua uwezo wenu mkatupa wajukuu tufanye kazi. Tukisema tuhamie Chadema mtasema sisi watukutu, mtulee kwa vitendo tusiwe tunakaa tu kwenye midahalo," alisema.

Waziri wa zamani, Prof. Sospeter Muhongo alisema Mwalimu Nyerere aliwapeleka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) lengo ni ili wanafunzi wakati huo wajue familia walizotoka ni maskini.

Katika kongamano hilo wapishi wa Mwalimu Nyerere nao walieleza wanavyoishi naye na kubwa, walimwelezea licha wakati mwingine walikuwa wakifanya makosa lakini alichukulia ni makosa ya kibinadamu na alisamehe.



Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Barclays Tanzania, Aron Luhanga (kulia), akitangaza udhamini wa benki hiyo kwa wasichana sita wenye uhitaji watakaopewa mafunzo ya ufundi stadi katika Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kutoka (kushoto) ni Mkurugenzi wa Shirika la Pact Tanzania, Marianna Balampama, Mratibu wa kozi fupi wa Veta, Mashaka Kassara na Mkurugenzi wa Huduma za Kibenki wa Kampuni wa benki hiyo, Brian Kalero. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti miradi ya Mwenge yatua Takukuru

INATOKA UK 2

kasoro hizo zilifanya ubora wa miradi hiyo kutia shaka hususani katika uimara na matumizi duni ya vifaa huku baadhi ikibainika kuwa makandarasi walikuwa hawasimamii majukumu yao vizuri huku mamlaka husika zikishindwa kuchukua hatua zozote.

Mhagama alisema baadhi ya miradi ilikutwa na ubora usioridhisha hasa ujenzi wa visima vya juu vya kuhifadhia maji ambayo kuta zake zilikuwa na nyufa hata kabla ya miradi hiyo kuanza kutumika.

"Mwenge ulikuta baadhi ya miradi makadirio ya gharama za ujenzi zilikuwa haziendani na gharama zilizoko sokoni, vitendo vinavyofanywa na wahandisi wetu katika miradi na kuhujumu fedha za Watanzania," alisema Mhagama.

Aliongeza kuwa miradi iliyozinduliwa na kuwekwa mawe ya msingi na Mwenge wa Uhuru nchini ni 1,390 yenye thamani ya Sh. trilioni 4.7.

Baada ya maelezo hayo, Magufuli alimwagiza mkuu huyo wa Takukuru kuwa: "Nataka ukafanye uchambuzi kila ukurasa, kila nukta. Nataka unipe taarifa ya miradi yenye dosari pia naamini Ofisi ya Waziri Mkuu nayo itafuatilia ripoti hii kwa maana nakujua huwa unafuatilia kweli kweli."

# Magufuli asisitiza kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa vitendo



INATOKA UK 2

Aliyataja baadhi ya mambo hayo kwa vitendo kuwa ni kupambana na rushwa kwa kuanzisha mahakama ya kushughulikia ufisadi, watumishi hewa takribani 20,000 na wafanyakazi wenye vyeti feki 14,000 kuondolewa katika utumishi wa umma.

Mambo mengine ni kutoa Sh. bilioni 23.8 kwa ajili ya elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari, kutoa Sh. bilioni 470 kwa mwaka kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu, kuboresha huduma za afya kwa kujenga hospitali mpya 69 za wilaya na vituo vya afya 352 na kuongeza bajeti ya dawa kutoka Sh. bilioni 31 hadi Sh. bilioni 270.

Pia alisema katika kuongeza kasi ya ujenzi wa viwanda, serikali imeanza ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere katika Mto Rufiji litakalozalisha megawati 2,115 kwa gharama ya Sh. Trilioni 6.5 na ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa (SGR) kwa Sh. trilioni 7.3.

Sambamba na miradi hiyo, alisema serikali inafanya upanuzi wa bandari kazi ambayo itagharimu Sh. trilioni moja, kujenga viwanja vya ndege 11, kununua ndege 11 na kununua meli mpya na kukarabati za zamani.

Aidha, Rais Magufuli alisema serikali ya awamu ya yano inamuenzi Baba waTaifa kwakuhakikisha inasimamia vizuri rasilimali na maliasili zikiwamo misitu, wanyamapori na madini kupitia sheria mpya ya mwaka 2017 ambayo imewezesha kuongezeka kwa mapato ya madini kutoka Sh. bilioni 191 mwaka 2016/17 hadi Sh. bilioni 335 mwaka 2018/19.

# RC Dom atinga kanisani kuhamasisha uandikishaji

INATOKA UK 4

"Mwalimu Nyerere alikataa ubaguzi na leo (jana) ametimiza miaka 20 tangu kifo chake. Tukianza ubaguzi hatutabaki salama mkitaka hawa waondoke wale waondoke hatutafika. Mwalimu Nyerere alituonya, hivyo tumuenzi kwa vitendo. Kubwa ni kufuata sheria ukizingatia sheria hakuna tatizo," alisema.

Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwa siku zilizobaki na kuchagua viongozi ambao watamsaidia Rais Magufuli kufanya kazi kwa kuwajali wananchi wanyonge.

Awali, mmoja wa wazee wa Muhoro, Tindwa Simba, alisema kusuasua kwa uandikishaji huenda kunatokana na kusitishwa kwa mikutano ya vyama vya siasa ambayo wananchi wengi walikuwa wakijua nini wafanye kwa viongozi wanaowachagua.

"Umuhimu wa jambo hili una maana gani? Mikutano ya vyama vya siasa imezuiwa ingawa demokrasia ilianza muda mrefu. Sasa wananchi tunaona inapindishwa," alisema.

Simba alishauri mikutano ya vyama ifanyike ili wajue viongozi wazuri na wabaya na ndiyo sababu alisema watu wengi hawakujutokeza kujiandikisha badala yake sasa wanahamasishwa hadi mashambani wakati hawajui viongozi watawafanyia nini.

**SIMIYU YASUASUA**

Mkoani Simiyu, licha ya serikali kuongeza muda wa siku tatu za kujiandikisha, mchakato huo umeendelea kusuasua katika vituo vya uandikishaji katika maeneo mbalimbali ikiwamo makao makuu ya mkoa, Bariadi.

Jana na juzi kwa mfano, baadhi ya vituo vikiwamo Izunya, Somanda, Nyaumata na Kisiwani, idadi ya watu waliojitokeza ilikuwa ndogo kulinganisha na wakazi wa maeneo hayo.

Mwandikishaji wa kituo cha Izunya, John Magolonga, alisema ndani ya muda wa siku saba uliotolewa kwa wananchi kwa ajili ya uandikishaji, mwitikio umeonekana kuwa mdogo.

Magolonga alisema katika kituo hicho, mpaka juzi waliojiandikisha walikuwa 373 huku mwandikishaji wa kituo cha Kisiwani, Nyanja Mutani, akisema mwitikio bado haujawa mzuri ingawa ana matumaini makubwa kuwa siku zilizoongezwa idadi itakuwa kubwa kwa kuwa wananchi wengi huwa wanajitokeza siku za mwisho.

***Imeandikwa na Augusta Njoji, DODOMA, Futuna Selemani, PWANI, Mwandishi Wetu, DAR na Happy Severine, SIMIYU.***

# Saccos waliosoma China yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Watanzania waliosoma China (CAAT), wamezindua chama cha kuweka na kukopa fedha (SACCOS) katika mkutano wa siku moja wa kimkakati uliofanyika Dar es Salaam, ukilenga kuwakutanisha waliosoma China ili kujadili fursa zilizopo kati ya nchi hizo mbili.

Akizungunza katika mkutano huo, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd aliyekuwa mgeni rasmi na mlezi wa jumuiya hiyo, aliipongeza CAAT kwa kuandaa mkutano huo. Alisema Tanzania kwa sasa sera zake imelenga katika kuinua uchumi wake.

Alisema ni wakati mwafaka kwa wanajumuiya hao kutumia Saccos hiyo kuanzisha biashara na viwanda kutokana na uwepo wa mazao yatokanayo na kilimo, uvuvi, ufugaji na rasilimali zilizopo.

"China kwa muda mrefu ilikua imefunga milango yake. Sasa baada ya kufungua milango yake nchi nyingi zilikimbilia kwenda kuwekeza kule. Ni dhahiri kuwa hawa ni watu very potential (muhimu) kwetu. Tutumie fursa hii kuwekeza China. Twende tukaombe vibali kuanzisha biashara zetu nchini China. Mmefungua Saccoss itumieni vizuri ili muweze kupata maendeleo yenye tija kwa mtu binafsi na kwa taifa letu, alisema Balozi Seif.

Balozi Seif ambaye aliambatana na Balozi wa China nchini, Wang Ke pamoja na balozi mstaafu wa Tanzania nchini humo, Abdulrahman Shimbo, alisisitiza jumuiya hiyo kutotumika kisiasa na kuahidi kuwa serikali itashirikiana na jumuiya kuhakikisha malengo ya jumuiya hiyo yanafikiwa.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Saccos (CAAT), Dk. Fatma-Roselyn Waziri, alieleza sababu kubwa ya kuanzishwa kwa Saccos hiyo ni fursa walizoziona China. Alisema kupitia Saccos hiyo, hisa zitanunuliwa na wataweka akiba na kukopesha wanajumuiya kama njia moja ya kuinua wanajumuiya kiuchumi. Alisema kuwa wanatarajia ndani ya miaka mitatu wanatarajia kuwa na benki.

**"China kwa muda mrefu ilikua imefunga milango yake. Sasa baada ya kufungua milango yake nchi nyingi zilikimbilia kwenda kuwekeza kule. Ni dhahiri kuwa hawa ni watu very potential (muhimu) kwetu. Tutumie fursa hii kuwekeza China. Twende tukaombe vibali kuanzisha biashara zetu nchini China...**

# Azaki zaiomba serikali unafuu wa kodi

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

JUKWAA la Wakurugenzi wa Asasi za Kiraia (Azaki) nchini, limeiomba serikali kutoa unafuu wa kodi kwa asasi hizo ili ziweze kufanya shughuli zao na kutoa mchango katika maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Hayo yamesemwa na Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa tano wa wakurugenzi wa asasi za kiraia jijini Mwanza, huku mgeni rasmi akiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliyewakilishwa na Kamishna wa Sera za Bajeti wa wizara hiyo, Shogholo Msangi.

Kauli mbiu ilikuwa "Kodi zinazohusiana na Azaki na mchango wao kwa maendeleo ya taifa".

Olengurumwa alisema, kati ya changamoto nyingi za kisheria zinazoathiri utendaji wa sekta ya Azaki ni masuala ya msamaha wa kodi hasa katika mazingira ya jinsi gani mashirika yanapata hifadhi ya hisani kwa ajili ya unufaikaji wa msamaha huo licha ya kufanya kazi nzuri ambayo ni ya kujitolea katika nyanja mbalimbali ikiwamo utetezi wa haki za binadamu, uchechemezi katika maeneo kadhaa, usambazaji wa huduma za kijamii, hivyo inapaswa mchango wao utambulike kwa kusamehewa kodi hususan inayotokana na faida.

"Sekta ya asasi za kiraia nchini ni muhimu kwani wanachangia maendeleo mbalimbali ya jamii ikiwamo kuchangia fedha za kigeni, elimu kwa kujenga shule, afya kwa kujenga zahanati, kilimo, kutoa elimu ya uraia, pia zinatoa ajira takribani 500,000 ambapo fedha wanazozipata zinatokana na wadau kutoka nje ambazo ni za msaada, hivyo inakuwa kazi kuwaambia waongeze fedha kwani wanazozitoa zinatakiwa kulipa mishahara wafanyakazi, kulipa NSSF pamoja na TRA," alisema na kuongeza:

"Hivyo tunaomba serikali kutoa unafuu wa kodi kwa baadhi ya maeneo ikiwamo kodi ya faida, tunafanya kazi ya kujitolea siyo kama mashirika mengine yanayotafuta faida."

Kamishna wa Sera za Bajeti wa Wizara ya Fedha na Mipango, Shogholo Msangi, alisema, kwa mujibu wa sheria, ni wazi kwamba pamoja na kuwapo kwa mazingira mbalimbali ya kisheria ambayo asasi za kiraia inaweza kusamehewa kodi. Na kwamba kwa ujumla zina wajibu wa kufuata matakwa ya sheria hizo ikiwamo kulipa kodi.

"Kupitia mkutano huu napenda kutoa wito kwenu wanaazaki wote kuzingatia sheria hizi kwa vitendo ili kwa pamoja tuendelee kulijenga taifa letu, ninatambua kuwa katika sheria zetu na utekelezaji wake katika taasisi husika za serikali hazikosi changamoto zinazoweza kupunguza ufanisi wenu katika kazi zenu na zoezi zima la ulipaji wa kodi," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Uratibu wa Azaki Tamisemi, Andrew Komba, alizitaka asasi za kiraia kurasimisha shughuli zao nchini ili ziweze kutambulika kisheria na mipango ya serikali ikiwa na Tamisemi na wajibu wa kujua ni kwa namna gani wanapaswa kulipa kodi.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kushoto), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa SACCOS ya Jumuiya ya Watanzania waliosoma China (CAAT) katika mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa SACCOS (CAAT), Dk. Fatma-Roselyn Waziri, wa pili kulia ni Mwenyeki wa Jumuiya hiyo, Dk. Liggyle Vumilia na wa pili kushoto ni Balozi mstaafu wa Tanzania China, Luteni Jenerali mstaafu Abdulrahman Shimbo. **MPIGAPICHA WETU**

# Makandarasi waagizwa kukamilisha miradi maji

**Na Mohamed Saif, MTWARA**

MAKANDARASI wanaotekeleza miradi ya maji kwenye wilaya za Newala, Tandahimba na Masasi, mkoani Mtwara wametakiwa kuongeza kasi ya utekelezaji wake ili ikamilike mapema.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, alitoa agizo hilo mkoani hapa kwa nyakati tofauti alipofanya ziara kwenye miradi ya maji inayotekelezwa kwenye wilaya hizo.

Naibu Katibu Mkuu Sanga alitembelea mradi wa Mkwiti uliyopo Wilaya ya Tandahimba, chanzo cha maji cha Mitema, mradi wa Makonde na mradi wa Kilidu yote ya Wilaya ya Newala na mradi wa Chipingo wilayani Masasi.

Baada ya kuzungukia miradi, Mhandisi Sanga alisema hajaridhika na kasi ya utekelezaji wake, licha ya kwamba vifaa vinavyohitajika kukamilisha miradi hiyo ikiwamo mabomba na mitambo ya kusukuma maji vikiwa vimekamilika.

Alisema haoni kwanini miradi inatekelezwa kwa kusuasua licha ya kuwapo vifaa muhimu eneo la mradi. "Nimezungukia maeneo ya miradi, nimeona vifaa muhimu vinavyohitajika kukamilisha miradi vipo, hakuna sababu ya kuendelea kupoteza muda," alisisitiza Mhandisi Sanga.

Alisema kinachotakiwa ni wananchi kupata maji mapema iwezekanavyo, na kwamba suala la kupoteza muda halitokubalika hasa ikizingatiwa maeneo inapotekelezwa miradi yanasumbuliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji.

"Nimeona mitaro imechimbwa na imekamilika na mabomba yapo hakikisheni kuanzia sasa mabomba yanalazwa ili kuepusha gharama ya kufanya kazi mara mbili ya kuchimba mitaro ya maji," aliagiza Sanga.

## Ahimiza watoto warithi elimu badala ya mali

**Na Friday Simbaya, MUFINDI**

MKURUNGEZI wa Shule za Sekondari za Real Hope, Dickson Mwipopo, amewataka wazazi na walezi wilayani Mufindi mkoani Iringa, kuwapeleka watoto shule wapate maarifa na ujuzi badala ya kujinasibu kuwa watawarithisha mashamba ya miti.

Alisema kuwa kuna baadhi ya wazazi na walezi wilayani humo wamekuwa na kawaida ya kuwarithisha watoto miti badala ya elimu.

Akizungumza jana wakati wa mahafali ya Sekondari ya Real Hope iliyopo mjini Mafinga, alisema kuwa wakati wengine wanawekeza katika sekta nyingine aliamua kuwekeza katika elimu na kuongeza kuwa pasipo na elimu hakuna maendeleo mengine.

Alisisitiza kuwa ili watoto waweze kusimamia mashamba ya miti vizuri waliyorithishwa na wazazi wao, hawanabudi kwanza kwenda shule wakapate maarifa na mwanga na hatimaye kuendesha mashamba yao kwa ufanisi.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Jamhuri William, aliwaalika wawekezaji kutoka ndani na nje kuwekeza katika wilaya hiyo kutokana na mazingira wezeshi katika masuala mbalimbali.

Alibainisha kuwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2018/2019, Wilaya ya Mufindi ilikuwa na jumla ya viwanda vikubwa, vya kati na vidogo 161 katika mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu, ambavyo kwa pamoja vimeajiri watu zaidi ya 10,000 na kukaribisha wawekezaji kuwekeza katika sekta ya elimu.

William alimpongeza Mkurugenzi wa Shule za Real Hope, kwa uwekezaji katika sekta ya elimu pamoja na kuzingatia taratibu, kanuni na sheria za nchi na kulipa kodi serikalini.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, Abel Nyamahanga, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo, aliwataka wanafunzi kutumia maarifa waliopata kikamilifu ili kujiletea maendeleo. Dk. Nyamahanga alisema kuwa lazima kuwapo na tofauti kati ya mtu asiye na elimu na aliyesoma kwani ni chanzo cha maarifa katika kiuchumi, siasa, sanyasi na teknolojia.

Akijibu risala ya wahitimu hao 41, kuhusu changamoto ya maji na bwalo la chakula, aliahidi kuchangia mfuko 100 ya saruji ujenzi utakapoanza.

**Alibainisha kuwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2018/2019, Wilaya ya Mufindi ilikuwa na jumla ya viwanda vikubwa, vya kati na vidogo 161 katika mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu, ambavyo kwa pamoja vimeajiri watu zaidi ya 10,000 na kukaribisha wawekezaji kuwekeza katika sekta ya elimu.**

# NEMC: Ni mwiko kutumia mifuko laini ya nailoni

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewatahadharisha na kuwaonya wachuuzi reja reja wa maji na bidhaa nyingine kuacha kutumia mifuko ya nailoni kufungia bidhaa hizo.

Aidha, baraza limewaonya kuwa kutumia mifuko laini ya plastiki ni kuvunja sheria kwani vifungashio hivyo vimepigwa marufuku.

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema mifuko hiyo japo imepigwa marufuku kasi ya kuitumia inaongezeka.

Aliwaonya wachuuzi wanaoitumia kuuza maji na kufungia bidhaa nyingine kuacha kwa kuwa maji yanayouzwa pia usalama wake kwa matumizi ya binadamu haujathibitishwa. Jijini Dar es Salaam, mifuko hiyo laini inatumika kuchuuza maji yanayoitwa 'kandoro' na bidhaa nyingine kama vile karanga, bisi na ubuyu. Kiongozi huyo alisema kurudi kwa maji hayo mitaani kunatishia usalama wa afya za watu na mazingira.

"Licha ya kwamba hiyo mifuko hairuhusiwi, hatujui maji hayo yanatoka wapi. Hali hii inahatarisha afya ya mlaji. Kama kweli ni mjasiriamali na unataka kuzalisha na kuuza maji basi nenda Shirika la Viwango (TBS) na hivyo vifungashio na maji yako, wakapime waangalie maji unazalishia eneo gani. Kwa sasa maji ya nailoni hatuyaruhusu kabisa," Dk. Gwamaka alisema.

Aliwaambia waandishi ambao wanaofuatilia utekelezaji wa marufuku ya serikali ya matumizi ya mifuko ya plastiki.

Alisema timu ya NEMC ipo mtaani kwa ajili ya ukaguzi wa mazingira-hivyo atakayekutwa akitumia mifuko hiyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwamo kifungo au faini kutokana na vifungu vya sheria za kutunza mazingira.

"Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alikwishaeleza kuwa hayo maji hayaruhusiwi. Niwaombe Watanzania kutoa ushirikiano katika kutunza mazingira yetu kwa kutoa taarifa pale ambapo kuna uvunjifu wa sheria ya mazingira."

Aliwataka wananchi kupiga simu namba 0800110116 au kutuma ujumbe kwenda namba 0683540344 na kueleza kuwa simu hiyo haina gharama inatumika bure.

Gwamaka aliwaonya wanaozalisha na kusambaza mifuko mbadala ambayo haikidhi vigezo vilivyowekwa na TBS kwamba watachukuliwa hatua.

Alivitaja baadhi ya vigezo kwamba ni pamoja na kuwa na uzito usiokidhi, anuani ya mzalishaji au nembo ya biashara na kuthibitishwa na TBS.

Aidha, Mkurugenzi wa Sheria wa NEMC, Bernard Kongoza, alisema baraza linafanya kazi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha sheria za mazingira zinafuatwa na kuwaonya wanaokiuka maagizo hatua kali za kisheria zitachukuliwa.



Rundo la takataka likiwa limetelekezwa bila kuzolewa katika Soko la Nguzo Nane, mjini Shinyanga jana, hivyo kuhatarisha afya za wateja na wafanyabiashara wa soko hilo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wanavijiji wajitolea kujenga shule

**Na Sabato Kasika**

SHULE ya Sekondari Mabui, iliyopo Musoma Vijijini mkoani Mara, inatarajia kupokea takribani wanafunzi wapya 157 wa kidato cha kwanza watakaoanza masomo mwaka ujao.

Wakati ikisubiri kupokea idadi hiyo ya wanafunzi, shule hiyo ya kata inakabiliwa na uhaba wa vyumba vitatu vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi hao wapya.

Mkuu wa sekondari hiyo, Generose Severine, aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) kilichokuwa kikijadili jinsi ya kujenga vyumba hivyo na Nipashe kupata nakala ya taarifa yake.

"Shule yetu ina wanafunzi 304 na madarasa, lakini pia inatarajia kupokea takriban wanafunzi wapya 157 wa kidato cha kwanza, hivyo patakuwepo na upungufu wa madarasa matatu," alisema Generose. Baada ya taarifa hiyo, wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Musanja walikubaliana kuanza ujenzi wa madarasa matatu kuanzia kesho Jumatano.

Mwenyekiti wa WDC, Elias Ndaro, alisema, vijiji vyote vitatu vya kata hiyo, ambavyo ni Musanja, Mabui na Nyabaengere, vitashiriki kikamilifu kuhakikisha ujenzi unaanza na kukamilika haraka.

Ndaro alisema, kila mkazi wa Vijiji Vitatu vya kata hiyo mwenye umri wa miaka 18 hadi 59 atachangia Sh. 5,000 huku wengine wasio na uwezo wa kifedha watashiriki kwa kufanya kazi.

"Ujenzi wa vyumba vitatu ukianza, Mbunge Profesa Sospeter Muhongo, atakuja hapa shuleni kwa ajili ya kuendesha harambee na atachangia ujenzi," alisema Ndaro.

Aliongeza kuwa mbunge huyo alishachangia mabati 54 ya kuezeka darasa moja na kutoa vitabu vya masomo ya Sayansi na Kiingereza.

Mwenyekiti huyo alisema, kwa utaratibu waliojiwekea ni kila kijiji kujenga chumba kimoja cha darasa na kwamba makubaliano waliofikia kwenye kikao cha WDC yatatekelezwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma, Charles Magoma, alisema Musoma Vijijini ina sekondari za kata 18, binafsi mbili na kwamba wananchi kwa kushirikiana na serikali yao wanajenga nyingine mpya tisa.

"Wananchi wamedhamiria kwamba ifikapo Januari 2020, sekondari mpya zitakazochukua wanafunzi wa kidato cha kwanza ziwe zimekamilika, ambazo ni Dan Mapigano ya Kata ya Bugoji na Busambara ya Kata ya Busambara," alisema Magoma.

Alisema, hizo mbili zitachukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakani, wakati nyingine ikiwamo sekondari ya Nyasaungu inayojengwa na kijiji kimoja cha Nyasaungu ndani ya Kata ya Ifulifu zikiendelea kujengwa.

## Takukuru yaonya rushwa uchaguzi serikali za mitaa

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Longido, Ally Mikidadi, amewataka wananchi kujiepusha na vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Amewataka wananchi kutoa taarifa za watu watakaotangaza nia endapo watajihusisha na utoaji wa rushwa ili wapate nafasi za uongozi.

Mikidadi alisema hayo juzi wakati akizungumzia mchakato wa uchaguzi huo, huku akisisitiza ni kosa la jinai kutoa, kupokea au kushawishi rushwa chini ya kifungu cha Sheria namba 15 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007.

Alisema kutenda kosa hilo pia ni kinyume cha Sheria ya Serikali za Mitaa Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Miji Sura ya 288, kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika Novemba, mwaka huu.

"Kumchagua kiongozi anayetoa rushwa ni kukwamisha maendeleo ya nchi. Chagueni viongozi watakaoleta maendeleo. Watoa rushwa wananunua madaraka, mkiwapa nafasi watakuja kuwahujuhumu warejeshe fedha zao walizotumia kipindi cha kampeni," alisema Mikidadi.

Katika kudhibiti vitendo vya rushwa, alisema taasisi hiyo imeshatoa elimu katika maeneo mbalimbali wilayani humo, vikiwamo vijiji vya Engikaret, Eworendeke na lesing'ita.

"Wananchi wanaelimu na tumewaelekeza namna ya kutupatia taarifa, hivyo tukribani kuna mtangaza nia anayefanya kampeni kinyume cha taratibu kwa kushawishi vitendo vya rushwa tutamchukulia hatua za kisheria," aliongeza.

Alisema kwa watangaza nia kutoa vyakula mfano sukari, mchele na vinywaji kama pombe, kutoa nguo na kanga za kampeni ni rushwa na imetajwa katika kifungu cha sheria namba 15 na 16.

Mikidadi alisema serikali inatoa fedha nyingi za miradi ya maendeleo, hivyo aliwasisitiza kuchagua viongozi wenye sifa na weledi watakaosaidia kuleta maendeleo, lakini kuchagua viongozi wanaotumia nguvu ya pesa watakuja kuhujumu miradi hiyo.

**"Wananchi wanaelimu na tumewaelekeza namna ya kutupatia taarifa, hivyo tukribani kuna mtangaza nia anayefanya kampeni kinyume cha taratibu kwa kushawishi vitendo vya rushwa tutamchukulia hatua za kisheria," aliongeza.**

# Ukosefu mabweni wasababisha utoro, ujauzito

**Na Allan Isack, ARUSHA**

SHULE ya Sekondari ya Namanga wilayani Longido, inakabiliwa na upungufu wa mabweni ambao umesababisha baadhi ya wanafunzi kukatisha masomo na wengine kujihusisha na biashara ya mirungi.

Akizungumza katika mahafali ya 10 ya shule hiyo, Mkuu wa Shule, Mtesigwa Missana, alisema upungufu wa mabweni ya wasichana katika shule hiyo, umesababisha baadhi ya wasichana kupata ujauzito kutokana na vishawishi wanavyovipata njiani wakati wa kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Missana alisema eneo la mpaka wa Namanga lina mwingiliano wa watu kutoka nchi ya jirani ya Kenya, hivyo ni rahisi kwa wasichana kudanganywa na vitu vidogo wakati wa kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Kwa upande wa wanafunzi wa kiume, alisema changamoto inayowakabili ni utoro kwa kuwa wamekuwa wakijihusisha na biashara haramu ya mirungi katika eneo hilo.

"Shule inapofunguliwa tukiwapima wasichana baadhi wanakuwa na ujauzito kutokana na shule kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi ambao hawatoshelezi kwenye mabweni. Kwa wavulana tatizo lao ni utoro kwani wanaacha kuja shuleni kwa ajili ya kwenda kufanya biashara ya mirungi eneo la mpakani," alisema Missana.

"Mabweni yaliyopo yana uwezo wa kubeba wanafunzi 216 kati ya wanafunzi 732, waliopo shuleni hapa," aliongeza.

Mkuu huyo pia alisema shule inakabiliwa na ukosefu wa bwalo la chakula, jiko, uzio, mktaba, uhaba wa maji, nyumba za walimu na umaliziaji wa chumba kimoja cha maabara ya fizikia.

Alisema kukosekana kwa uzio kwenye shule hiyo, usalama wa watumishi na wanafunzi ni mdogo kwa kuwa wakati wa kiangazi tembo hupita eneo la shule kwa ajili ya kutafuta maji.

Mgeni rasmi katika mahafali hayo, Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdalla Ulega, aliitaka jamii ya kifugaji kusomesha watoto wa kike na waepuke utamaduni wa kimila kuwaozesha wakiwa wadogo.

Pia aliwashauri wahitimu wa kidato cha nne, kutumia elimu waliyoipata shuleni hapo kwenda kuleta mabadiliko kwenye jamii.

"Ninawapongeza wazazi kwa kujitoa kuwalea vyema na kuwapatia elimu na mahitaji bora, ninawaasa muwaenzi sana wazazi wenu na kusoma kwa bidii. Huko mwendako mkatumie elimu hii kuleta mabadiliko," alisema Ulenga.

Aidha, katika hatua ya kukababiliana na changamoto hizo, hususani ya bweni, Ulega na wataalamu wa Wizara ya Uvuvi na Mifugo waliongoza uchangiaji wa ujenzi wa bweni na kupatikana zaidi ya Sh. milioni tano.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kulia), akionja maziwa yanayotengenezwa na Kiwanda cha Kilimanjaro Fresh, alipokitembelea jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# RPC Arusha ahimiza watu kujiandikisha

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha, limewaomba wananchi mkoani hapa kujitokeza kwa wingi katika uandikishaji wa daftari la wapigakura kwa ajili ya kuwawezesha kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shanna, aliyasema hayo jana ofisini kwake baada ya kukamilisha ziara ya kutembelea na kukagua hali ya usalama kwenye vituo vya kujiandikisha wapigakura jijini Arusha.

Kazi ya kujiandikisha ilianza Oktoba 8 na inatarajia kukamilika Oktoba 17 saa 12 jioni.

Shanna alisema Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha usalama na ulinzi, ili kuwezesha wananchi kujiandikisha katika hali ya utulivu na amani pamoja na wakati wote wa kampeni mpaka uchaguzi utakapofanyika na matokeo kutangazwa.

"Nimekuta kazi ya uandikishaji imedorora, hivyo natoa wito kwa wananchi watumie muda wa nyongeza wa siku tatu uliotolewa na serikali ili kushiriki kujiandikisha kwenye daftari la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na wachague viongozi wao," alisema.

Kamanda Shana, alisema serikali imeongeza siku tatu ambapo zoezi hilo lilikuwa lifikie mwisho Oktoba 14, sasa limesogezwa mbele hadi Oktoba 17, saa 12:000 jioni kutokana na kubainika kuwa wananchi wengi walikuwa hawajajitokeza kujiandikisha.

"Ni vyema wananchi wakatambua umuhimu wa kujiandikisha na haki yao. Naomba watu wajiandikishe ili wapate fursa ya kuwachagua viongozi bora na wanaowataka," alisisitiza.

Kamanda Shanna alisema hadi sasa hakuna tukio lolote la uhalifu ambalo limetokea kwa ajili ya kuvuruga uandikishaji huo na alionya kuwa Jeshi la Polisi halitasita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayejihusisha na uvunjifu wa amani.

Katika kuhakikisha usalama unaimarishwa, alisema Jeshi la Polisi litatumia vitabu vitatu ambavyo ni kuzingatia kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa za mwaka 2019.

Pia alisema wanatumia mwongozo wa uchaguzi wa serikali za mitaa na watazingatia sheria na taratibu za polisi zilizoko kwenye mwongozo wa jeshi hilo wakati wote wa kampeni, kupiga kura hadi kutangazwa kwa matokeo.

## Ardhi yaanza kushughulikia malalamiko

**Na Mwandishi Wetu, ROMBO**

HATIMAYE Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, imeanza mchakato wa kughughulikia malalamiko ya Chama cha Ushirika wa Mazao cha Tarakea Amcos ambacho kiliomba kupimiwa eneo lake la ardhi kwa miaka 13 bila mafanikio.

Katibu wa Tarakea Amcos, Bertha Shirima, alithibitisha serikali kuanza kuchukua hatua za kuhakikisha eneo hilo linapimwa ili kuruhusu shughuli nyingine za maendeleo kufanyika ikiwamo uwekezaji wa jengo la biashara.

"Tumefika mahali pazuri, tunaishukuru sana serikali na hasa Mkuu wa Wilaya ya Rombo kwa kusimamia jambo hili. Aliahidi kwamba litapimwa na sasa tunaanza kuona mwanga katika maelekezo yake," alisema.

"Unajua sisi tunataka kuanzisha duka kubwa la pembejeo na hardware (vifaa vya ujenzi) ili kuwasaidia wakulima, kama tutapata mkopo kutoka benki, lakini tunakwama kuendelea na mchakato kwa sababu ya kukosa hiyo hati."

Kutokana na ufuatiliaji wa jambo hilo kuanza kuzaa matunda, Shirima alimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo kwa kuwahi kwenda katika chama hicho na kutoa amri kwa Idara ya Ardhi kutoa hati hiyo ndani ya siku 14.

Hivi karibuni, chama hicho kupitia bodi yake kilieleza kukwamishwa na idara hiyo pamoja na Serikali ya Kijiji cha Kibaoni, kupata hati miliki ya ardhi ya eneo lao.

Alinukuliwa Kaimu Mwenyekiti wa Tarakea Amcos, Adam Sudi, akisema walianza mchakato wa kutafuta hati hiyo mwaka 2006 na 2007, walilipa ada ya upimaji katika Idara ya Ardhi kiasi cha Sh. 700, 000 na kuwekewa alama za mipaka (bicons) na kisha kupewa fomu ili kuipeleka ofisi ya kijiji kupata baraka, hawajawahi kurejeshewa fomu hiyo, licha ya kuulizia kila mara," alieleza.

# Atangaza nia kugombea Moshi Mjini

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MAKAMU Mwenyekiti Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Mkoa wa Kilimanjaro (Shivyawata), Hellen Mmbando, amesema ana nia ya kugombea ubunge wa Jimbo la Moshi Mjini katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Alisema uamuzi wake, unalenga kuwahamasisha wanawake wengine kujitokeza kushiriki kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mbalimbali ukiwamo wa serikali za mitaa na vijiji unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Alitangaza nia hiyo, wakati wa mafunzo ya uongozi, demokrasia na utawala bora kwa wanawake, na uwakilishi wa watu wenye ulemavu katika Mkoa wa Kilimanjaro. Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika la kiraia la Kwieco, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

"Msiishie kujiandikisha, ombeni na uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, lakini hata ule uchaguzi mkuu ujao wa mwakani. Mimi nawatangazia kabisa kwamba nagombea ubunge Moshi Mjini 2020.

"Nawashukuru waliofikiria kuja na mradi huu wa majaribio wa mwaka mmoja wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia mkoani Kilimanjaro, tunajadili uongozi na mtazamo wa jamii kuhusu wanawake katika uongozi, nini kifanyike kuondoa mtazamo hasi? Wanatupa mbinu za wanawake viongozi katika ushawishi na uwasilishaji wa matatizo katika kuleta usawa wa kijinsia."

Mbando ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watu Wenye Ulemavu Mkoa wa Kilimanjaro, alisema takwimu zinaonyesha wanawake wanaojitokeza kuwania nafasi za uongozi ni wachache.

Kwa upande wake, Rabia Mshana ambaye ni Mtunza Hazina wa Chama Walemavu Mkoa wa Kilimanjaro (Chawata), akichangia hoja hiyo alisema wanawake wanaotarajia kujiandikisha ni kubwa kuliko wanaume na uzoefu umeonyesha hata kwenye kupiga kura wanawake huwa wanajitokeza kwa wingi kuliko wanaume, lakini kwenye kugombea uongozi hali imekuwa ni tofauti.

"Wanawake ambao huomba nafasi za uongozi kuanzia kwenye vyama vyao hadi kwenye uongozi wa jamii imekuwa ndogo kulinganisha na wanaume," alieleza Rabia.

Wakati wa uzinduzi huo, Mratibu wa mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia mkoani humo, Veronica Ollomi, alisema mradi huo unalenga kujenga uelewa na uwezo kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia, haki za binadamu, na uwezeshaji wa wanawake na wasichana kwenye jamii.

"Mradi huu unakwenda kuimarisha na kusimamia majukwaa na mitandao ya wanawake, ambayo tayari imeshaunda ndani ya mkoa ili kuendelea kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa ajili ya kuhamasisha haki za binadamu, usawa wa kijinsia, uongozi na kujengea uwezo wanawake na wasichana," alisisitiza Ollomi.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akiendesha harambee ya umaliziaji wa msikitini wa Matui, wilayani Kiteto juzi, ambapo jumla ya Sh. milioni 2.2 zilikusanywa. **PICHA: GIFT THADEY**

# Latra yapewa angalizo migogoro ya madereva

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameinyooshea kidole Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra), kuhusu migogoro inayoendelea kuchomoza kati ya madereva wa pikipiki za matairi matatu maarufu 'Bajaj' na wa mabasi madogo ya abiria.

Mghwira ameeleza masikitiko yake hayo katika kikao cha Bodi ya Barabara, wakati akichangia hoja kuhusu migogoro hiyo namna inavyoweza kuumiza wasafiri kama haitakomeshwa kwa kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

"Nyie Latra ni lazima mjiangalie, haiwezekani mambo haya ya migogoro yanajitokeza mara kwa mara. Hamna budi kuwa makini na kuhakikisha migogoro kati ya waendesha Bajaj na Hiace inamalizika mara moja, naona kila wakati wakigombea vituo vya kupakia abiria na usajili wa barabara," alisema.

Alitoa wito kwa Wakala wa Barabara (Tanroads) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), katika Mkoa wa Kilimanjaro kuhakikisha barabara za vijijini zinajengwa kwa kiwango cha lami, na siyo kujenga zinazoenda nyumbani kwa viongozi ambao mchango wao katika kukuza uchumi ni mdogo.

Alisema fedha nyingi za mikopo ya barabara zinashindwa kurejeshwa kutokana na fedha hizo kutumika kujenga barabara za kwenda kwa viongozi, badala ya kujenga barabara ziendazo kwa wazalishaji wakubwa wa uchumi.

Katika maelekezo yake, Dk. Mghwira alisema barabara za vijijini ndio zenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara.

Naye, Katibu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi nchini (Taboa), Enea Mrutu, aliibua hoja ya kutaka serikali isigawe vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga kwa wabigadebe katika vituo vya mabasi, kwa kuwa sasa wamegeuka kero kwa abiria.

Alishauri vitambulisho hivyo vitolewe kwa utaratibu uliotolewa na Rais John Magufuli na sio kwa wapigadebe wa stendi za mabasi, kwa vile wengi wao siyo wastaarabu na waaminifu kwa mali na pesa za abiria, wanapoingia stendi.

Meneja leseni wa Latra Mkoa wa Kilimanjaro, Leo Ngowi, alisema wanakusudia kuanzisha utaratibu wa abiria kukata tiketi kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia simu ya kiganjani.

"Tunataka sasa kuwaondoa wapigadebe vituo vyote vya mabasi, kwa kuanzisha ukataji wa tiketi za kielektroniki na hii itawasaidia wamiliki wa mabasi kuongeza mapato yao. Hawa wamiliki wanapoteza mapato makubwa kutokana na wapiga debe," alieleza Ngowi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 15, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 18




## Uganda yaja na mabadiliko ya sheria

Ukurasa 19



Kupokezana mwanga/ vijiti (Passing the torch)



Ukurasa 14

## Fahamu namna ya kuzuia maafa



# Wazee Shinyanga wapaza vilio

Ukurasa 16

ELIMU KUTOKA POLISI

# Fahamu namna ya kuzuia maafa



Moja kati ya maafa yaliyosababishwa na mvua. **PICHA: MTANDAO**

MAAFA ni matokeo ya majanga au janga ambalo husababisha vifo, upotevu wa mali au mazingira ambapo jamii iliyoathirika haiwezi kukabili kwa uwezo na rasilimali zake bila ya msaada kutoka nje ya jamii hiyo.

Janga au Majanga ni balaa au baa linaloweza kusababisha maafa.

Ili maafa yatokee ni lazima liwepo janga na vitu vinavyoweza kuathiriwa na janga hilo mfano watu, Miundombinu au mazingira.

### SABABU ZA KUATHIRIWA NA JANGA AU MAJANGA

Kuwa karibu na eneo la janga, Mabadiliko ya hali ya hewa na Uharibifu wa mazingira ni baadhi ya sababu.

Aidha, umaskini, kutokujua au kufahamu, matatizo ya kijamii na kisiasa.

### AINA ZA MAAFA

Kwanza ni maafa yanayosababishwa na nguvu za kiasili bila au pakiwa na visababishi vidogo kutoka kwa binadamu mara nyingi hutokana na jiolojia, haidrolojia au mabadiliko ya hali ya hewa.

Mfano ya aina hii ya maafa ni ukame, tetemeko la ardhi, kimbunga, mafuriko, milipuko, radi na magonjwa ya milipuko.

Kuna maafa yanayosababishwa na vitendo vya kibinadamu kwa bahati mbaya, makusudi au uzembe.

Mifano ya aina hii ya maafa ni pamoja na ajali ya vyombo vya usafiri au viwandani, moto, wakimbizi, migongano ya kijamii/vita.

Vilevile kuna aina ya makundi ya maafa ambayo hutokea kwa kasi yaani ghafla na yale yanayotokea polepole.

### MAAFA YANAYOTOKEA GHAFLA

Ni moja ya makundi ya aina ya Maafa yanayotokea kwa ghafla bila ya kutegemewa mfano tetemeko la ardhi, ajali, moto pamoja na milipuko ya kemikali.

Katika aina hii ya maafa huwa mara nyingi hakuna muda wa kutosha wa kutoa onyo kwa wananchi.

### MAAFA YANAYOTOKEA POLEPOLE

Hii ni aina nyingine ya makundi ya maafa ambayo huwa na tabia ya kujengeka polepole ndani ya jamii.

Baadhi ya mifano ya aina hii ya maafa ni pamoja na ukame, migongano ya kijamii na vita.

Katika aina hii ya maafa, huwa kuna muda wa kutosha wa kutoa onyo au tahadhari na jamii inaweza kujiandaa kukabiliana nayo.

### NAMNA YA KUZUIA MAAFA

Ni hatua zinazochukuliwa (Kabla ya maafa) kwa kusudi la kuzuia maafa yasitokee kabisa au kupunguza madhara yake.

Maafa yanaweza kuzuilika au kupunguza madhara yake ndani ya jamii kwa kuzingatia tahadhari zinazotolewa mara kwa mara na mamlaka husika, Kuhama kutoka kwenye maeneo yasiyofaa kwa maisha ya kibinadamu.

Kwa mujibu wa Mtalaam wa kukabiliana na maafa wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Nasser Mwakamboja, jamii haiwezi kuzuia maafa yote lakini baadhi ya maafa yanaweza kuzuiliwa.

Aidha, kwa yale ambayo hayawezi kuzuiwa, madhara yake yanaweza kupunguzwa kwa kutekeleza baadhi ya mipango mahsusi inayotakiwa kufanyika kabla, wakati na baada ya maafa kutokea.

"Uelewa mdogo wa namna ya kukabiliana na maafa ni miongoni mwa changamoto za kuzuia na kupunguza madhara ya maafa pindi yanapojitokeza." Anasema ACP Mwakamboja.

Kuzuia ni hatua muhimu na imedhihirisha kuwa ni gharama nafuu kuliko ile ya kukabili maafa.

***Imetolewa na;***
***Kitengo cha Uhusiano***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.***
***S.L.P 9141***
***Dar es Salaam***
***Baruapepe habariphq@yahoo.com, habari.phq@tpf.go.tz***



TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

## Enyi waandishi, kazi ni kanzi

'KANZI' ni hazina kubwa au vitu vya thamani. Kanzi ni kama hazina. Twafunzwa umuhimu wa kazi ambayo ni hazina yetu ya siku za shida au zijazo.

Neno 'kazi' laweza kuwa na maana mbili au tatu lakini ninalolizungumzia kwenye makala yangu ni shughuli yoyote anayofanya mtu kwa ajili ya kupata riziki ya kuendeshea maisha yake. Mwandishi ni mtunzi wa makala, kitabu, kazi ya sanaa au habari mbali mbali za matukio. Yasemwa mwandishi wa habari ni masikio, pua na macho ya wasomaji.

Uandishi au uandikaji, ni shughuli inayohusu masuala ya kuandika kama vile habari au kitabu. Kwa hiyo mwandishi husika, hunusa na huona matukio mbalimbali kisha kuwajuza wananchi kwa njia ya magazeti, redio na runinga.

Kwa hakika uandishi unahitaji utulivu na hekima ili kuwafahamisha wasomaji wa magazeti, watazamaji wa runinga na wasikilizaji wa redio kuhusu matukio yatokeayo nchini na kwingine ulimwenguni.

Mwandishi mzuri huandika kwa maneno yanayotambulika kwa wote badala ya kutumia maneno ya kihuni yatumikayo mitaani! Mwandishi aweza kuwa na habari nzuri lakini akaiharibu au kuipotosha kwa kutumia maneno ya mitaani yaani simo* ambayo si lugha sahihi.

*Simo ni msemo wa muda unaozuka katika jamii na kisha kupotea. Lugha ya aina hiyo kwa Kiingereza yaitwa 'slang' ambayo kwa Kiswahili ni simo au misimu, yaani lugha ya mitaani.

Soma hii: "Taifa Stars, Sudan 'vibe' kama lote" ni kichwa cha habari inayohusu mchezo wa kandanda kati ya Taifa Stars na Sudan jijini Dar es Salaam. Ni wangapi wanaojua maana ya "'vibe' kama lote?"

Aya ya pili ya habari husika iliandikwa: " Kampeni pacha ya Tunakanyaga Mpaka CHAN, iitwayo Chaji Simu Yako, tukutane Taifa Kuwamulika Wasudan, nayo imepamba moto ikilenga kuchagiza mashabiki kumiminika kwa wingi kuisapoti Stars ikiwakanyaga Sudan kuelekea kwenye fainali hizo Cameroon."

Yaelekea watazamaji hawakuchaji (nguvu zinazozalishwa na umeme) simu zao na kusababisha kukosa mwanga wa 'kuwamulika' wachezaji wa Sudan hata kufanya Taifa Stars wafungwe 1-0 kwenye uwanja wa nyumbani, tena mbele ya umati wa Watanzania! (Haya ni maoni yangu.)

"Kampeni pacha ya Tunakanyaga Mpaka CHAN." 'Pacha' ni neno lenye maana tatu: 1) watoto wawili au zaidi waliozaliwa kwa mimba moja; 2) kitendo cha kuzifunga pamoja nazi ambazo hazijafuliwa; 3) ni –enye kuambatana na kingine (Wazanzibari husema 'chengine.') Je, neno 'pacha' kwa muktadha ninaoujadili lilistahiki kutumiwa?

"… imepamba moto ikilenga kuchagiza mashabiki kumiminika kwa wingi kuisapoti Stars …" Neno 'chagiza' ni kitenzi elekezi na maana yake ni ghasi mtu kwa kumdodosa sana; udhi, sumbua. 'Chagizi' ni –enye kusumbua na 'chagizo' ni shinikizo; udhia, usumbufu, kero. Je, mwandishi ametumia neno 'chagiza' kwa usahihi?

"Bodaboda ya Mchongo wa (jina la gazeti) yatua Morogoro" ni kichwa cha habari inayoeleza washindi wa mchezo wa gazeti ninaloliheshimu.

Maana ya 'mchongo' ni mtindo wa utengenezaji wa samani ya mbao unaoitafautisha na nyengine, kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha la Zanzibar.

*Visawe ni maneno yenye maana zinazokaribiana. Kwa mfano, 'mtoto' na 'mwana' humaanisha kitu kimoja.

Visawe hutumika ili kuwasilisha dhana ileile iliyokusudiwa bila kubadilisha maana. Kwa hiyo visawe hupamba lugha ama katika mazungumzo au katika uandishi wa aina mbalimbali.

Kwa mfano 'shabihi' ni fanana, landana. 'Simanzi' maana yake ni majonzi, jitimai, ukiwa, huzuni. 'Taadhima' ni heshima, adabu, tasfida. 'Wajihi' ni sura, uso. 'Kibahaluli' maana yake ni kibatari, koroboi.

Maana ya 'kuwadi' ni kijumbe, gambera, mtalaleshi, kibirikizi. 'Laghai' ni danganya, nyenga, kenga, ongopa. 'Weweseka' ni hohosa, babaika, kiakia, hangaika, riyariya. 'Mvulana' maana yake ni ghulamu, janadume, barobaro. 'Mtu' ni adinasi, mja, mwanadamu, mahuluki.

"Messi vyenga kama ana gundi miguuni vile." Mwandishi katumia neno 'vyenga' akiwa na maana ya chenga nyingi. Hata hivyo 'chenga' haina wingi hata iitwe 'vyenga!'

Baadhi ya maneno yasiyokuwa na wingi ni baba, mama, dada n.k. Ni kupotosha Kiswahili kusema 'wababa, wamama, wakaka, wadada.'

Upotoshwaji huu hufanywa sana na Wakristo wenzangu! Kama ilivyo mitaani kaka huitwa 'mkaka' neno lenye maana ya mti wa porini wenye kiini cheusi na kigumu na majani madogomadogo; mkurungu.

"Wakati mashabiki wengi wa Toto Africans wakijiuliza heshima ya klabu yao itarejea lini, beki wa timu hiyo Robert Magadula amesema tulizeni mzuka mambo mazuri yanakuja watulize mzuka."

Mwandishi katumia neno 'mzuka' mara mbili. Alikuwa na maana gani? 'Mzuka' ni pepo; mahali patukufu akhera ambapo mtu mwema duniani ataishi baada ya kufufuliwa.

Pia ni jini, yaani kiumbe dhahania (-enye kutokuwa na umbo linaloshika au uwezo mdogo wa kutokea) asiyeonekana aliyeumbwa kwa moto; mtu habithi/khabithi yaani asiyejali utu wa mwingine. Chembe ya urithisho ya mzazi kwa mtoto wake.

**Methali: Ada ya mja, hunena: mwungwana ni kitendo.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

UCHAMBUZI
NA REUBENI LUMBAGALA

# Ajira za watoto zinakiuka haki ya elimu, zipigwe vita



Watoto kama hawa wanastahili kupata haki yao ya elimu na si kuwaingiza kwenye ajira za utotoni. **PICHA: MTANDAO**

AJIRA ni shughuli yeyote halali anayoifanya mtu ili kujiingizia kipato na hatimaye kuweza kumudu kuendesha maisha yake.

Mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, yaani kuanzia umri 0 hadi 17. Kwa hiyo, ajira ya mtoto ni hali ya mtu chini ya miaka 18 kufanyishwa kazi za ujira maalum.

Kimsingi, mtu anayepaswa kufanya kazi ni yule mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea kwani mwenye aina hiyo ya umri huchukuliwa kuwa ni mtu mzima, mwenye uelewa na uwezo wa kumudu kufanya kazi na kuwa na uwezo wa kudai malipo yanayowiana na kazi anayoifanya. Mtoto hapaswi kufanyishwa kazi kwa sababu umri wake hauruhusu.

Na ikumbukwe kuwa, kazi ya mtoto ni kwenda shule kusoma na kupata maarifa ya kumwezesha kuja kufanya kazi baadaye atakapofikisha umri sahihi kisheria.

Haki ya kupata elimu ni haki ya msingi ya mtoto. Haki hii haipaswi kuvunjwa kwa sababu nyingine yeyote kutokana na ukweli kwamba elimu kwa mtoto ni maandalizi ya kutengeneza mustakabali wake mwema wa maisha yake ya sasa na ya baadaye.

Hivyo, mtoto anaposhirikishwa katika ajira ni dhahiri haki ya kupata elimu inavunjwa kwa sababu muda ambao mtoto atapaswa kuwa shuleni, atakuwa katika maeneo mengine ya shughuli kama sokoni, vituo vya mabasi, migodini, baharini nk.

> “ Serikali imeamua kutekeleza ahadi yake ya kutoa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne ili kuwapatia nafasi kila mtoto kupata elimu.

Pamoja na changamoto ya umaskini kwa baadhi ya kaya, haki ya mtoto ya kupata elimu inapaswa kubaki palepale.

Baadhi ya kaya huamua kuwatumia watoto wao kufanya shughuli za kiuchumi kama vile kuuza maandazi, peremende, ndizi, keki, ili kuweza kupata kipato.

Ni lazima jamii itambue kuwa ipo faida kubwa ya kupeleka watoto wao shule kulinganisha na kuwatumikisha kwenye shughuli za kiuchumi.

Suala la kusoma linaweza kuonekana kama jambo lisilo na faida kwa baadhi ya jamii kutokana na matunda ya kusoma kuchukua muda hadi kuja kuonekana. Hata hivyo, ukweli utabaki kuwa uwekezaji unaolipa na wenye tija ni ule wa wazazi na walezi kupeleka watoto wao shule ili kuelimika.

Elimu ni uwekezaji pekee ambao hauna kufilisika wala kupata hasara kwani maarifa, ujuzi na stadi zinazoingia katika ubongo wa msomaji hubaki kichwani daima.

Jamii ijifunze kwa familia ambazo ziliamua kupeleka watoto shule (watoto wa kiume na wa kike) na matunda ambayo kwa sasa wanayapata kupitia watoto wao.

Wazazi na walezi wazitumie rasilimali walizonazo katika kuwasomesha watoto wao ili baadaye wanufaike na matunda ya elimu watakayopata watoto wao.

Mzazi anaweza kudhani kumfanya mtoto wake mchungaji wa mifugo kama mbuzi, ng'ombe, kondoo ni faida kwake lakini mifugo hiyo inaweza kufa na familia hiyo kuingia katika lindi la umaskini huku mtoto huyo akiwa mjinga kwa kutopata elimu.

Mzazi anaweza kupeleka mtoto wake kuuza peremende, maandazi sokoni ili kupata kipato lakini kipato hicho kikaendelea kuwafanya wazidi kuwa maskini na mtoto huyo akibaki katika lindi la ujinga na familia nzima kuwa maskini.

Jamii zote yaani wakulima, wafugaji, wavuvi, wawindaji wanapaswa kuelimishwa kuhusiana na umuhimu wa kusomesha watoto wao na kuachana na tamaa ya kupata fedha kwa kuwatumia watoto hao kama njia ya uzalishaji mali, kwani kwa kufanya hivyo ni kosa kisheria na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Serikali imeamua kutekeleza ahadi yake ya kutoa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne ili kuwapatia nafasi kila mtoto kupata elimu.

Kuendeleza kuwatumikisha watoto ni kuikwamisha serikali katika mipango yake ya kupata wasomi wa kutosha katika nchi hii kwa kutoa elimu bila malipo.

Serikali hutumia Sh. bilioni 24 kila mwezi kutekeleza sera ya elimu bila malipo. Fedha hizi ni nyingi na kama si utashi wa serikali wa kutaka kila mtoto kupata elimu, fedha hizo zingeweza kutumika katika matumizi mengine yasiyo ya lazima kama semina, warsha na makongamano mbalimbali.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiwa ziarani mkoani Singida aliwaagiza Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kufanya msako kwenye stendi za mabasi ili kuwabaini watoto wasiokwenda shule.

Waziri Majaliwa alisema “Hatutarajii kuona vijana wadogo wauza biashara kwenye vituo vya mabasi... Mkurugenzi chukua OCD siku moja, nenda kwenye miji yenu midogo, saka watoto wote wanaofanya biashara stendi, watambue wazazi wao, halafu kamata wazazi wao wajieleze ni kwanini wanawaacha watoto wao waende stendi badala ya kwenda shule...tunataka kila mtoto wa Kitanzania aende shule”.

Agizo hili ni kwa viongozi wote nchini katika kuhakikisha kila mtoto anapata elimu na kuachana na ajira za watoto.

Familia na jamii kwa ujumla tushirikiane katika vita hii ya ajira za watoto ili watoto wapate elimu. Sote tuwe na sauti moja kusema “Shule kwanza, ajira baadae”. Tafakari, chukua hatua.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Kwa maoni na ushauri: (+255) 764 666349.***

UVUMBUZI

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Wazee Shinyanga wapaza vilio

## • Ni kuhusu Sera ya Wazee • Wataka itekelezwe kwa vitendo



Wazee wa Wilaya ya Shinyanga wakiwa kwenye siku ya maadhimisho ya wazee duniani yaliyofanyika katika Kata ya Tinde Shinyanga vijijini. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

MZEE ni mtu aliyefikisha umri wa miaka 60 na kuendelea. Asilimia kubwa ya watu wa umri huu, huwa hawana nguvu tena ya kufanya kazi za kuwaingizia kipato, na hivyo kuanza kuwa tegemezi.

Asilimia 96 ya wazee nchini wana maisha magumu, hasa wale wa maeneo ya vijijini.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba wengi wao hawakuwa na ajira rasmi, ukiacha asilimia nne kati yao ambayo ilikuwa na ajira na hivyo kupata mafao.

Aidha, kuna waliopata fursa ya kuwa na miradi ya kuwaingizia kipato na hatimaye pesa za kijikimu kimaisha. Kwa wazee ambao hawakuwa na ajira rasmi, ama miradi ya uwekezaji wanakumbana miongoni mwao pia na janga la kutelekezwa na watoto wao na hivyo kukosa huduma mbalimbali zikiwamo za matibabu.

Matokeo yake ni kupoteza maisha kwa sababu ya kukosa fedha za kugharimia matibabu.

> Na kwa kuwa wengi wao hujikuta pia wametelekezwa na watoto wao, msaada mkubwa wa kuokoa maisha yao umebaki serikalini, ikiwa ni pamoja na kupatiwa matibabu bure.

**SERA**

Sera ya Wazee ya mwaka 2003, inatamka wazi kwamba wazee wote wenye umri wa kuanzia miaka 60 na kuendelea, wanatakiwa kupewa huduma bure za matibabu kwenye hospitali zote za Serikali, zahanati na vituo vya afya.

Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kwenye utekelezwaji wa sera hiyo nchini, kama ilivyo katika Wilaya ya Shinyanga Vijijini.

Wazee hawana vitambulisho vya matibabu bure, hakuna madirisha maalumu ya wazee katika vituo vya afya, ukosefu wa madaktari bingwa wa magonjwa yao pamoja na huduma za afya kuwa mbali na wanapoishi.

**KATIBU**

Katibu wa Baraza la Wazee Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Boniphace Boazi, anasema idadi kubwa ya wazee wilayani humo wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa matibabu, kwa kukosa vitambulisho pamoja na huduma za afya kupatikana mbali na makazi yao.

Anasema kwenye wilaya hiyo kuna jumla ya wazee 12,922, jinsia ya kiume wakiwa 6,173, na ya kike 6,749. Boazi anasema, walio na vitambulisho vya matibabu bure ni 5,568 na waliosalia ambao ni 7,354 hawana vitambulisho hivyo.

"Sasa ugumu wa maisha kwa Wazee hawa unatokana na ukweli kuwa shughuli za kiuchumi walizokuwa wakizifanya kwa kiasi kikubwa, zilikuwa ni kilimo na ufugaji ambazo katika umri wao wa sasa hawawezi kuzifanya tena," anasema na kuongeza:

"Na kwa kuwa wengi wao hujikuta pia wametelekezwa na watoto wao, msaada mkubwa wa kuokoa maisha yao umebaki serikalini, ikiwa ni pamoja na kupatiwa matibabu bure."

Katibu huyu anaomba Sera ya Wazee ya mwaka 2003, itekelezwe kwa vitendo na si maneno tu.

"Nasema hivyo kwa sababu kila mwaka tunapoadhimisha siku ya wazee, tunazitaja changamoto hizo hizo na hakuna mabadiliko japo kidogo...mfano takwimu hizi za wazee wenye vitambulisho vya matibabu na wasionavyo ni hizo hizo, hakuna hata ongezeko," anasema.

Anaitaka Serikali sasa iitekeleze sera hiyo kwa vitendo ili kundi hili la wazee ambao ni hazina ya taifa, lipewe fursa zilizoainishwa katika sera hiyo, vitambulisho, madirisha maalumu na upatikanaji wa uhakika wa dawa wanazoandikiwa.



Katibu wa Baraza la Wazee Wilaya ya Shinyanga vijijini, Boniphace Boazi, akizungumza kwenye siku ya Maadhimisho ya Wazee duniani yaliyofanyika ki- wilaya katika Kata ya Tinde, Shinyanga vijijini.

**MWENYEKITI**

Akizungumzia changamoto ya umbali, Mwenyekiti wa baraza wilayani humo Edward Lupimo, anasema inatokana na baadhi ya maboma ya zahanati katika vijiji kutokamilika kwa muda mrefu sasa.

"Na ndiyo maana wazee wanakumbana na changamoto ya kusafiri kati ya kilometa saba hadi 10, kufuata matibabu," anasema.

Anatolea mfano vijiji vya Numbili, Buchama na Ngokolo vilivyo na majengo ya zahanati yaliyojengwa kipindi kirefu kwa nguvu za wananchi, lakini Serikali imeshindwa kuyakamilisha na kusababisha wazee kukosa huduma za kiafya kwa karibu.

"Siku moja nilitembelea vijiji ambavyo havina huduma za afya, nikakuta wazee wanapata shida ya kupata matibabu... tunaiomba Serikali maeneo ambayo yamejengwa maboma ya zahanati yakamilishwe kwa ustawi wa wazee hawa," anasema.

**WAZEE**

Joseph Meja ni mzee anayeishi Kijiji cha Nhumbili, Shinyanga vijijini.

Anasema hana kadi ya matibabu bure, hivyo amekuwa akikabiliwa na changamoto kubwa ya kupata huduma ya matibabu.

"Mzee unapokuwa huna kitambulisho huwezi ukapewa matibabu, na hata kama wakikuhurumia watakupa huduma ya vipimo lakini si dawa na lazima utaambiwa ukanunue," anasema na kuongeza:

"Kutokana na ukweli kwamba mimi sina uwezo, basi hurudi tu nyumbani kutumia miti shamba," anasema.

Kwa upande wake Masanja Shija, ambaye ni mzee kutoka kijiji cha Ngokolo, anasema kwenye kijiji hicho kuna Zahanati iliyojengwa kwa nguvu za wananchi.

Anasema tatizo imechukua muda mrefu kukamilika na hivyo kusababisha afuate huduma ya matibabu umbali mrefu, zaidi ya kilomita Saba kwenda Kituo cha Afya Tinde.

"Tunaomba boma la zahanati kwenye kijiji chetu likamilishwe ili wazee tupate huduma ya matibabu kwa karibu, sababu huduma zinapokuwa mbali wakati mwingine tunashindwa kabisa kwenda kwenye tiba, na kubaki tukitumia dawa za asili ambazo hazina vipimo na ni hatari kiafya," anasema.

**MRATIBU**

Mratibu wa Shirika la kutetea haki za wazee mkoani Shinyanga (Tawlae), Eliyasenya Nnko, anasema ili changamoto zinazowakabili wazee ziishe, ni lazima watungiwe sheria yao, na si kuishi kwa sera ili kila kitu kipate kutekelezwa kwa mujibu wa Sheria.

Anasema Shirika lao limekuwa likipigania haki za wazee hasa kwa upande wa matibabu, lakini tatizo ni bajeti ya wazee kutotiliwa maanani kwenye mipango ya halmashauri kwa mujibu wa sheria, na ndio sababu hata vitambulisho vya matibabu bure vinatolewa kwa kusuasua.

"Naipongeza serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli kwa kutambua umuhimu wa wazee kiasi cha kuwaingiza kwenye wizara ya afya," anasema na kuongeza:

"Lakini ninaomba Rais atoe msukumo itungwe sheria ya wazee, ili masuala yao yawe kwa mujibu wa sheria na si kuishi kwa sera ambayo haina nguvu."

**IDARA YA MAENDELEO**

Deus Mhoja ni mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga vijijini.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Hoja Mahiba, anasema kuwa utolewaji wa vitambulisho vya matibabu bure kwa wazee si suala la mjadala ila kinachokwamisha ni ufinyu wa bajeti.

Anasema kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020, Halmashauri hiyo imeshatenga fedha kwa ajili ya vitambulisho bure vya matibabu kwa wazee wote.

"Kwa sasa baadhi ya wazee wameshapigwa picha na taarifa zao zinaingizwa kwenye kumbukumbu za halmashauri yetu," anasema na kuongeza:

"Serikali inatambua mchango wa wazee kwenye taifa hili na itaendelea kutatua changamoto zote moja baada ya nyingine... ukilinganisha miaka ya nyuma na sasa hali iko tofauti kutokana na kujengwa vituo vingi vya afya nchini na upatikanaji wa dawa za kutosha."

Akizungumzia umaliziaji wa Maboma ya huduma za afya, anasema Halmashauri tayari imeshapeleka idadi ya Maboma yote Serikali Kuu.

"Tunasubiri tu fedha zitoke na kuanza kuyamalizia ili wananchi wapate huduma karibu," anaongeza.

**MGANGA MKUU**

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga Vijijini, Dk. Amosi Mwenda, anatolea ufafanuzi suala hilo la madai ya uhaba wa dawa.

Anasema kuna baadhi ya dawa haziruhusiwi kuwapo kwenye zahanati na vituo vya afya, hivyo wazee wanapo ambiwa wakanunue au waende hospitali ya wilaya na mkoa. mahali zilipo ndipo hudai hakuna dawa.

"Halmashauri yetu tuna dawa kwa asilimia 96, lakini kuna baadhi ya dawa haziruhusiwi kuwepo kwenye zahanati na vituo vya afya, sababu hatuna wataalamu wa kutoa huduma hizo," anasema na kuongeza: "Tunakabiliwa na upungufu wa watumishi kwa asilimia 68, ndiyo maana wazee wakiambiwa wakanunue dawa ndipo hudai hakuna dawa."

**MADIRISHA YA WAZEE**

Dk. Mwenda anatolea ufafanuzi pia suala la utengwaji wa madirisha ya wazee.

Anasema kutotengwa kwa madirisha hayo kunatokana na uhaba wa watumishi wakiwamo madaktari bingwa wa magonjwa ya wazee.

"Tulichofanya ni kuandika vibao vya mzee apewe kipaumbele kwanza kwenye huduma za matibabu," anasema.

**DC**

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anasema ameshalitolea maagizo suala la upatikanaji wa matibabu bure kwa wazee kwa maofisa tarafa wilayani humo.

"Nimewaagiza watoe maelekezo kwa watendaji wa kata kuwapatia barua ya utambulisho wazee wote ambao bado hawajapata vitambulisho hivyo," anasema.

Anabainisha kwamba haiwezekani mzee ambaye bado anasubiri kupatiwa kitambulisho cha matibabu bure akose tiba.

"Pamoja na hayo nawaagiza pia wauguzi waache kutoa lugha chafu kwa wazee wetu, kwani nimekuwa nikipokea malalamiko hayo katika vituo vyetu kikiwamo kituo cha Afya Tinde, ambapo nilifika na kulikemea hilo," anasema na kuongeza:

"Kumbukeni wazee hawa ni dawa na hazina ya taifa letu, tuwaenzi kwa kuwatekelezea mahitaji yao na si kuwa nyanyasa."

Mbunge wa viti maalumu mkoani Shinyanga Azza Hilali kupitia chama cha mapinduzi CCM, anawatoa wasiwasi wazee wilayani humo kuwa Serikali yao sikivu chini ya Rais Magufuli, itaendelea kutatua changamoto moja baada ya nyingine.

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Maandalizi ya wanavyuo kuchukia adui rushwa



Baadhi ya wanafunzi kutoka vyuo vikuu na shule za sekondari, wakifuatilia mawasilisho ya mtoa mada wakati wa mjadala wa namna ya kupambana na rushwa nchini Tanzania, kongamano lililofanyika jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

**Na Nickolaus Kasera**

NUKUU ya Baba waTaifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, iliyosambaa na imekunukuliwa mara nyingi ni 'Rushwa ni Adui wa Haki.'

Iko wazi rushwa ni adui wa maendeleo na kwenye kumkumbuka na kumuenzi Mwalimu Nyerere, hatuna budi kuwaandaa vijana ambao ndio viongozi wa leo na kesho.

Mwezi ujao kuna kongamano linalotarajiwa kufanyika katika Chuo Kikuu cha Ruaha, mjini Iringa kujadili mambo hayo.

Mapema mwaka huu, Jaji Mkuu Mstaafu Barnabas Samatta, alipohutubia kongamano iliyofanyika katika Shule ya Sheria iliyopo jijini Dar es Salaam, aliwaasa vijana kuamini kweli rushwa ni adui wa haki.

Jaji Mstaaafu Samatta aliendelea mbali kwa kauli: "Kama sote tuliomo kwenye ukumbi huu tujuavyo, rushwa si kansa iliyoanza jana au juzi….."

Si rahisi kuorodhesha vyote vinavyosababisha au kulazimisha watu kutoa rushwa. Hapo nitazitaja zile sababu kuu tu ambazo ninaamini kuwa ndizo zinazoendeleza kuwapo kansa hii ya rushwa ndani ya nchi yetu."

Jaji Samatta anaziorodhesha sababu zinazomshawishi au kumlazimisha mtu kutoa rushwa ni pamoja na: Kurahisisha au kuharakisha upatikanaji wa huduma, bidhaa au mafao. Anaeleza, ili kupata kile ambacho mtu ana haki chini ya sheria, kukipata, lakini bila utoaji wa rushwa upatikanaji wa kitu au huduma hiyo utachelewa.

Kingine ni mtu kupata asichostahili kitakachofanikisha malengo yake wakati huo au baadaye au kupata zaidi kuliko alivyostahili kwa leango hilo hilo au lingine.

Pia, kuna hofu kuwa bila kutoa rushwa mtu hatapata kile ambacho ana haki ya kukipata. Hapa, aina na kiwango cha msukumo kutoka kwa mwomba rushwa kinaweza kuchangia mwelekeo wa mtoaji rushwa.

Lingine, ni imani kuwa atapata hasara au zaidi asipotoa rushwa kuliko akitoa; kupata ambacho hastahili ili kumkosesha au kumtesa mpinzani au adui wake.

Jambo lingine ni kufanikisha kukwepa au kupunguziwa ulipaji kodi, faini barabarani au aina nyingine ya malipo kwa mamlaka ya dola. Kwa upande wa wala rushwa, haya ndio baadhi ya malengo yanayowafikisha kwenye tamaa ya kutenda uovu huo na kukiuka sheria dhidi ya vitendo vya rushwa.

Mapato (hasa mshahara) yasiyotosheleza uendeshaji wa maisha; kulenga kupata haraka mafanikio zaidi kuliko ambavyo amepata huko nyuma. Pia, kuna kupambana na ukweli kwamba mshahara alipwao Mwafrika si kwa matumizi ya kepeke yake au yale ya familia yake tu. Mara nyingi, mshahara huo unategemewa kusaidia pia jamaa.

Hulka ya ulafi; Hata akiwa tajiri mtu mwenye udhaifu wa tabia ya ulafi (kujilimbikizia mali) hatasita kupita barabara ielekeayo kwenye rushwa.

Kukua kwa familia na hivyo kuongezeka kwa mahitaji ndani ya familia. Pia, kuna kuongezeka kwa majukumu katika jamii na michango inayohitajika kutoka kwenye kila kona inaweza kunyonya uadilifu wa mtu kutegemea na kiwango cha uadilifu wake.

Kuna jambo la kulenga kupata mafanikio au mafanikio zaidi kwenye uwanja wa siasa na kujitengenezea maisha mazuri kiuchumi kwa siku za baada ya kuachapa kazi, kustaafu au kufukuzwa kazini.

Aidha, kuna jambo la kujiwezesha kuwapiku washindani wake katika biashara au shughuli nyingine; kujiongezea heshima katika jamii kwa njia ya utajiri au kujiwezesha kuingia uwanja wa siasa na kupambana akijiamini sana kwa mafanikio makubwa.

Nimekumbuka simulizi ya mhitimu wa shahada ya ya ugavi na ununuzi, ambaye baada ya kufunguka macho aliapa kuwarejeshea wazazi wake digrii yao akisema walimlazimisha kuisomea kwa dai: "Huko ndiko kuna hela. Ni dhahiri tunahitaji mabadiliko ya fikra ndani ya kada ya vijana."

**Anapatikana kwa anwani:samawatiarts@yahoo.com**

## JE, WAJUA?

# Kula mayai kila siku kunaweza kusababisha magonjwa ya moyo



Ulaji mayai au vyakula vilivyochanganywa nayo unapaswa kufanya kwa uangalifu. **PICHA: MTANDAO.**

KULA mayai pamoja na vyakula vingine kunaweza kuusaidia mwili kufyonza madini muhimu kwa afya bora, wataalamu wa afya wanasema.

Kwa mfano utafiti umebaini kuwa kuongeza yai katika saladi, kunachangia kiwango cha vitamini E tunayopata katika saladi.

Hata hivyo, kwa miongo kadhaa sasa, wataalamu wamekuwa wakiumiza vichwa kujua ikiwa ulaji wa mayai ni mzuri au mbaya kwa afya yako.

Yawezekana jawabu la swali hilo linategemeana na mayai mangapi unakula kwa wiki.

Hii ni kulingana na utafiti mpya uliochapishwa kwenye Jarida la Jumuiya ya Matabibu wa Marekani (JAMA). Kwa mujibu wa jarida hilo, kula mayai mawili tu kwa siku kunaweza kusababisha magonjwa ya moyo na hata kifo cha mapema.

Hilo linatokana na kiwango kikubwa cha 'kolestro'- (cholesterol) kinachopatikana kwenye kiini. Yai kubwa moja linakuwa na mpaka miligramu 185 za kolestro kwa mujibu wa Idara ya Kilimo ya Marekani, zaidi ya nusu ya kiwango cha kolestro ambacho Shirika la Afya Duniani (WHO) linashauri mtu ale kwa siku cha miligramu 300.

Na katika takwimu za hivi karibuni kutoka Kamati ya kimataifa ya Yai, kuanzia 2015, inaonyesha kuwa Marekani ni nchi ya tano kwa ulaji zaidi wa mayai duniani, huku kila mtu akila mayai 252 kila mwaka. Lakini nchi hiyo ina matatizo ya magonjwa ya moyo ambayo husababisha asilimia 20 ya vifo.

Japan, ambako ulaji wa mayai unafikia kiwango cha mayai 328 kwa mtu, ilirekodi asilimia 11 tu ya vifo.

"Ulaji wa mayai kiasi cha walau matatu hadi manne kwa wiki, ni sawa," Waliongeza wataalamu wa Uingereza.

### IDADI INAYOSHAURIWA

Mwandishi mwenza wa utafiti huo Norrina Allen, Profesa mshiriki wa madawa ya kinga katika Chuo Kikuu cha Northwestern anapendekeza mtu asile mayai zaidi ya matatu kwa wiki.

Aidha, ushauri unatolewa kwa wanaopenda kula mayai hasa sehemu nyeupe ya yai.

"Siwaambii watu wayaondoe kabisa kwenye milo yao, ila ninapendekeza tu kwamba wayale kiasi," anasema Tom Sanders mmoja wa waandishi wa utafiti huo.

Anabainisha kwamba utafiti huo uliwalenga Wamarekani.

"Wastani wa kiwango cha kolestro kinacholiwa na Wamarekani kinaweza kufikia karibu mayai 600, hiki kikiwa ni kiwango cha wastani wa juu kuliko kile kinacholiwa nchini Uingereza, ambacho ni miligramu 225 kwa siku," anabainisha Sanders.

Utafiti uliochapishwa mapema mwaka huu unapinga madai kwamba kula mayai hakuna madhara kwa afya yetu.

Watafiti walichunguza data 30,000 ya watu waliofuatiliwa kwa miaka 17 na kubaini kuwa kula zaidi ya yai moja hata ukiongezea nusu kwa siku, kunamweka mtu katika hatari ya kupata ugonjwa wa moyo au hata kifo.

"Tulibaini kula zaidi ya yai moja hata ukiongeza nusu kila siku, kulichangia kwa asilimia 6 hatari ya mtu kupata ugonjwa wa moyo," anasema Profesa Allen. Utafiti huo uliangazia data ya aina moja iliyotokana na ripoti ya washiriki wamekula nini.

Waliulizwa walichokula katika kipindi cha mwezi mmoja au mwaka kisha ikafuatiwa na matokeo ya vipimo vya hali ya afya yao kwa hadi miaka 31.

Hii inamaanisha kwamba watafiti walipata kiasi kidogo ambacho washiriki walikuwa wanakula, japo walibadilisha chakula mara kwa mara.

### UTAFITI WA AWALI UNATOFAUTIANA NA HUU

Utafiti mpya unatofautiana na kazi za tafiti za awali ambazo zilibaini kuwa hakuna uhusiano kati ya ulaji wa yai na uwezekano wa hali ya juu wa kupata magonjwa ya moyo.

Lakini Profesa Allen anasema kwamba hizo zilikuwa na sampuli tofauti chache na zilikuwa na muda mfupi wa kufuatilia walaji wa mayai.

Hata hivyo, watafiti wanakiri kuwa huenda kuna makosa katika uchunguzi wao.

Data kuhusu ulaji wa yai zilikusanywa kwa njia ya maswali ambapo ilibidi walioulizwa kukumbuka chakula chao katika kipindi cha miezi na miaka.

Watafiti wengine pia walisema kuwa matokeo ni ya kuchunguzwa na ingawa walieleza uhusiano kati ya ulaji wa yai na kuongezeka kwa hatari ya ugonjwa wa moyo na kifo cha mapema, hawawezi kuthibitisha sababu.

### UWIANO WA HATARI

Utafiti wa JAMA ulichakata taarifa kutoka katika majaribio sita yaliyohusisha zaidi ya watu 30,000 katika kipindi cha miaka 17.

Watafiti wamefikia hitimisho kuwa kula miligramu zaidi ya 300 za kolestro kwa siku, kunaongeza hatari ya kupata magonjwa ya moyo kwa asilimia 17 na vifo vya mapema kwa asilimia 18.

Uwiano huo wa hatari huongezeka zaidi kwenye ulaji wa mayai, na wanasayansi wamebaini kwamba kula mayai matatu au manne kwa siku kunaongeza hatari ya magonjwa ya moyo kwa ulaji wa mayai.

Aidha, wanasayansi wamebaini kuwa kula mayai matatu au manne kwa siku kunaongeza hatari ya magonjwa ya moyo kwa asilimia 6 na vifo vya mapema kwa asilimia 8. Kwa mujibu wa utafiti huo, madhara hayo ya mayai hayaathiriwi na umri, nguvu ya mwili, matumizi ya tumbaku na historia ya kuwa na shinikizo la damu.

"Utafiti wetu umebaini kuwa, endapo watu wawili watafuata aina moja ya mlo na tofauti pekee ikawa ni ulaji wa mayai, basi yule mwenye kula mayai mengi ana uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa ya moyo," anasema Profesa Allen. **BBC**

## RIPOTI

# Uganda yaja na mabadiliko ya sheria

## • Kuruhusu kunyonga wapenzi wa jinsia moja

WAZIRI wa maadili nchini Uganda, Simon Lokodo, ametangaza mipango ya kuanzisha tena sheria inayopinga mahusiano ya jinsia moja, iliyofutwa na Mahakama ya Katiba mwaka 2014.

Waziri Lokodo ameliambia shirika la habari la Reuters kuwa sheria hiyo mpya itamuadhibu hukumu ya kifo yeyote atakayeenda kinyume nayo.

"Sheria yetu ya sasa inatubana sana. Inasema kuwa kitendo hiki ni jambo la kuvunja sheria. Tunataka iwekwe wazi kuwa mtu yeyote anayepigia debe suala hili anaweza kushtakiwa. Wale wanaofanya vitendo vya kushangaza watahukumiwa kifo," anasema na kuongeza:.

"Mahusiano ya aina hii si kitu cha kawaida kwa watu wa Uganda na kumekuwa na waajiriwa wengi shuleni ambao ni wapenzi wa jinsia moja wanaowafundisha watu uongo kuwa mtu anazaliwa na hisia za mapenzi ya jinsia moja."

Mwezi Februari mwaka 2014, Rais Yoweri Museveni alisaini muswada wa sheria wa kuwabana wapenzi wa jinsia moja, lakini sheria hiyo ilifutwa na Mahakama mwezi Agosti mwaka huo huo.

Mabadiliko hayo yalitokea baada ya kubainika kuwa wabunge walipitisha sheria hiyo bila kufuata utaratibu wa kisheria.

Waziri Lokodo amesema muswada mpya ambao utawasilishwa bungeni wiki zijazo unaungwa mkono na wabunge pamoja na Rais Museveni.

"Tumekuwa tukizungumza na wabunge na tumehamasisha idadi kubwa, wengi wao wanakubaliana na jambo hili," anasema.

Waziri Lokodo anasema kuwa nchi yake ipo tayari kwa mashambulio yoyote watakayoyapata juu ya kampeni hiyo.

"Hatupendi kutumiwa, tunajua kuwa kitendo hiki kitawachukiza watu wengi wanaotusaidia kwenye uongozi na masuala ya bajeti...hatuwezi kusikiliza watu ambao wanataka tukubali suala ambalo ni kinyume na maadili yetu," anasema.

Kwa sheria za sasa hivi ambazo ni za kutoka enzi za utawala wa Waingereza, mapenzi ya jinsia moja ni kosa ambalo watu wanaweza kupewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Wanaharakati wanasema sheria hii mpya itaanzisha mashambulizi makali kwa watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Pepe Julian Onziema kutoka shirika la Sexual Minorities Uganda linalofanya kazi na mashirika mengi yanayounga mkono mapenzi ya jinsia moja, ameiambia Reuters kuwa wafanyakazi wake wamejawa na hofu.

"Sheria hii ilipotangazwa kwa mara ya kwanza, iliongeza chuki na ubaguzi, mamia ya watu ambao wanashiriki mapenzi ya jinsia moja wanalazimika kuhama nchi na kugeuka wakimbizi na wengi watafuata endapo sheria hii itapitishwa," anasema na kuongeza:

" Itatufunga sisi kuonyesha ushirikiano wetu hata kufanya kampeni za kuelimisha jamii."

Onziema anasema wapenzi wa jinsia moja watatu na mmoja ambaye alibadilisha jinsia wameuawa ndani ya mwaka huu nchini Uganda, na wiki iliyopita mtu mmoja alipigwa hadi kufa kwa sababu ni mpenzi wa jinsia moja. **BBC**



Waziri wa Maadili wa Uganda, Simon Lokodo. **PICHA: MTANDAO.**

## UCHAMBUZI WA KITABU:
## NA ILZE ALBERTS

# KUPOKEZANA MWANGA/VIJITI (PASSING the TORCH)

KARIBU katika uchambuzi huu wa kitabu cha namna ya kupokezana vijiti. Ni kitabu kizuri sana kwa kila mmoja ambaye anayafikiria maisha, mbali na kujifikiria yeye tu pekee.

Ni kitabu cha mwongozo wa namna unavyoweza kupokezana nafasi na kuwajengea wengine uwezo mkubwa wasihangaike kuanza upya kana kwamba hapakuwa na msingi awali.


Uhifadhi wa utajiri wa kifamilia kuanzia kizazi kimoja hadi kingine ni jambo bora linalofanya maisha ya vizazi vingine yawe rahisi zaidi.

Msingi huu wa familia wa kufikiria kizazi kingine ndiko kumefanya baadhi ya familia ziendelee kudumu kibiashara na kinguvu katika kugusa maisha yao hadi jamii inayowazunguka.

Huu ndio mwaliko wa mwandishi Ilze Alberts kuwa tunapofikiria maisha yetu kwa mfumo wa kupokezana vijiti, basi inasaidia kurahisisha maisha ya vizazi vingine.

Je utafurahi kuona ulichotafuta au mifumo ya biashara ambayo uliitengeneza inakufa baada ya kufa kwako?

Hii inatokea kwa watu wengi ambao wanasahau kupokezana vijiti kwa familia zao kuwa wanapokuwa hai walipaswa kushirikisha uzoefu, maarifa na mbinu kwa wengine ili baadaye kilichotafutwa au kujengwa kiendelee kuwapo hata kama waasisi watakufa.



Kupokezana vijiti kama ilivyo katika riadha ni njia sahihi ya kuifuata kuendeleza ustawi wa familia, jamii na taifa kwa ujumla wake. **PICHA: MTANDAO**

Huu ndio mwaliko wa Alberts katika kutuhimiza kuwashirikisha wengine mifumo ya maisha na biashara ili kilichojengwa kiendelee kudumu vizazi hadi vizazi.

Awali ya yote ili uweze kupokezana vijiti, lazima pawe na maono makubwa ya familia ya namna gani maisha yataacha alama na mchango mkubwa kwa watu wengine.

Hii ikiwa na nguvu kubwa ya mahusiano ya sheria za asili ambazo zinagusa juu ya utoaji na upokeaji. Kuwa ili upate sharti uwe umetoa.

Na hili linaonekana katika familia zenye kutambua uendelevu wa vitu, lazima zifanye kazi ya kutoa nafasi kwa wengine ili pawepo kudumu kwake. Bila hilo haiwezekani kudumu kwa vitu vinavyokosa kujitoa.

Ili utajiri wa familia udumu lazima pawe na uongozi, usimamizi na uhifadhi wa rasilimali watu na mali zinginezo. Lazima wanafamilia wajengewe uongozi wa kijamii, kibiashara na usimamizi wa masuala ya kifedha na uwekezaji.

Kwa familia zinazojua umuhimu huu wa kuwa na uongozi ndizo zinazoweza kufikiria juu ya umuhimu wa kupokezana vijiti na kuonyeshana mwanga kizazi kimoja hadi kingine.

Ni jambo la ajabu pale ambapo kizazi kingine kije kuteseka sababu kizazi kingine kilipuuza kupokezana nafasi na vijiti kwa wengine.

Katika kuandaa kizazi kimoja hadi kingine cha tatu na kuendelea. Umuhimu wa ushirikishwaji wa wanafamilia katika ngazi kuanzia ngazi ya kifikra, kiroho, kiuchumi, kimwili na kihisia kunatoa nafasi kubwa ya ujenzi wa msingi imara kwa vizazi vingine vipya vitakavyokuja hapo baadaye.

Familia ambazo hudumu na kuwa na nguvu zinatambua nafasi ya wanafamilia kukua kiuchumi, kiroho na kifikra kama mihimili mikubwa ya ujenzi wa biashara na uwekezaji.

Hili huanzia kufundishwa watoto wao hadi wanafamilia namna hizi ngazi zinakuwa msingi imara kwao.

Ulaji mzuri ni hitaji muhimu sana la kudumu kwa vizazi na utajiri wa kifamilia. Ulaji mbovu unafupisha safari ndefu ya upokezanaji wa vijiti au nafasi kwa watu wengine.

Ulaji mbovu husababisha afya kuwa dhaifu na kukaribisha magonjwa kama kisukari na presha na mwisho watu hupoteza uhai wao.

Kupoteza nafasi zao za kuishi kunaambatana na kupoteza uzoefu na maarifa walioyakusanya miaka mingi kushindwa kuwashirikisha wengine.

Hivyo ulaji bora, ufanyaji wa mazoezi na kujali afya kama familia kunasaidia kudumu kwa familia kwa kipindi kirefu na hata uhifadhi wa utajiri wa kifamilia huendelea kudumu.

Afya bora kifamilia haishii kuwa na ulaji bora pekee. Ila ni pamoja na nafasi za mapumziko mazuri, kuboresha akili, roho na mwili. Na jambo lingine ni maisha yanayojaa shukrani. Kipengele hiki ni muhimu kwa ustawi wa familia na utajiri uliojengwa na wanafamilia.

Mapumziko na usingizi mzuri ni hitaji muhimu kwa afya za wanafamilia kimwili na kiakili. Maboresho haya yakiwa vizuri ndio unajenga uimara wa wanafamilia wanavyoona maisha yalivyo.

Familia yenye utajiri na kuwajengea wengine uwezo wa kutengeneza utajiri ina nafasi kubwa ya kuchangia maendeleo ya jamii.

Ushiriki wa familia nyingi zenye utajiri kwa mambo ya jamii ni pamoja na uwezo wa kutoa upo katika mikono yao. Hili linaleta maana kubwa maishani kwa familia nyingi ambazo zimeleta mchango mkubwa kwa jamii.

Tunaona mifano kama ya familia ya (Reginald) Mengi, (Said Salim) Bakhresa, (Jomo) Kenyatta. Zote hizi zina mchango mkubwa kwa jamii katika kuleta athari chanya.

> Mapumziko na usingizi mzuri ni hitaji muhimu kwa afya za wanafamilia kimwili na kiakili. Maboresho haya yakiwa vizuri ndio unajenga uimara wa wanafamilia wanavyoona maisha yalivyo.

Mwandishi katika kitabu hiki anatualika nasi kuchukua hatua hii sasa kuhakikisha tunajenga msingi bora kwa wanafamilia wetu ili siku tunapokuwa hatuna uwezo au nafasi zetu zimefika ukomo wa kuishi, basi wengine wataendelea pale ambapo sisi tuliishia.

Kwa namna hii inawapa nguvu zaidi vizazi vingine kutohangaika wapi pakuanzia.

Kuwa msingi imara kwa wengine siku utakapoondoka uwe umewaachia msingi bora wa wao kusimama na kusonga mbele.

Katika huu uchache wa kitabu hiki tuendelee kuhimizwa ili kufikiri kuwa nafasi zetu ni kama vijiti. Ifikapo zamu ya kupokezana wape ruhusa wengine kuchukua nafasi.

Pia iwe nafasi ya kuwaangazia mwanga wengine wasipate shida wapi wangeanzia. Hivyo ujuzi wako, mbinu, mifumo, maono washirikishe watu wa familia yako, ukiwa unawaandaa kuchukua jukumu la kuendeleza pale utakapoishia.

***Mchambuzi anapatikana kwa namba***
***+255 676 559 211***
***raymondpoet@yahoo.com***



WADAU
SABATO
KASIKA

# Sauti za wadau

MTINDO wa baadhi ya wanafunzi kwenda na simu shuleni bado ni changamoto, ingawa taratibu za wizara husika haziruhusu. Wadau wa elimu wanasemaje?



**DEBORAH MASANGURA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

INAWEZEKANA baadhi ya wazazi na walezi wanaamini na wanasema kwamba wanafunzi kuzuiwa kwenda na simu shuleni ni utaratibu na sheria zilizopitwa na wakati.

Lakini niwakumbushe kuwa hakuna sheria inayopitwa na wakati, mbona zipo sheria za tangu ukoloni na zinatumika?

Jamii ijue kuwa hata huko Ulaya ambako mambo hasa ya kisasa yanatokea, wanatafuta jinsi ya kuwaepusha watoto wao na mitandao.

Lakini cha ajabu ni kwamba sisi watu ambao tuko nyuma kimaendeleo tunataka kujiingiza kwenye mambo makubwa bila kujua kuwa yanatuharibu. Hivi kweli wanaokwenda na simu shuleni wanajitakia mema katika elimu?

Mimi ningeishauri serikali kuendelea kushikilia msimamo wa kuzuia wanafunzi kuwa na simu shuleni ama wawe nazo lakini wanapofika shuleni zikusanywe na kutunzwa katika ofisi ya mkuu wa shule hadi kumalizika muda wa masomo ndipo wapewe kuwasiliana na wazazi wao na hasa wanafunzi wa bweni na wale wa kutwa wapewe na kurudi nazo nyumbani.

Lakini ingekuwa ni bora zaidi iwapo wangezuiwa kabisa na hakuna ubaya wowote, kwani vinginevyo zitawaweka pabaya. Nasema hivyo kwa sababu ni rahisi kujihusisha na matendo maovu kwa kutumia simu hizo hizo.

Kwa maana hiyo ndiyo sababu kubwa za kuwazuia wanafunzi kumiliki simu kwa lengo la kuwaokoa kwenye mambo ya hatari, ambayo yanaweza kuwapata kupitia simu za mkononi ambazo kimsingi zina faida na hasara.



**STELLA MAHUDA (MKAZI WA MJINI IRINGA)**

KWANZA kabisa nijitambulishe kuwa mimi ni mdau wa elimu. Na kuhusu suala hili la simu ni kwamba sisi Watanzania bado tuna miaka mingi zaidi ya kujifunza matumizi sahihi kwa njia ya simu za mkononi, siyo kuruhusu tu bila kuyajua, kwani kufanya hivyo tutazidi kuwapoteza vijana wetu na hasa wanafunzi.

Nina sababu za msingi za kusema hayo, kwasababu kuna shule nyingi, ambazo wanafunzi wamekuwa wakikamatwa na simu na hata kusimamishwa au kufukuzwa shule ikiwamo hiyo ya Mbeya ambayo, mkuu wa mkoa aliingilia kati baada ya kuona wanakoelekea wanafunzi siko.

Labda niwakumbushe wazazi kwamba mawasiliano mengi ya wanafunzi katika simu huwa yanahusu masuala ya mapenzi, ingawa wapo wanaohalalisha matumizi ya simu kwa wanafunzi, eti wanapakuwa masomo, lakini ukweli ni kwamba wengi wao wanazitumia kwa ajili ya mawasiliano yanayohusu mahusiano ya kimapenzi na pia kuangalia picha na video chafu.

Kwa mazingira kama hayo sioni umuhimu wowote kwa wanafunzi kuwa na simu shuleni kwa kisingizio kuwa zinawasaidia kutafutia mambo ya masomo, huo ni uongo ambao hautakiwi kuungwa mkono na mzazi yeyote anayempenda mwanawe. Watu wafundishwe matumizi sahihi ya simu.

Lakini pia tutambue kuwa kuruhusu simu shuleni ni kushusha kiwango cha elimu kwa wanafunzi...wanaweza kutumiana ujumbe wa kukataliwa na wapenzi wao na kujikuta wakichanganyikiwa na kufanya vibaya katika masomo yao, ndiyo maana nasisitiza kuwa wanafunzi wasiwe na simu shuleni.



**OTHINIEL MNKANDE (MWALIMU EFFORTS SEKONDARI, BAGAMOYO)**

WANAFUNZI kuwa na simu ni marufuku kabisa shuleni kwetu, kwani tunatambua madhara yake. Mtindo wa baadhi ya wazazi kuwapa watoto wao simu na kwenda nazo shuleni wakidhani kuwa wanawapenda, wajue kuwa wanawaharibia maendeleo yao ya shule.

Kwanza kabisa wazazi wenye mtindo huo ni vyema wakapima faida na hasara za simu za mkononi ili wagundue kuwa hasara ni kubwa kuliko faida. Ingawa sina takwimu zozote, lakini naamini simu zimechangia wanafunzi wengi na hasa wa kike kujiingiza kwenye mambo ya ngono bila wengine kutarajia.


Wapo ambao unakuta wanaombwa namba za simu zao na kuzitoa wakidhani kwamba wanaozichukuwa wanakuwa na nia njema, lakini matokeo yake wanawaingiza kwenye vishawishi na kujikuta katika hatari ya kufanya ngono.

Pia wapo, ambao wamekuwa wakizutumia kwa kuangalia picha za ngono na mambo mengine machafu yanayokwenda kinyume na maadili.

Kwa mazingira kama hayo ni bora wanafunzi wasiende na simu shuleni au wasimiliki simu kabisa.

Ingawa katika kundi hilo wapo wachache wanaozingatia matumizi sahihi, lakini ni bora wakazuiwa tu ili kuwanusuru na matatizo ambayo yanaweza kuwakuta.

Inawezekana wapo wanaoamini kwamba utaratibu wa kuzuia wanafunzi kwenda na simu shule umepitwa na wakati.



**MIRIAM LUWANDA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWA maoni yangu siyo sahihi wanafunzi kwenda na simu shuleni, kwani utafiti unaonyesha kwamba mitandao ya simu na intaneti inachangia kuwaharibu, hivyo kuwaruhusu waende na simu shuleni ni sawa na kutoa ruhusa ya kuwaingiza kwenye matatizo.

Mbona miaka ya nyuma simu hazikuwepo lakini wanafunzi walikuwa wanasoma vizuri tu?

Lakini leo wakati huu wa utandawazi ndiyo mambo yamekuwa mabaya kabisa kwenye elimu, wanafunzi wana simu ambazo wao na wazazi wao wanadhani kuwa zinasaidia lakini wanafanya vibaya kwenye mitihani.

Hivyo ni vyema wale wanaong'ang'ania kwenda na simu shuleni wakajua kuwa ni hatari kwa mustakabali wao wa baadaye kwenye suala zima la elimu.

Elimu haitakiwi kuchanganywa na mambo mengine ya kipuuzi kwani mwisho wake ni kushindwa vibaya.

Ningeshauri kwamba wanafunzi wanaokwenda na simu shuleni wafukuzwe ili wasiwaharibu wenzao kwani elimu haiwezi kuchanganywa na mzaha, hivyo wanaotaka kusoma waangalie mbele kwanza na kuachana na mambo ya simu, kwani hizo watazitumia tu wakishamaliza masomo yao.

Ushauri wangu ni kwamba siyo vibaya kwenda na wakati, katika matumizi ya simu za mkononi, lakini pia kuna haja ya kujua kuwa huo wakati unatupeleka wapi.



**CHRISTINA LAZARO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NILIKUWA siamini kama maisha yanakwenda yanabadilika kiasi hiki, ambacho sasa imekuwa ni kama jambo la kawaida kusikia wanafunzi wanakwenda na simu shuleni, huku wakijua wazi kuwa taratibu haziruhusu.

Lakini tukio la huko Mbeya ambalo mkuu wa mkoa alichapa baadhi ya wanafunzi waliokuwa wakituhumiwa kwa makosa mbalimbali likiwamo hilo la kwenda na simu shuleni, liwe fundisho kwa wazazi na hata kwa wanafunzi wenyewe, kwani inawezekana wapo wanaomiliki simu bila wazazi wao kujua.

Hii si salama kwa mustakabali wa maendeleo yao kielimu, ni vyema wakaachana na tabia hiyo haraka. Simu ni kwa ajili ya mawasiliano, lakini pia ni anasa kulingana na jinsi mtu anavyoitumia. Wanafunzi kuwa na simu si vizuri. Jambo la msingi ni kufuata taratibu zilizowekwa na serikali za kutokwenda na simu shuleni, kwasababu zina matatizo.

Ndiyo maana nikasema ni mawasiliano na pia ni anasa, zinawafanya baadhi yao kutokuwa makini katika masomo na kufikiria mambo ya nje ya shule. Wala wasidhani sheria ya kuzuia simu shuleni imepitwa na wakati, kwani wakati huu wa utandawazi ni mbaya zaidi kwao wanatakiwa kuwa makini badala ya kudandia kila kitu na kudhani ni kizuri.

Vipo vingine havifai kabisa na hasa hizi simu kwa wanafunzi ni mbaya, hivyo ni vyema tuwe makini na watoto wetu kuhusu matumizi ya simu.



# Waeleza changamoto soko la mazao

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

BAADHI ya wakulima wadogo wa Kijiji cha Ihombe, Kata ya Utengule Usongwe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwatafutia masoko ya mazao wanayozalisha badala ya kuishia kuwahamasisha kulima.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini hapo, wakati wataalamu kutoka Kampuni ya Balton inayojihusisha na masuala ya kilimo, wakitoa elimu ya kilimo cha kisasa kwa wananchi hao.

Mmoja wa wakulima hao, Joshua Shombe, alisema katika kijiji hicho wananchi wamehamasika kulima, lakini kinachowakwamisha ni masoko ya mazao hayo kutopatikana kirahisi hali inayowafanya wakate tamaa ya kuendelea kuzalisha.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili wamezalisha mahindi ya kutosha, lakini mpaka sasa wanahangaika kupata soko hali inayowafaya kuwaomba wataalamu wanaotoa elimu ya kilimo bora wawasaidie hata kupata soko.

"Sisi hatusubiri mtu atulazimishe kulima na tunawashukuru wawezeshaji kwa kutusaidia elimu ya kilimo cha kisasa, lakini tunaomba serikali yetu itusaidie hata kupata masoko maana kuna baadhi ya mazao hayana soko kabisa kwa sasa," alisema Shombe.

Naye Elizabeth Mwasile, alisema kutokana na kukosekana kwa soko la mahindi katika Mkoa wa Mbeya, ni bora serikali iangalie namna ya kuanzisha viwanda ambavyo vitawasaidia wakulima kupata soko la mazao hayo.

Alisema endapo vitaanzishwa viwanda, wakulima wanaweza wakawa wanachakata mazao yao na kuyaongezea thamani kabla ya kuuza tofauti na sasa wanauza mazao ghafi moja kwa moja.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Utengule Usongwe, George Yola, alikiri wakulima wa kata hiyo kuhamasika kulima, lakini changamoto inayowakabili ni soko.

Alisema soko la mazao ya kilimo huwa linabadilika na halina kanuni maalumu kwa madai kuwa wakati mwingine bei zinapanda na kushuka kwa kiasi kikubwa hali inayowakatisha tamaa wakulima.

"Sisi kazi yetu ni kuwahamasisha wakulima kuzalisha kwa tija kwa kufuata hatua za kilimo bora kuanzia shambani mpaka kuhifadhiwa, lakini kuhusu soko huwa sio jukumu letu, kwa sasa wakulima wengi wanalima kwa kubahatisha," alisema Yola.

Naye Ofisa Kilimo kutoka Kampuni ya Balton, Samwel Gambalela, alisema zipo sababu mbalimbali za wakulima kupata hasara kwenye shughuli zao hizo ikiwamo sera za nchi.

Alisema ili wakulima wapate masoko ya mazao yao lazima uwepo ushirikiano kati ya serikali na wadau wengine zikiwamo kampuni binafsi kutafuta mbinu za kupata masoko.

# Walilia wakalimani lugha za alama

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JAMII imetajwa kuwa chanzo cha kukandamiza haki ya kupata elimu kwa wenye ulemavu wa kusikia walio kwenye umri wa kwenda shule kwa madai ya kutopatiwa wakalimani wa kutafsiri lugha za alama, vifaa maalum vya kusikia na wengine kufichwa ndani.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Mbeya, Tusajigwe Mwalwega, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu tathmini ya watoto wenye ulemavu wa kusikia kupata elimu.

Tusajigwe alisema mtoto mwenye ulemavu huo anakosa haki ya kusoma kwa sababu ya ulemavu alionao na baadhi ya familia kuamini kumpeleka shule ni kupoteza muda.

Aliiomba serikali na familia kutengeneza mazingira rafiki ya mtoto huyo ili apate haki yake ya msingi ya elimu na kutimiza ndoto zake kama ilivyo kwa wengine.

"Nilikwenda ofisi moja kupata huduma, lakini kulikuwa na changamoto ya mawasiliano na wahusika, niliwaomba wanitafutie mkalimani ili nieleze shida yangu wakaniambia ninaringa ninao uwezo wa kuongea kama wengine, nilijisikia vibaya sana hii inaashiria kuwa bado kuna ubaguzi na hatuwezi kuhudumiwa vizuri kama wengine," alisema Tusajigwe.

Aliwaomba wasamaria wema wanaoshuhudia watoto wenye tatizo hilo kufichwa ndani kutoa taarifa kwenye chama chao ili kuangalia namna ya kuwasaidia kupata haki ya kusoma na huduma nyingine.

Alisema mtoto mwenye ulemavu huo asionekane mzigo ndani ya familia bali anaonekane baraka kama ilivyo kwa watoto wengine na kwamba akipatiwa elimu anaweza kuwa mkombozi ndani ya familia.

Esther Solomon, mkazi wa Kata ya Uyole, alisema ili kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia miongoni mwa jamii kila mmoja anatakiwa kuwajibika kwa kuhakikisha anaripoti vitendo hivyo.

Alisema vitendo kama ubakaji, ulawiti na vipigo vilivyopitiliza kwa kinamama vikiripotiwa bila woga na wahusika wakichukuliwa hatua za kisheria jamii itabadilika.

Mkurugenzi wa Chuo cha Wakalimani wa lugha za alama jijini Mbeya, Philemon Mwansasu, alisema kupitia chuo hicho watoto wenye tatizo hilo watapata elimu na kutimiza ndoto zao.

Alisema chuo hicho kinaanzishwa kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu wakalimani kwenye shule na pia kutoa nafasi kwa watoto wenye ulemavu wa kusikia kufanya vizuri kwenye mitihani yao.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemas Mwangela, akijiandikisha kwenye daftari la kupigia kura katika Kituo cha Mwenge wilayani Mbozi mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM YASSIN**

# Wakulima wakumbushwa kuongeza thamani mazao

**Na Grace Mwakalinga, SONGWE**

SERIKALI imewahimiza wakulima kuongeza thamani ya mazao wanayozalisha ikiwamo kutengeneza bidhaa na vifungashio ili kujihakikishia soko la ndani na nje ya nchi.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, wakati akizungumza na wakulima kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Songwe.

Hasunga alisema wakulima wamejitahidi kulima mazao mengi, lakini changamoto iliyopo ni uhakika wa soko, hivyo wakiweza kuongeza thamani ya mazao yao kwa kuyafanya bidhaa watafanikiwa kuuza.

"Nawasihi wananchi tuwe wazalendo kwa kupenda vya kwetu, wema huanzia nyumbani huwezi kujiita Mtanzania wakati hupendi vya kwenu, tuwaunge mkono wajasiriamali, lakini tusisite kuwashauri ili kuboresha hii itasaidia hata wageni kuiga uzalendo huu," alisema Hasunga. Aliwasisitiza wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo na kwamba itasaidia kuvuna mazao mengi na yenye ubora ambayo yataendana na ushindani wa soko la dunia.

Miongoni mwa wakulima hao, Gwantwa Lutufyo, alisema wanajitahidi kuongeza thamani ya mazao, lakini changamoto ni kushindwa kumudu gharama za kununua vifungashio, pia hawana utaalamu wa kutosha katika kutengeneza ili viendane na soko la ushindani.

Alisema amekuwa mkulima wa mahindi kwa miaka saba sasa, lakini wakati mwingine mazao yake huozea ndani kwa sababu ya kukosa soko, hivyo elimu ya kuongeza thamani ya mazao aliyoipata itamsaidia kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na mahindi.

Boniface Mwazembe kutoka Kijiji cha Senjele, alisema wakulima wanakabiliwa na changamoto ya pembejeo za kilimo ikiwamo mbolea na dawa.

Aliishauri serikali msimu ujao wa kilimo kusimamia ugawaji wa pembejeo za kilimo hasa maeneo ya vijijini kunakodaiwa kuwapo na uchakachuaji mkubwa.





## Waombwa kutembelea wenye mahitaji

**Na Ibrahim Joseph, Dodoma**

TAASISI za kifedha na watu binafsi zimeombwa kutembelea vituo vya yatima na watu wenye mahitaji ili kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili kwa kuwa ni sehemu ya jamii.

Wito huo ulitolewa na Meneja wa Benki ya NMB tawi la Dodoma, Harold Lambileki, alipokuwa akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa kituo cha watoto yatima cha Nyumba ya Matumaini kilichopo Miyuji jijini hapa.

Lambileki aliziomba taasisi za fedha na watu binafsi kujenga tabia ya kutembelea vituo vya kutunza yatima na wenye mahitaji ili kuona umuhimu wa kusaidia katika maeneo hayo.

"Wakati mwingine mtu akisikia vituo vya kutunza yatima anaweza kufikiri kawaida tu, lakini ukifika eneo husika unaona jinsi walivyo na changamoto ya mahitaji ya kila siku, hivyo ninaomba tujenge tabia hiyo ya kufika kuwaona wenzetu hawa," alisema.

Alisema kupitia watu binafsi au vikundi, wanaweza kupeleka msaada wowote kwenye vituo hivyo kutunza wahitaji kutokana na kukabiliwa na changamoto ya mahitaji kila siku.

"Kwa mtoaji anaweza kuona kama ametoa kidogo, lakini ukipeleka pale utaona kumbe umesaidia kitu kikubwa sana, unaweza kupeleka hata sukari kuanzia kilo moja na mwingine akapeleka unga wa kula ni msaada tosha kwa hawa wenzetu," alisema.

Aidha, alisema katika Wiki ya Huduma kwa Wateja, wafanyakazi wa tawi hilo walichangishana zaidi ya Sh. milioni mbili ili wanunue vitu na kukabidhi katika kituo hicho.

Alitaja baadhi ya vitu walivyoweza kupeleka ni unga wa mahindi na ngano, sukari, mafuta ya kujipaka, sabuni za kuongea na kufulia, jiko la gesi pamoja na mtungi wake na juisi na pipi vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni mbili.

Mkuu wa kituo cha kulea watoto yatima cha nyumba ya matumaini, Sista Aurea Vicent, alisema kituo kina watoto 63 wanaotunzwa hapo.

Sista Vicent alisema katika idadi hiyo wapo wanaosoma shule za msingi, sekondari na wengine wanasoma vyuo vikuu kwa kulipiwa na kituo.

Aliongeza kuwa watoto wanaotunzwa hapo ni wale ambao ni yatima na wazazi wao walifariki na ugonjwa wa Ukimwi kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alibainisha kuna baadhi ya watoto wachache ambao sio waathirika wa Virusi vya Ukimwi (VVU) wanaotunzwa hapo kutokana na kupelekwa na Idara ya Ustawi wa Jamii kwa kukosa watu wa kuwatunza.

"Wengi wa watoto waliopo hapa waliletwa wakiwa kwenye hali mbaya, lakini tunamshukuru Mungu tunajitahidi kuwasaidia matibabu na lishe mpaka wanakuwa hivi walivyo, watoto hawa wanahitaji ukaribu katika kuwahudumia kuanzia matumizi ya dawa mpaka lishe," alisema.

# Mgogoro uongozi sokoni wamalizwa

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

HATIMAYE mgogoro wa uongozi katika Soko la Sabasaba jijini Dodoma, umepatiwa ufumbuzi baada ya kudumu mwaka mmoja na nusu bila kuwa na viongozi.

Mgogoro huo ulitokana na wafanyabiashara hao kukosa imani na viongozi wao kwa madai kuwa wanatumia vibaya madaraka na kutosoma mapato na matumizi.

Ufumbuzi huo umepatikana baada ya Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, kuwakutanisha wafanyabiashara na viongozi hao ili kupata ufumbuzi wa mgogoro huo, na kuchaguliwa viongozi wa mpito ambao watakaa madarakani kwa siku 90.

Chibago alisema wafanyabiashara hao kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu wameishi bila uongozi kutokana na mgogoro uliokuwa umejitokeza na kuwavua madaraka viongozi hao.

Alisema katika kipindi chote hicho wafanyabiashara wao walikuwa hawana viongozi hadi uongozi wa jiji ulipoamua kukaa pamoja ili kuweza kutatua mgogoro huo.

"Tangu viongozi waliokuwa madarakani kwa kipindi cha nyuma waondolewe madarakani wafanyabiashara walikosa viongozi, hali ambayo imechangia kukosa maendeleo ya kiuchumi kwa upande wao," alisema.

Alisema huduma muhimu zilikosekana kama upatikanaji wa mikopo kutokana na kutokuwapo kwa viongozi wanaotambuliwa kisheria.

Katibu wa muda wa soko hilo aliyechaguliwa, Denis Athumani, aliomba wafanyabiashara kuwa na imani na uongozi huo wa mpito kwa kuwa utafanya kazi kwa mujibu wa katiba yao.

Athumani alisema muda mrefu wamekaa bila viongozi, hivyo kuchaguliwa kwao watahakikisha wanatimiza mahitaji yanayohitajika kwa wafanyabiashara wote.

Naye Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, aliwataka wafanyabiashara kuvunja makundi na sasa wanafanya kazi ili kujiletea maendeleo.

Viongozi wengine waliochaguliwa Frank Lengeju ambaye atakuwa mwenyekiti wa muda, Makamu Mwenyekiti Majdi Hot, Katibu Msaidizi Nyamsuka Nyamsuka na mtunza hazina, Shukran Chizoza.



Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Tawi la Benki ya NMB Dodoma, Pamela Mahari (kushoto), akimkabidhi Sista Aurea Vicent (kulia), msaada wa vitu mbalimbali kwa ajili ya watoto wa kituo cha Nyumba ya Matumaini Miyuji, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bosi Zimamoto aeleza umuhimu wa wastaafu

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji, Thobias Andengenye, amesema wastaafu wa jeshi hilo bado wana jukumu la kuendelea kulishauri jeshi hilo katika utendaji kazi ili kuongeza ufanisi zaidi.

Andengenye aliyasema hayo katika hafla ya kumuaga Kamishna Jenerali mstaafu wa jeshi hilo, Pius Nyambacha pamoja na Kamishna mstaafu wa jeshi hilo ambaye alikuwa Mkuu wa Utawala, Michael Shija.

Alisema wanatakiwa kuendelea kulishauri jeshi hilo na kuunga mkono jitihada za serikali za kuimarisha sekta mbalimbali ikiwamo chombo hicho cha zimamoto na ukoaji.

"Wastaafu hawa wamelitumikia jeshi letu kwa muda mrefu na leo tunawaaga, lakini niwaambie kuwa wana wajibu wa kuendelea kulishauri jeshi hili pamoja na kuelezea yanayoendelea kufanyika, maboresho ambayo yamefanyika, maslahi ya watumishi, vitendea kazi pamoja na mambo mengine kama miundombinu," alisema Andengenye.

Aidha, Andengenye alisema watumishi waliopo wanatosha katika kuwafikishia wananchi huduma ya jeshi hilo katika maeneo mbalimbali.

Hata hivyo, alisema hakuna mahali walishindwa kufanya kazi kutokana na upungufu wa watumishi.

Naye Kamishna Jenerali mstaafu Nyambacha, alisema alivyoliacha jeshi sivyo lilivyo kwani sasa kuna mabadiliko makubwa yalioongezeka katika utendaji kazi licha ya kuwa na upungufu wa vifaa.

Alisema wananchi wamepata uelewa wa nini maana ya moto na namna ya kujikinga nao, hivyo elimu iendelee kutolewa ili kuwa na uelewa mpana zaidi.

Kwa upande wake, Kamishna mstaafu Shija alisema jeshi hilo likipata watumishi 6,000 itasaidia kuwafikishia wananchi huduma kwa urahisi kwani wana mpango wa kufika wilayani hadi ngazi ya vijiji.

"Nitawakumbusha askari wenzangu, kwani kazi yetu ni ya wito, unapookoa maisha na mali unapata uchungu sana unapoona mali inateketea, mfano tukio la ajali mkoani Morogoro vifo vilivyotokea vilikuwa vingi... sisi waokoaji itatuwia ngumu kuona kwamba kwa nini watu wanakufa," alisema.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa mapema yanapotokea matukio mbalimbali ya moto kuliko kuendelea kutoa lawama kuwa jeshi hilo linachelewa kufika maeneo ya matukio.



# Shule za Z'bar zapania kuondoa alama 'zero'

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MWAKILISHI wa Viti Maalum kupitia Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mkoa wa Kaskazini Unguja ambae ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema mkoa huo umefanikiwa kupunguza alama ya 'zero' kwa wanafunzi wa kidato cha sita na cha nne ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Aliyasema hayo huko Mkoa wa Kaskazini Unguja, katika hafla ya kukabidhi vyakula kwa uongozi wa kamati za shule za mkoa huo huko Mahonda na kusema serikali itaendelea na jitihada zake za kuhakikisha wanafunzi wa madarasa ya mitihani ya taifa wanafanya vizuri katika mitihani yao ya mwisho ili kuhakikisha alama za zero na daraja la nne kwa kidato cha nne zinaondoka katika shule za Zanzibar.

Alisema mkakati wa wizara ni kuhakikisha wanaondoa alama hizo pamoja na ufaulu wa kiwango cha daraja la nne katika shule za Zanzibar ili kuona kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa madarasa hayo unaimarika zaidi ikilinganishwa na sasa.

Pia aliwataka wanafunzi kushughulikia masomo yao pamoja na kujisomea kwa bidii ili waweze kufanya vziuri mitihani yao ya taifa na kufanikisha azma ya serikali kupitia Wizara ya Elimu ya kuondoa alama za zero kwa mkoa wao.

Naye Msaidizi wa Katibu Tawala Huduma za Jamii Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mshamara Choum Kombo, alisema zaidi ya wanafunzi 3,000 wa mkoa huo wanatarajiwa kufanya mitihani ya taifa ya kidato cha nne.

Aliseme lengo la kuweka kambi hizo ni kuwatayarisha na kuhakikisha wanafanya marudio ya masomo yao kwa ufanisi ili waweze kufaulu vizuri katika mitihani yao.

Zaidi ya Sh. milioni tisa zimetumika kwa ajili ya kununua mchele na mafuta kuwasaidia wanafunzi wa shule 23 wa Mkoa wa Kaskazini Unguja waliokuwapo katika kambi za matayarisho ya mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheri, akizungumza wakati wa mkutano wa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein (wa pili kulia) na watendaji wa wizara za SMZ, Kisiwani Pemba, uliofanyika Wawi Pemba, juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Serikali kutafiti wanafunzi kutofanya vizuri mtihani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SERIKALI Mkoa wa Kusini Unguja imesema itahakikisha inafanya utafiti ili kubaini matatizo yanayosababisha kutofanya vizuri kwa wanafunzi wa shule za mkoa huo katika mitihani yao ya taifa.

Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mahmoud Mohammed, alisema hayo wakati alipokuwa akizungumza na kamati ya Shule ya Paje, walimu na wanafunzi wa kidato cha nne kuhusu maandalizi ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne unaotarajiwa kufanyika mwezi Novemba, mwaka huu.

Alisema ni lazima kufanywe utafiti wa pamoja baina ya viongozi wa mkoa huo, kamati za elimu, walimu, wazazi na walezi kuhusu kuwapo kwa matokeo mabaya ya wanafunzi na kurudisha nyuma mipango ya serikali ya kuimarisha sekta ya elimu.

"Ni vyema tukawa na ushirikiano na mikakati ya pamoja ili kuleta matokeo mazuri katika mkoa wetu na kuwaandaa vijana hawa kufikia malengo yao, pia kuongeza idadi ya wataalamu," alisema Ayoub.

Vile vile, alisema utafiti unaonyesha kuwa matokeo ya mwaka jana ya kidato cha nne hayakuwa mazuri kwa kutokupatikana daraja la kwanza, jambo ambalo linahitaji kuwekewa mikakati madhubuti ili kuongeza ubora wa elimu na kupata mafanikio.

"Tuwatengenezee vijana wetu mweleekeo mzuri kuhusu hatima ya maisha yao kwa kuwapatia elimu kwa kuwa ndio msingi wa maisha yao ya sasa na baadaye, hivyo ni lazima tushirikiane juu ya hili kubaini sababu za kutofanya vyema kwa wanafunzi wa mkoa huu," alisema Ayoub.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kuanzisha shule ya kidato cha tano na sita katika mkoa huo, hivyo ni vyema kufanyike maandalizi ya kuwaanda vijana ili waweze kuitumia vyema fursa hiyo.

Hata hivyo, aliwaagiza viongozi wa majimbo kutekeleza wajibu wao wa kuwatumikia wananchi ikiwamo kusaidia kuondoa vikwazo vya elimu kwa shule zilizomo katika majimbo yao.

Mbunge wa Jimbo la Paje, Jaffar Sanya Jusa, aliahidi kutoa zawadi ya Shilingi milioni moja kwa kila mwanafunzi atakayepata ufaulu wa daraja la kwanza katika Shule ya Paje na kukabidhi fedha taslimu Sh. 300,000, kwa ajili ya kambi ya wanafunzi wa shule hiyo.

# Jamii yaonywa kuwanyanyasa watoto wa kike

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

JAMII nchini imetakiwa kutimiza wajibu wake kwa kuwapa watoto wa kike malezi bora na haki za msingi, ili waweze kufikia matarajio yao ya kujikomboa kielimu na kiuchumi pamoja na kuwa wajenzi wazuri wa taifa.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, alisema sio vyema kuwabagua watoto kati ya wanawake na wanaume kwa kuwa wote wana haki sawa mbele ya jamii.

Akizungumza katika kongamano la kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Kike Duniani kwenye ukumbi wa Sheikh Idriss Abdulwakil Kikwajuni mjini hapa, Castico alisema matukio mengi ya udhalilishaji dhidi ya wasichana yanatokana na jamii hasa wanaume kuwaona watoto hao kuwa ni sawa na bidhaa mbovu.

Katika kongamano hilo lililohudhuriwa na wanafunzi wa shule mbalimbali pamoja na wadau wa masuala ya watoto, Waziri Castico aliwataka wanajamii kujua kwamba kumkandamiza mtoto wa kike ni kuiangamiza nchi.

"Ukitaka kuiangamiza nchi yako wafanye wanawake wakandamizwe, wasiwe na uhuru, wasifanye chochote, hiyo nchi inapotea kwa sababu mtoto hatalishwa, hatavishwa, baba hatasaidiwa, mama mwenyewe hatafanya jambo lolote. Kwa hivyo ili nchi iendelee vizuri ni pamoja na kuinua morali ya wanawake," alisema Castico.

Alieleza kuwa, mambo ya kukatisha ndoto za watoto wa kike yanapingana na misingi ya haki za binadamu pamoja na miongozo ya dini, kwa kuwa wanapopata watoto majukumu ya ulezi hawayawezi kwa kuwa wakati wao haukuwa umefika.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafanya kila jitihada kuhakikisha udhalilishaji dhidi ya watoto wa kike na wakiume unakoma, ikiwamo kuunda sera, sheria na kanuni, ambazo mbali na kudhibiti zinatoa adhabu kali kwa wanaopatikana na hatia.

Mapema, Mkurugenzi wa Idara ya Wanawake na Watoto, Nasima Haji Chum, aliwataka wasichana kujiepusha na mambo yaliyowazidi umri na kwamba jukumu lao kubwa ni kuzingatia masomo.

Alisema elimu ni silaha muhimu itakayowafikisha kwenye malengo yao ya kuwa viongozi, madaktari, walimu, mainjinia, wanamichezo mahiri na mengine yenye manufaa.

Kwa upande wake, Mratibu wa programu ya uhifadhi na ulinzi wa mtoto kutoka Shirika la 'Save the Children' Khadija Juma, aliishukuru serikali kwa jitihada inazochukua kuhakikisha mtoto wa kike yuko salama.

Hata hivyo, akizungumzia hali halisi ya watoto hasa wa kike duniani, alisema inasikitisha kuwa miaka 25 sasa tangu azimio la Beijing la kumaliza vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya watoto maazimio yake na mengine mengi bado hayajafikiwa kikamilifu.

## Saccos yatangaza kuwekeza Dodoma

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Hazina Saccos, kitatumia Sh. bilioni 52 kujenga kitega uchumi cha kisasa katika Jiji la Dodoma kwa lengo la kujiongezea mapato na kuwahudumia wateja na wengi zaidi pamoja na kuwanufaisha wanachama wake.

Akizungumzia kuhusu mradi huo wakati wa mkutano mkuu wa chama hicho, Mwenyekiti wa Hazina, Aliko Mwaiteleke, alisema mradi huo utaongeza kipato kwa chama hicho na kukiwezesha kuhudumia wateja wengi zaidi, sambamba na kukuza uchumi wa wanachama na wa Dodoma kupitia makusanyo ya kodi.

Alisema mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 52 utajengwa katika eneo la ukubwa wa hekari 22 wanatarajia kujenga hoteli ya kisasa, kumbi za kufanyia mikutano, maduka makubwa na majengo ya ofisi ambazo zitatumika kama kitega uchumi kwa chama hicho chenye wanachama 5,600 nchi nzima.

Mwaiteleke alisema mpaka sasa upembuzi yakinifu wa mradi huo utakaojengwa kwa njia ya ubia kati ya Hazina Saccos na mwekezaji kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 22 kupitia utaratibu wa jenga, endesha na hamisha (Build, Operate and Transfer - BOT) ambapo mwekezaji atagharamia ujenzi wote na kuendesha kwa muda ambao utakubaliwa ndani ya mkataba.

Alisema Hazina imeamua kujenga Dodoma kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli za kuhamia mkoani humo na kuwaomba wafanyakazi pia kuunga juhudi hizo kwa kuchukua mikopo ya viwanja inayotolewa na chama hicho mkoani Dodoma.

Alisema mradi huo unasimamiwa na kamati ya watu saba wakiongozwa na Profesa Esta Eshengoma kutoka Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na wajumbe wake kutoka Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru), Bodi ya Manunuzi ya Umma (PSPTB), Kituo cha Uwekezaji (TIC), na Chuo Kikuu cha Ardhi ambao kwa sasa wanafanya kazi ya kusaka mwekezaji ili kufanikisha mradi huo.

Akifungua Mkutano Mkuu huo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Mary Maganga, aliipongeza Hazina Saccos kwa kuwapatia viwanja wanachama wake na kuwataka waviendeleze haraka ili kuondokana na changamoto ya kukosa makazi.

# Ushirika waagizwa kununua mbolea

**Na Mathias Canal, KATAVI**

SERIKALI imeviagiza vyama vya ushirika vya msingi (AMCOs) na vyama vikuu (FCU) kushiriki kwenye ununuzi wa mbolea wa pamoja (bulk procurement system BPS), ili kuwe na upatikanaji wa pembejeo hiyo kwa bei nafuu na kwa wakati.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitoa agizo hilo wakati akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani ambayo kitaifa ilifanyika Jumapili Oktoba 13, 2019 katika viwanja vya Shule ya Msingi Kashaulili Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi.

Alisema ili kuongeza matumizi ya mbolea nchini, Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA), imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha inapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu ikiwamo mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja BPS.

Aidha, imeendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo kutoa elimu kwa njia tofauti kwa lengo la kuongeza uelewa wa umuhimu na kuongeza matumizi ya mbolea nchini, hivyo ili tija na uzalishaji viongezeke vyama vya ushirika havina budi kushiriki kwenye ununuzi wa mbolea na kuwarahisishia wanachama wao ambao ni wakulima upatikanaji mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu.

Hasunga alitoa wito kwa wafanyabiashara wa mbolea kuiuza kwa bei elekezi iliyopangwa na serikali na wazingatie bei hizo kwa mbolea za kupandia (DAP) na kukuzia (UREA) ambazo zinaingizwa nchini kwa mfumo wa kwa pamoja BPS.

"Kama mnavyofahamu, serikali imeendelea kuratibu utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kupitia Benki za Maendeleo ya Kilimo (TADB), Uwekezaji TIB na Mfuko wa Pembejeo wa Taifa. Hivyo, nitoe wito kwa wakulima wote wa mkoa wa Katavi na mikoa mingine kujiunga katika ushirika ili kuweze kutumia fursa zinazotolewa na taasisi hizi ili kujiletea maendeleo," alisema Hasunga.

Waziri Hasunga alisema ili kuwa na matumizi sahihi ya mbolea, ufahamu juu afya ya udongo ni muhimu, hivyo, aliiagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kutoa taarifa ya afya ya udongo kwa wakulima na wadau wengine ili matumizi ya mbolea yaendane na mahitaji ya zao na udongo husika.

"Niwakumbushe wafanyabiashara wakubwa kuwa mbolea zinahitajika zaidi mikoani hivyo ni wakati mwafaka wa kuanza kusambaza mbolea haraka iwezekanavyo. Pia ni wakati sahihi wa kufungua matawi ya mauzo na maghala mikoani badala ya mbolea nyingi kurundikana ndani ya maghala ya Dar es Salaam, mahitaji yake ni madogo."

Alilitaka Shirika la Reli (TRC) kutoa kipaumbele katika usafirishaji wa mbolea kwa mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi, huku akiitaka Mamlaka ya udhibiti wa mbolea TFRA kuhakikisha inasimamia ubora wa mbolea kuanzia bandarini inapoingia hadi kwa muuzaji anayemuuzia mkulima.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene (katikati), akipata maelezo kwa Mwenyekiti wa Kiwanda cha plastiki cha Ok, Sami Ghaddar (kulia), alipotembelea kiwanda hicho, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnat Chaggu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kulinda taka hatari, chuma chakavu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kuendelea kusimamia matumizi ya chuma chakavu na taka hatarishi kwa sababu ni malighafi muhimu za viwandani.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, alisema hayo alipotembelea kiwanda cha OK Plastic cha Dar es Salaam.

Alieleza kuwa kiwanda hicho kinatumia chuma chakavu na taka hatarishi kama malighafi ya kutengeneza nyaya za shaba na kinatumia betri za magari chakavu kutengeneza mikeke ya kisasa.

Akizungumza na wafanyakazi na viongozi wa kiwanda hicho, Waziri Simbachawene aliwaahidi kuwa serikali itaendelea kusimamia marufuku ya usafirishaji wa chuma chakavu na taka hatarishi ili vitumiwe na viwanda vya ndani kutengeneza bidhaa kwa soko la ndani na nje.

"Nawashukuru ninyi OK Plastic, kwa sababu mmeonyesha kwa nini serikali ilifanya maamuzi ya kuzuia usafirishaji wa chuma chakavu na taka hatarishi nje ya nchi. Viwanda vya ndani ni muhimu sana katika kutoa nafasi za ajira, lakini tutasafirisha bidhaa hizo nje kama ambavyo OK Plast mnafanya. Hali hiyo itatuingizia pesa za kigeni na kuongeza thamani ya pesa yetu hapa nchini," ameieleza hafla hiyo."

Alisema kuwa ushahidi mwingine wa thamani ya marufuku hiyo ni kwamba chuma chakavu na taka hatarishi vinavyopatikana nchini bado vinahitajika mno kwani hivyo vinavyopatikana havitoshelezi mahitaji ya viwanda vya ndani.

"Duniani kote sasa wanatumia malighafi hizi za vyuma chakavu na taka hatarishi katika kujipatia malighafi za viwanda vyao. Hivyo nasi hatuna budi kurejeleza vyuma hivyo ili vitumike kama malighafi katika viwanda vya ndani," aliwaeleza wafanyakazi na kuongeza kuwa serikali iko makini na jambo hilo kwa sababu uwekezaji wa ndani unachangia ukuaji wa pato la taifa," alisema Simbachawene.

Akijibu ombi la kiwanda hicho, lililotolewa na Anacleto Pereira, kwamba serikali itafute njia nzuri ili kiwanda chao kipate shaba kutoka kwa wachimbaji wadogo wa shaba nchini, aliwashauri kuweka mipango yao vizuri ili wanunue shaba kutoka kwa wachimbaji hao wa ndani.

Pereira aliishukuru serikali kwa kuweka marufuku hiyo na kueleza kwamba hapo nyuma kiwanda chao na vingine vilikuwa vinakabiliwa na uhaba wa malighafi hiyo wakati chuma chakavu na taka hatari vinapelekwa nje kuneemesha watu wengine.

# Wakenya wapokea miili waliofariki ajali ya ndege

**NAIROBI,** Kenya

WAKENYA jana walikusanyika kupokea mabaki ya miili ya wapendwa wao waliokufa katika ajali ya ndege ya Ethiopian Airlines.

Familia za marehemu wa ajali ya ndege ya Ethiopian Airlines iliyoanguka mjini Addis Ababa Machi na kuwaua watu wote 157 waliokuwamo ndani ya ndege hiyo wamekusanyika mjini Nairobi kwa ajili ya kupokea miili ya jamaa zao.

Katika ajali hiyo, Wakenya 32 walifariki katika ajali hiyo. Redio ya kibinafsi nchini Kenya ilituma ujumbe katika mtandao wa kijamii wa Twitter ulionyesha picha za marehemu wa ajali hiyo, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jommo Kenyatta mjini Nairobi.

Ndege hiyo chapa ET302 kutoka katika Mji Mkuu wa Ethiopian Addis Ababa kuelekea Nairobi nchini Kenya iliangua muda mfupi baada ya kuondoka. Vipimo vya vinasaba (DNA) kuoanisha masalia ya watu 157 waliouawa katika ajali hiyo vilifanyika miezi kadhaa iliyopita baada ya ajali.

**Ndege ya Boeing 737 Max-8 ilianguka miezi sita tu baada ya ndege nyingine ya aina hiyo kuanguka na kuwaua watu 190 waliokuwamo.**

Watu kutoka nchi 30 walikuwa wamepanda ndege hiyo, huku wengi wao wakiwa ni raia wa Kenya.

Ilikuwa ni siku za huzuni kwa familia za Wakenya 32 waliofariki ambapo walipata fursa kwa mara ya kwanza kutazama masalia ya miili ya wapendwa wao.

Mazishi ya faragha yalifanyika lakini haikuwekwa wazi ikiwa masalia hayo yalitolewa kwa familia zao. Maofisa nchini Ethiopia walieleza kuwa miili mingine ambayo bado haijafahamika itazikwa katika kaburi la kumbukumbu litakalowekwa katika eneo la tukio la ajali hiyo.

Ndege ya Boeing 737 Max-8 ilianguka miezi sita tu baada ya ndege nyingine ya aina hiyo kuanguka na kuwaua watu 190 waliokuwamo.

Awali, ndugu na jamaa wa wahanga wa ajali hiyo walilalamikia Shirika la Boeing kwa kuchelewa kutoa matokeo ya vinasaba ambayo yangesaidia kutambua miili ya wapendwa wao.

Iliripotiwa kuwa miili ya marehemu wa ajali hiyo ilikuwa imeteketea kiasi cha kutotambulika kwa urahisi.

**Wakati huo huo**, ndugu wa watu waliofariki katika ajali ya ndege aina ya Boeing 737 Max iliyopata ajali nchini Indonesia mwaka jana wamekuwa wakidanganywa ili wasipatiwe fidia.

Mawakili wao waliliambia Shirika la Utangazaji la BBC kuwa familia nyingi zilishawishiwa kusaini fomu zinazowazuwia kuchukua hatua za kisheria.

Kipindi cha BBC cha Panorama kiligundua kuwa watu wengine ambao ni waathiriwa walisaini makubaliano sawa na hayo baada ya ajali nyingine mbili, zilizowazuwia kuishtaki kampuni ya Boeing katika mahakama za Marekani. Lakini, Boeing haikutoa kauli yoyote juu ya makubaliano hayo.

Abiria wote 189 na wahudumu wa ndege walifariki wakati ndege ya Boeing 737 Max ilipoanguka baharini dakika 13 tu baada ya kuondoka kutoka katika Mji Mkuu wa Indonesia Jakarta Oktoba 29, 2018. **BBC**



Wapiganaji wa jamii ya Wakurdi nchini Syria wakiwa wamejiandaa kukabiliana na vikosi vya majeshi ya Uturuki. **PICHA: ALLIANCE**

# Mtoto mchanga azikwa akiwa hai

**NEWDELH,** India

MTOTO mchanga wa kike amepatikana akiwa amezikwa hai katika kaburi la kina kifupi kaskazini mwa India.

Mkuu wa Polisi India, Abhinandan Singh ndiye aliyefichua kisa hicho.

Singh aliwaambia waandishi wa habari kuwa mtoto huyo alipatikana na mwanakijiji aliyekuwa ameenda kumzika mtoto wake aliyefariki baada ya kuzaliwa.

Mtoto huyo (pichani) aliyekuwa amewekwa ndani ya chungu na kuzikwa katika shimo la futi tatu, amekimbizwa hospitali ambako anaendelea na matibabu. Alisema Jeshi la Polisi limeanzisha uchunguzi kuhusiana na kisa hicho.

"Tunajaribu kutafuta wazazi wa mtoto huyo kwani tunashuku huenda hatua hiyo ilifikiwa kutokana na idhini yao," alisema Singh wakati akizungumza na waandishi wa habari katika jimbo la Uttar Pradesh.



Kwa mujibu wa Singh, mwanakijiji mmoja alimpata mtoto huyo alipokuwa akifukua kaburi la kumzika mwanawe aliyefariki baada ya kuzaliwa.

"Walipokuwa wanaendelea na shughuli ya uchimbaji kaburi kijiko cha kutoa mchanga katika shimo liligonga chungu kilichokuwa kimezikwa fiti tatu. walipokitoa walikuta ndani kuna mtoto," alisema Singh na kuongeza:

"Polisi walimpeleka mtoto huyo katika hospitali iliyo karibu ambako anaendelea kupokea matibabu."

Suala la kijinsia nchini India linatajwa kuwa katika hali mbaya zaidi duniani.

Wanawake mara nyingi hubaguliwa katika jamii huku watoto wa kike wakichukuliwa kama mzigo wa kiuchumi, hasa katika jamii masikini.

Wanaharakati wa kutetea usawa wa kijinsia wanasema watoto wa kiume wanapendelewa zaidi kuliko wa kike. **BBC**

## Japan, Korea Kusini zapania kumaliza mivutano

**TOKYO,** Japani

WAZIRI Mkuu wa Korea Kusini, Lee Nak-Yon, ataitembelea Japan wiki ijayo ikiwa ni mara ya kwanza tangu Japan ilipoiwekea vizuizi vya biashara nchi hiyo na kupalilia mizozo ya kibiashara, kidiplomasia kati ya nchi hizi mbili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Nak-yon atatembelea Japan kuanzia Oktoba 22 hadi 24, atahudhuria sherehe za kuvikwa taji kwa mfalme Naruhito.

Pia anatarajiwa kushiriki katika hafla itakayoandaliwa na Waziri Mkuu, Shinzo Abe na baadaye kufanya naye mazungumzo.

Mazungumzo yatakayokuwa ya ngazi ya juu kabisa kuwahi kufanyika tangu mvutano ulipozuka mwaka jana kuhusu madai kwamba Japan iliwalazimisha wananchi wa Korea ya Kusini wafanye kazi za sulubu wakati wa vita vikuu vya pili vya dunia.

"Tunataraji ziara hii itasaidia, kwa kuwa pande hizi mbili zinatambua umuhimu wa kuendeleza mazungumzo ili kuimarisha uhusiano," alisema ofisa mmoja wa serikali ambaye hakutaka jina lake lijulikane.

Uhusiano kati ya majirani hao wawili uliingia dosari tangu uliporejeshwa kuwa wa kawaida mwaka 1965 baada ya korti kuu ya Korea ya Kusini kuamuru mwaka jana kampuni mbili ya Japan yawalipe fidia wafanyakazi wa enzi za vita.

Japan imeeleza kuwa mzozo huo umeshatatuliwa kwa kutiwa saini mkataba wa mwaka 1965 uliourejesha katika hali ya kawaida uhusiano kati ya nchi hizo mbili.

Mvutano huo ulichukua sura nyingine na kuathiri pia masuala ya biashara na usalama, huku Japan ikiweka vizuizi vya biashara yake kuelekea Korea Kusini huku Korea ya Kusini nayo ikisitisha mkataba wa ushirikiano kati ya idara za upelelezi za nchi hizo mbili.

Waziri Mkuu Abe na kiongozi mwenzake wa Korea Kusini, Lee Nak-yon, mwandishi wa habari wa zamani aliyewahi kuwa ripota nchini Japan, wameanzisha uhusiano madhubuti tangu walipoanza kujishughulisha na siasa.

Wawili hao wamekutana kwa mara ya mwisho katika kongamano la kimataifa nchini Urusi Septemba mwaka 2018. **DW**



Shinzo Abe



Lee Nak-Yon

# CUF yaipa neno serikali uchaguzi mitaa

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimedai kumepokea taarifa za matukio yanayokiuka kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa kutoka maeneo mbalimbali, huku kikieleza sababu za watu kusuasua kujiandikisha.

Madai hayo yalitolewa jana na Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa chama hicho, Mneke Jaffar, alipozungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam.

Alisema wakati kanuni za uchaguzi kama zilivyotangazwa kupitia matangazo ya Serikali nambari 371, 372, 373 na 374 zinaagiza zoezi la kujiandikisha lifanyike kwenye vituo vilivyo katika maeneo ya umma, kuna wasimamizi wa vituo vya uandikishaji waliofunga vituo na kupita majumbani na kuandikisha kwa ubaguzi.

"CUF kimefanya utafiti kwa dodoso maalum tangu kuanza uandikishaji katika mikoa minane na kubaini sababu kadhaa kukwamisha mwitikio wa wananchi kujitokeza kujiandikisha na hatimaye kupiga kura," alisema Mneke.

Alisema wanataka serikali ipokee sababu hizo na kufanya utafiti wa kina zaidi na hatimaye kuchukua hatua mwafaka, badala ya kudhani kuongeza siku tatu kwa kuwa ndiyo tiba ya tatizo hilo.

Alidai kuwa sababu ya kwanza wananchi hawajahamasishwa vya kutosha kama ilivyokuwa ikifanyika huko nyuma.

"Mwaka 2004, 2009 na 2014 wananchi walikuwa wakisukumwa kupitia mikutano ya hadhara na harakati za kisiasa, ambapo vyama vya siasa na asasi za kiraia vilibeba jukumu la kuwahamasisha wananchi kujiandikisha na kuwaeleza umuhimu wa kufanya hivyo," alisema na kuongeza:

"Kwa muda mrefu sasa ni CCM pekee inayofanya mikutano ya hadhara na harakati za kisiasa bila kubughudhiwa, huku wakilindwa na Jeshi la Polisi. kutohamasika kwa wananchi ni miongoni mwa sababu kuu zinazokwamisha uandikishaji."

Mneke alisema sababu ya pili wananchi wamekata tamaa ya kushuhudia uchaguzi huru na wa haki unaopelekea anayepata kura nyingi kutangazwa mshindi. Baadhi wametoa mifano ya uchaguzi mdogo uliofanyika tangu 2016 na kudhihirisha kutoridhishwa na ukiukwaji taratibu.

Sababu ya tatu alisema wananchi wengi wameonyesha wasiwasi wao kuhusu utayari wa Serikali ya CCM kushuhudia kampeni na uchaguzi vikifanyika.

Kwa mujibu wa Mneke, sababu ya nne wananchi wanaamini kwamba uchaguzi unakuwa na walakini kwa mfano wa 2017 na 2019 viongozi (Wabunge na Madiwani) waliopatikana kwa tabu wahamie CCM na kugombea tena nafasi hizo hizo na kutangazwa washindi na wengine kupitishwa bila kupingwa kwa nguvu za dola.

Kutokana na hali hiyo, CUF imependekeza serikali itamke kwamba vyama vya siasa viko huru kisheria kufanya mikutano ya hadhara kuhamasisha wananchi kujiandikisha na kuzungumzia masuala yanayohusu nchi yao kama Katiba ya nchi inavyotaka.

"Ni muhimu serikali ikatoa tamko hilo mapema, ili hawa waandishi katika vituo vya kura wasitumie kodi zetu kwa kusinzia tu vituoni kutokana na kukosa wa kuwaandikisha," alisema.

Pia CUF imeitaka serikali iwaondolee hofu Watanzania kwa kuwaambia kwamba sasa imedhamiria kuona uchaguzi ukifanyika na kwamba itasimamia kuhakikisha unakuwa huru na haki.

Kadhalika, kimeitaka serikali kupitia Tamisemi izuie vitendo vya waandishi wa wapigakura kuhama vituoni na kwenda majumbani kuandikisha watu holela.

"Tunalitaka Jeshi la Polisi kwa mara nyingine kuwa 'neutral' (kutoegemea) katika mchakato mzima wa uchaguzi kuanzia hatua ya kujiandikisha mpaka kutangazwa washindi," alisema.



Meneja wa Usimamizi Mfumo wa Uzalishaji kutumia Stampu za kodi za kielektroniki (ETS) wa kampuni ya TBL kiwanda cha Mbeya, Ibrahim Marwa (kushoto), akitoa maelezo kwa Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede (katikati) na ujumbe wake walipofanya ziara ya kikazi kiwandani hapo, kukagua matumizi ya mfumo huo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka uchaguzi usiwagawe wananchi

**Na Futuna Suleiman,** RUFIJU

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amewataka wananchi kumuenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nterere, kwa kuishi kwa amani na upendo bila kubaguana kwa misingi ya ukabila wala udini.

=Aliyasema hayo wilayani Rufijii alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Muhoro Ikwiriri na viunga vyake katika zoezi la uhamasishaji wananchi katika daftari la wapigakura.

=Alitoa angalizo hilo baada ya kujitokeza changamoto ya ubaguzi katika zoezi hilo katika baadhi ya wilaya zilizopo mkoani humo, ambapo baadhi ya wananchi wamekuwa wakiwakataa wafugaji wasiandikishwe kwa madai kuwa ni wageni wahamiaji hawastahili kujiandikisha licha ya kuwapo kwenye maeneo hayo kwa muda mrefu.

="Mwalimu Nyerere alikataa ubaguzi na leo (jana) ametimiza miaka 20 tangu kifo chake, tukianza ubaguzi hatutabaki salama ...mkitaka hawa waondoke wale waondoje hatutafika, Mwalimu Nyerere alituonya tumuenzi kwa vitendo kubwa ni kufuata sheria ukiizingatia sheria hakuna tatizo," alisema Ndilikilo..

=Kadhalika, aliwataka kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwa siku zilizobaki na kuwachagua viongozi ambao watamsaidia Rais John Magufuli kufanya kazi kwa kuwajali wananchi wanyonge.

="Mpeni Rais heshma yake, chagueni viongozi wanaokwenda kwa spidi, mwenye huruma na watu wanyonge," alisema Mhandisi Ndikilo na kusisitiza kuwa:

="Msiwachague viongozi waliojivisha ngozi ya kondooo ndani mbwa mwitu, wakishapata wanatoa ngozi ya kondoo na kubaki na ya mbwambwitu ama fisi... kazi yenu iwe ni kuchuna ngozi zao kuangalia ngozi yaliyopo ndani, msikubali kuuziwa mbuzi kwenye gunia."

=Kwa mujibu wa Ndikilo, Halmashauri ya Mji Kibaha imeshika mkia katika uandikishaji, huku Kibiti ikiwa kinara ikifuatiwa na Wilaya ya Rufiji.=

# Prof. Mkumbo ataka kasi miradi ya maji

**Na Mohamed Saif**

MKANDARASI Kampuni ya Patty Interplan anayetekeleza mradi wa maji wa dharura wa Rwelu wa Mjini Mtwara, ametakiwa kuukamilisha mapema ili kuwaondolea adha wananchi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, alitoa agizo hilo juzi mkoani Mtwara wakati wa ziara yake ya kukagua hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa maeneo mbalimbali mkoani humo.

Baada ya ziara yake kwenye mradi huo, Prof. Mkumbo alisema ameridhishwa na hatua aliyoishuhudia ya ujenzi wake, lakini pia alimtaka mkandarasi kuhakikisha anaukamilisha mapema iwezekanavyo ili kuongeza kiasi cha maji yanayozalishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Mtwara (MTUWASA) kwa matumizi ya wakazi wa Mji wa Mtwara.

"Mkandarasi sio lazima usubiri hadi muda wa mkataba umalizike ndio ukabidhi mradi, kwa hatua hii niliyoiona unaweza na ni vizuri ukaukamilisha kabla ya muda," aliagiza Prof. Mkumbo.

Alisisitiza kuwa mkandarasi anapaswa kuweka kipaumbele kwenye kazi zinazopelekea wananchi kupata maji kwanza kisha ndipo kazi zingine ziendelee hasa ikizingatiwa kwamba wananchi hawataki kujua juu ya ujenzi wa miundombinu inayoendelea, wanachotaka ni kupata maji.

"Anzeni na maeneo yatakayoleta maji haraka masuala mengine yatafanyika kwa baadaye wakati tayari wananchi wanapata huduma ya maji," alisisitiza Prof. Mkumbo.

Prof. Mkumbo aliiagiza MTUWASA kuhakikisha inasimamia vyema miradi yake ili kuleta ufanisi na tija katika kuondoa adha ya upungufu wa maji kwenye maeneo inayosimamia.

# Uandikishaji Bariadi mwendo mdogo

**Na Happy Severine,** BARIADI

MBALI na serikali kuongeza siku tatu za kujiandikisha katika daftari la mpigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, zoezi hilo limeendelea kusuasua katika vituo vya uandikishaji vwilayani Bariadi mkoani Simiyu.

Hali hiyo inadhihirishwa na baadhi ya vituo vya Izunya, Somanda na Nyaumata na Kisiwani kuwa na wananchi wachache ikilinganishwa na idadi halisi ya wakazi wa maeneo hayo.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana waliotembelea vituo hivyo, mwandikishaji wa kituo cha Izuya, John Magolonga, alisema kwa siku saba zilizotolewa kwa wananchi kujiandikisha katika daftari la mpigakura, mwitikio umeonekana kuwa mdogo ukilinganisha na idadi ya wakazi wa maeneo wanayoishi.

"Siku saba zilizokuwa zimetolewa na serikali zimeonekana kuwa na mwitikio mdogo wa wananchi kujiandikisha ... ila matumaini yangu kuwa idadi hiyo itaongezeka kutokana na kuongezwa kwa siku tatu mbele," alisema.

Magolonga alisema kuwa katika kituo chake cha mtaa wa Izuya mpaka sasa ameandikisha jumla ya wananchi 373, huku akibaini idadi hiyo inaweza kuongezeka kutokana na kuongezwa kwa siku tatu.

Nyanja Mutani, mwandikishaji wa kituo cha uandikishaji mtaa wa Kisiwani, alieleza kuwa mwitikio wa wananchi bado haujawa mzuri, ingawa ana matumaini makubwa kuwa kwa siku zilizoongezwa, idadi itakuwa kubwa kwani wananchi wengi huwa wanajitokeza siku za mwisho.

Awali akizungumza na wanahabari Kaimu Katibu idara ya Uhamasishaji na Chipukizi wa Jumuiya ya Vijana wa CCM (UVCCM) Taifa, Leonard Singo, aliwataka wananchi wa Mkoa wa Simiyu kuwapuuzia wale wote wanaopotosha na kutaka kuharibu zoezi zima la uandikishaji kwani hawana nia njema na maendeleo ya nchi.

Singo alisema ni vema wananchi wote wakajitokeza kujiandikisha katika daftari hilo ili waweze kushiriki na kupiga kura kwa kuwachagua viongozi bora, wanaofaa na wapenda maendeleo ya nchi.

"Niwaombe sana wananchi wajitokeze kujiandikisha na waachane na upotoshwaji unaoendelea kufanywa chinichini na wasiopenda maendeleo ya nchi na endapo mtajiandikisha mtakuwa na uhuru wa kuwachagua viongozi mnaowataka ambao watasaidia kukuza amani ya nchi," alisema.



Gari lenye namba C 5413 A likiwa limekatika tela kutokana na kuwa chakavu katika eneo la Kwa Msunguri Mbezi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wakunwa mafunzo ya majanga

**Na Ndalike Sonda,** BAGAMOYO

WAANDISHI wa habari kutoka redio jamii 25 nchini walioshiriki mafunzo ya siku tano ya kuwajenga uwezo wa kuandika na kuandaa vipindi bora vinavyohusu maafa na majanga, wamesema mafunzo hayo yamewaimarisha katika kuandaa habari za maafa na majanga kwenye maeneo yao.

Wakizungumza kwa niaba ya wenzao mjini Bagamoyo mkoani Pwani, baadhi ya waandishi wa habari Saumu Ali Haji, Michael Mgozi na Amina Semagogwa wamesema kutokana na maafunzo hayo, elimu ya maafa na majanga wataitoa kupitia redio wanazofanyia kazi.

Walisema awali hawakuwa na uelewa wa kutosha namna ya kuripoti habari za maafa na majanga mbalimbali yanapotokea katika jamii, jambo ambalo liliwafanya wanahabari waandike habari ambazo hazina ujazo na uwiano wa kimamlaka.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, mratibu wa Asasi ya mtandao wa Radio Jamii Tanzania, (TADIO), Irene Makene, aliwapongeza washiriki na kuwataka kwenda kuyafanya kwa vitendo yale waliyofundishwa na wawezeshaji.

Mratibu wa mafunzo kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Getrude John, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kwenda kushirikiana na wafanyakazi wenzao katika kuleta mabadiliko katika jamii na kuwa wabunifu katika kutafuta habari zenye kuisaidia jamii.

UNESCO imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari 25 kutoka radio kijamii nchini juu ya kuandika na kuandaa vipindi vya kukabiliana na maafa na majanga. Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku tano mjini Bagamoyo, mkoani Pwani.

## Wafanyabiashara watembelea makumbusho kumuenzi Nyerere

**Na Beatrice Philemon**

ZAIDI ya wafanyabiashara 300 kutoka Shirika la Elimu ya Amani na mtandao wa wajasiliamali unaojulikana kama Kimbilio Letu in Pair International Network, wametembelea Makumbusho ya Taifa ili kumuenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Lengo la ziara hiyo lilikuwa kufahamu jinsi Mwalimu Nyerere alivyoanza kutafuta amani ya Tanzania, kitu ambacho kinavutia watu wengi ulimwenguni kuja kutembelea Tanzania.

Akizungumza na Nipashe baada ya kutembelea sehemu mbalimbali katika jengo la makumbusho ya Taifa, Makamu Mwenyekiti kutoka shirika la Elimu ya Amani, Dora Temba, alisema wameamua kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa kutembelea makumbusho hiyo ili kujua historia ya yake, jitihada alizozifanya katika kuleta uhuru wa Tanzania na ukombozi katika nchi nyingine za Afrika.

Pia kuvutia Watanzania kutembelea maeneo ya historia ili kuendeleza utalii wa ndani.

"Sisi kama wafanyabiashara na wanachama kutoka shirika la Kimbilio Letu in Pair International Network na Shirika la Elimu ya Amani tumekuja hapa kujifunza na pia tunataka watu wajue amani ni nini ili waendeleze amani iliyoanzishwa na waasisi wetu," alisema.

"Mbali na hilo, kila siku rais wetu (John Magufuli) anasisitiza amani katika nchi yetu kwa sababu viwanda haviwezi kuwapo kama hakuna amani," alisema.

"Kwanza anathamini watu masikini tena wale wenye kipato cha chini na sisi kama wanachama tunasapoti jitihada zake kwa kuelimisha masuala ya amani katika maeneo mbalimbali ikiwamo shuleni na matamasha mbalimbali nchini," alisema.

Anasema bila amani hakuna maendeleo, bila amani hakuna mtalii anayeweza kuja kutembelea

Naye Meneja Sera na Mipango taasisi hiyo, Charles Sabinian, alisema kuwa wameamua kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa kutembelea makumbusho ya Taifa ili wajue vizuri historia ya Mwalimu Nyerere na Tanzania na jinsi alivyoweza kuleta uhuru wa Tanzania na ukombozi katika nchi zingine.

# MESSI AMZUNGUMZIA NEYMAR, AMTAJA GUARDIOLA




**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amekiri kuwa alijua Neymar wa PSG atajiunga na Real Madrid wakati wa dirisha la usajili lililopita baada ya kuona Barcelona wameshindwa kumsajili, huku pia akimtaja kocha wa Manchester City, Pep Guardiola kuwa ndiye aliyemkuza.

Messi amesema hayo alipokuwa akihojiwa katika Kituo cha Televisheni cha RACI, ambapo alisema Neymar alionyesha nia ya kuondoka jijini Paris na alijua Rais wa Madrid, Florentino Perez na uongozi wa timu hiyo watamfuata kumsajili.

"Nilijua Neymar anakwenda Real Madrid, kwani Barcelona ilishindwa kumsajili," alisema Messi katika mahojiano hayo.

Akimzungumzia Guardiola, Messi alisema uwezo wa kocha huyo ndio ambao ulisaidia kukuza kiwango chake.

"Nimepata bahati ya kukutana na matukio mengi makubwa mazuri, bado kipindi cha Guardiola nilikuwa mmoja wa wachezaji bora.

"Kila mwaka nimekuwa nikipambana kuongeza ubora, nafikiri ni wakati wa (Pep) Guardiola, ndipo nilipokua sana kisoka wakati huo,"alisema Messi.

Pia mchezaji huyo hakusita kubainisha nyakati mbaya kuwahi kukutana nazo kwenye maisha yake ya mpira, bao lake bora, mechi bora na timu bora pamoja na safu ngumu ya ulinzi kuwahi kukutana nayo.

# Mandzukic tayari kutua Old Trafford

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imetajwa kwamba imefikia mahala pazuri kwa ajili ya kumsajili nyota wa Juventus, Mario Mandzukic, kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail.

Nyota huyo raia wa Croatia alikaribia kutua kwa 'Mashetani Wekundu' hao kipindi cha majira ya joto kilichopita, kabla ya usajili wake kushindikana dakika za mwisho.

Kwa mujibu wa taariifa hizo, Man United wapo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 10 kwa ajili ya kupata huduma ya kiungo huyo.

Mandzukic, mwenye umri wa miaka 33, amekuwa hana namba ya kudumu kwa sasa ndani ya kikosi cha Juventus na kocha Maurizio Sarri yupo tayari kumuachia mshindi huyo wa pili wa Kombe la Dunia akiwa na Croatia.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Man United watamsajili mchezaji huyo wakati wa dirisha dogo la usajili Januari mwakani.

Chanzo kimoja kimelidokeza Daily Mail kwamba, tayari Man United wamefikia makubaliano binafsi ya kumsajili mchezaji huyo.






# Uwanja wa Sporting kupewa jina la CR7

**LISBON,** Ureno

RAIS wa klabu ya Sporting Lisbon ya nchini Ureno amethibitisha kuwa anataka kubadili jina la uwanja wake, Jose Alvalade wenye uwezo wa kubeba mashabiki 50,000 na kuupa jina la nyota wa klabu ya Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo.

Rais huyo amesema kwa heshima ya mchezaji huyo uwanja huo watauita kwa jina la "Cristiano Ronaldo Arena au CR7 Arena."

Ikumbukwe uwanja wa nyumbani wa Sporting ulipewa jina la mwanzilishi wa klabu hiyo, Jose Alvalade mwaka 1956, lakini ripoti zinaeleza wanafikiri kubadili jina hilo na kuupa jina la mchezaji waliyemlea katika Academy.

Ronaldo aliondoka klabuni hapo na kujiunga na Manchester United mwaka 2003 na sasa ni miaka 17 tangu atengeneze jina hapo Sporting.

Alianza kuichezea Sporting msimu wa 2002-2003, Ronaldo akawa mchezaji wao wa kwanza kucheza kwenye timu ya chini ya miaka 16, timu za chini ya miaka 17 na chini ya 18, timu ya B, na timu ya kwanza, yote ndani ya msimu mmoja.

"Ni nadharia ambayo hatutaiweka kando na ni wazi tumekuwa tunajivunia sana kuwa na jina lake kuhusishwa na sisi," alisema rais huyo.

Cristiano yuko na kila wakati atakuwa alama kubwa katika historia ya klabu yetu," Rais wa Sport Frederico Varandas aliiambia Tuttosport.

"Ni urithi wa Ronaldo unaochochea kizazi kijacho kwenye klabu hii. Tayari tunatunza maadili yake kwenye ukuta wa uwanja wa vijana.

"Cristiano hakika ni mchezaji bora wa Ureno wa wakati wote na mmoja wa wachezaji bora katika historia ya mchezo huu wa mpira wa miguu," aliongeza Varandas.

## HABARI MICHEZO

# Van der Sar kumpindua Woodward

**AMSTERDAM,** Uholanzi

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United, Edwin van der Sar amesema kwamba, anataka kurudi kwenye timu hiyo kuchukua nafasi ya Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa sasa, Ed Woodward.

Van der Sar mwenye umri wa miaka 48, aliyeitumikia kwa miaka sita kwenye timu hiyo, akishinda mataji manne ya Ligi Kuu England, kwa sasa ni mkurugenzi mtendaji huko kwenye kikosi cha Ajax.

Akizungumza na televisheni moja ya Uholanzi, Van der Sar alisema atakuwa tayari kurudi Man United, lakini kama tu atahakikishiwa nafasi kama hiyo anayoshikilia kwa sasa kwenye kikosi cha Ajax.

Woodward ndiye anayeshikilia nafasi ya kuwa mkurugenzi mtendaji mkuu kwenye kikosi cha Man United, lakini wakati huo huo akiwa makamu mwenyekiti mtendaji.

"Mimi ni mkurugenzi mtendaji mkuu, nafasi ambayo ni tofauti kabisa na mkurugenzi wa soka," alisema Van der Sar.

"Ukiweka kando mke wangu na wanangu, nina vitu vingine viwili ninavyovipenda kwenye maisha yangu. Navyo ni Ajax na Manchester United. Ajax waliniibua mimi, wakanipa nafasi na kuwa kipa wao namba moja.






# MOURINHO: RONALDO DE LIMA BORA ZAIDI YA MESSI, CR7

**LONDON,** England

JOSE Mourinho ameibuka kwenye mjadala wa mchezaji gani bora zaidi kati ya Mreno mwenzake Cristiano Ronaldo na Lionel Messi, huku yeye akiwatupa wote, kwa mujibu wa Daily Mail.

Mounriho kocha wa zamani wa Manchester United, Real Madrid, Inter Milan na FC Porto na Chelsea, amemtaja nyota wa zamani wa Brazil, Ronaldo kuwa mchezaji bora zaidi aliyewahi kumwona kwenye maisha yake.

Mourinho alisema: "Ronaldo, El Fenomeno, Cristiano Ronaldo na Leo Messi wamekuwa na maisha marefu kwenye soka, kwa sababu wamethubutu kulinda viwango vyao kuwa bora kila siku kwa zaidi ya miaka 15.

"Hata hivyo, ukitazama vipaji na akili ya mpira ndani ya uwanja, hakuna anayemzidi Ronaldo (Nazario). Nilipokuwa Barcelona na Bobby Robson, hapo ndipo nilipomwelewa Ronaldo kuwa ni mchezaji bora zaidi kuwahi kumwona ndani ya uwanja.

"Majeraha yalimuua mapema, lakini kile kiwango alichokionyesha kipindi kile akiwa na umri wa miaka 19, kilikuwa balaa."

# *AS Roma kutumia Kiswahili*

**ROME,** Italia

KLABU ya AS Roma ya Italia inayoshikiriki Ligi Kuu ya Serie A, imebainisha kwamba inataka kuanza kutumia lugha ya Kiswahili kwenye kurasa zake rasmi za mitandao ya kijamii, kwa mujibu wa tovuti yake.

Klabu hiyo iliandika ujumbe wa Kiswahili kumpongeza mwanariadha kutoka Kenya, Eliud Kipchoge ambaye aliweka historia ya kuwa mtu wa kwanza katika historia ya mbio za nyika kwa kukimbia kilomita 42 kwa muda wa chini ya saa mbili.

AS Roma waliandika "INCREDIBBLE" na ndipo watu wengi hususan kutoka Kenya walianza kumlazimisha 'Admin' wa akaunti hiyo ya Twitter, Ku-tweet kwa lugha ya Kiswahili na wengine wakiomba klabu hiyo ifungue akaunti rasmi ya Kiswahili.


Baada ya maombi hayo, AS Roma walijibu kwa Kiswahili kwa kuandika "Admin amefurahi, asante wote, mnanifundisha swahili lala salama."

Baada ya hapo Rais wa Klabu hiyo, James Joseph Pallotta alisema kuwa maombi hayo yamepokelewa na muda si mrefu watafungua ukurasa wa Kiswahili.

"Kama mnahitaji ukurasa wa AS Roma wa Kiswahili kweli mnastahili kuwa nao. Unawajia muda si mrefu. Amani na upendo kwenu nyote," aliandika Pallotta kwa Kiswahili kwenye ukurasa wake wa Twitter.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LACAZETTE KUREJESHA UTATU WAO ARSENAL

## Sasa fiti kuivaa Sheffield United baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa huku...

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Alexandre Lacazette ameripotiwa kuwa tayari kurejea kujifua na kikosi cha kwanza wiki hii na anatarajiwa kuwa fiti kabisa wakati 'Gunners' itakapoivaa Sheffield United baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

**Lacazette amekuwa nje ya kikosi cha Arsenal kutokana na majeraha ya kifundo cha mguu tangu Gunners ilipocheza dhidi ya mahasimu zao wa Kaskazini mwa London, Tottenham Hotspur Septemba Mosi, mwaka huu.**

Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa alicheka na nyavu katika mechi hiyo, lakini baadaye ilielezwa kwamba alikuwa akicheza na maumivu katika kifundo chake cha mguu.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Lyon, amefumania nyavu mara mbili katika mechi tatu msimu huu na Arsenal haikupoteza mechi yoyote ya Ligi Kuu kwa kipindi chote akiwa chumba cha majeruhi, ikishinda michezo miwili na sare idadi kama hiyo.

Kwa upande mwingine, kukosekana kwa straika huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 28, kulitoa nafasi kwa Pierre-Emerick Aubameyang kuwika katika nafasi ya mshambuliaji wa kati kwenye kikosi hicho cha Unai Emery, ambapo ameweza kufumania nyavu mara tano kwa Septemba pekee. Na kutokana na mafanikio hayo, nyota huyo wa kimataifa wa Gabon, amechaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu England kwa mwezi huo.

Kwa mujibu wa Sky Sports, kuimarika kwa majeraha ya Lacazette kumeendelea kuwa chanya na straika huyo ameripotiwa kutupia jicho mechi ya Ligi Kuu kati ya Arsenal na Sheffield United kuwa ya kwanza kwake kuitumikia klabu yake wakati huu akirejea.

Mfaransa huyo anatarajiwa kuanza mazoezi kamili na wachezaji wenzake na anaweza kuwa miongoni mwa kikosi kitakachoshuka katika dimba la Bramall Lane kuivaa Sheffield United baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Kurudi kwa Lacazette ni furaha kwa mashabiki wa Arsenal, ambao watakuwa wakitumai kuona utatu wao wa safu ya ushambuliaji ukirejea, ambao utajumuisha usajili mpya Nicolas Pepe, katika wiki chache zijazo.

Arsenal kwa sasa inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, licha ya kukabiliwa na majeruhi wengi tangu kuanza kwa msimu mpya.

Gunners itawavaa Sheffield United Oktoba 21, mwaka huu katika ratiba ya mechi ya Ligi Kuu England ijayo.

## ZISIKUPITE

### SPURS KURUDIWA FERNANDES

TOTTENHAM Hotspur inajiandaa kurejea nia yake ya kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon, Mreno Bruno Fernandes, 25, wakati dirisha la usajili la Januari litakapofunguliwa. ***(A Bola - in Portuguese)***

### MANDZUKIC, UTD WAKUBALIANA

MANCHESTER United itapaswa kutumia pauni milioni 10 kama watataka kumsajili mshambuliaji Mcroatia Mario Mandzukic, 33, kutoka Juventus katika dirisha la usajili la Januari, lakini tayari mchezaji huyo ameshafikia makubaliano ya mdomo na 'Mashetani Wekundu' hao. ***(Express)***

### MBAPPE, KANE LULU BARCA

BARCELONA ingependa zaidi kuwanasa mshambuliaji wa Paris St-Germain, Mfaransa Kylian Mbappe, 20, na straika wa Tottenham na England, Harry Kane, 26, kuliko straika wa Liverpool na Brazil, Roberto Firmino, 28. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### JORGINHO AIMULIKA SERIE A

WAKALA wa Kiungo wa Chelsea, Jorginho, hajaweka kando uwezekano wa nyota huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 27 kurudi Serie A. ***(Radio Sportiva - in Italian)***

### GIROUD AMSHUKIA LAMPARD

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Olivier Giroud amekataa kumkosoa kocha wa kikosi hicho, Frank Lampard, lakini straika huyo mwenye umri wa miaka 33, amesema "hawezi kukubaliana" na nafasi finyu anayoipata ya kucheza hapo Stamford Bridge. ***(Le Pelerin, via Star)***

### RAKITIC ANUKIA MAN UNITED

BARCELONA inaweza kuwa tayari kumuuza kiungo Ivan Rakitic, 31, katika dirisha la Januari na Manchester United inaaminika imefungua meza ya mazungumzo na nyota huyo wa kimataifa wa Croatia. ***(Sport - in Spanish)***

### RAIS PSG KUUZIWA HISA LEEDS

MMILIKI wa Leeds United, Andrea Radrizzani anasema anafikiria kuuza hisa kwenye klabu kwa wazabuni watatu, ikiwa ni pamoja na kwa Qatari Sports Investment- ambayo inaendeshwa na Rais wa Paris St-Germain, Nasser al-Khelaifi. ***(Times)***

### ERIKSEN NJIAPANDA REAL

UWEZEKANO wa Real Madrid kutoa ofa kwa kiungo wa Spurs, Mdenmark Christian Eriksen, 27, kunaweza kutegemea ni kwa namna gani timu hiyo itakavyoonyesha kiwango na kama kutokuwa na majeruhi wa muda mrefu. ***(AS)***

### DECLAN RICE AIKANA UNITED

KIUNGO wa England, Declan Rice, 19, amesisitiza ni mwenye furaha hapo West Ham United, akifafanua kuhusu taarifa za kujiunga na Manchester United kama "zote ni tetesi tu hadi kitu fulani kitokee- na hakuna kitu". ***(Mirror)***

### BAYERN WAMLILIA MULLER

RAIS wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amesema "hawezi kufikiri" mshambuliaji Thomas Muller, 30, kuondoka klabuni hapo, licha ya Mjerumani huyo kutokuwa na furaha kwa kupunguziwa majukumu na mabingwa hao wa Bundesliga. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

## Namungo yatamba haijapotea Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kukabiliwa na majeruhi, uongozi wa Namungo FC ya Lindi, umesema timu yao imeanza vema msimu wake wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Namungo FC ambayo imecheza mechi tano, ina pointi saba na katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20, iko katika nafasi ya saba.

Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Kungu, aliliambia gazeti hili jana kuwa, wanaamini watafanya vizuri katika mechi zinazofuata baada ya wachezaji wake waliokuwa majeruhi kurejea kikosini.

Kungu aliwataja wachezaji hao wa kikosi cha kwanza ambao walikuwa majeruhi sasa afya zao zimeimarika kuwa ni pamoja na Bigirimana Blaise, Paul Ngalema na Reliants Lusajo.

"Tumecheza ugenini mechi mbili, sasa tunarudi nyumbani na habari njema ni kuwa wachezaji wetu tegemeo watatu wa kikosi cha kwanza waliokuwa majeruhi wamepona na wamerudi kikosini, tunasema burudani imerudi nyumbani," alisema Kungu.

Namungo inatarajiwa kuwakaribisha Lipuli FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa.

## Usaili Morogoro kufanyika J'mosi

**Na Mwandishi Wetu**

WAGOMBEA 17 waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), utakaofanyika Oktoba 27, mwaka huu, wanatarajiwa kufanyiwa usajili Jumamosi, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Uchaguzi, Roman Luoga, alisema usaili huo utafanyika kuanzia saa 3:00 asubuhi kwenye Hoteli ya Cherry na wagombea wote waliorejesha fomu wanatakiwa kufika na vyeti vyao halisi bila kukosa.

Luoga alisema leo ndio mwisho wa kupokea pingamizi na kuanzia kesho hadi Oktoba 18, mwaka huu, kamati yake itajadili pingamizi zilizowasilishwa na baada ya hapo wataelekea katika mchakato wa usaili.

"Oktoba 20 itakuwa ni siku ya kutangaza orodha ya mwisho ya wagombea na Oktoba 21 hadi 26, mwaka huu ni muda wa kufanya kampeni," Luoga alisema.

Aliwataja wagombea waliojitokeza kuwa ni pamoja na Paschal Kihanga na Mnzava Abrahamu wanaowania uenyekiti huku Aristotle Nikitas na Rajab Kiwanga wakichuana kwenye nafasi ya Makamu Mwenyekiti wakati Hamisi Semka akiwa ni mgombea pekee wa nafasi ya Katibu Mkuu.

Jimmy Lengwe, Stephen Mdachi na Emmanuel Kimbawala wanawania nafasi ya Katibu Msaidizi wakati Peter Mshigati anawania cheo cha Mweka Hazina, Hassan Bantu (Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TFF) na Ramadhan Myolele anawania nafasi ya Mjumbe Mwakilishi wa klabu.

# SABABU IAAF KUIKATAA REKODI YA KIPCHOGE

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Mkenya Eliud Kipchoge kuweka jina lake katika vitabu vya historia upande wa mbio za nyika, kufuatia kumaliza kilomita 42 za mbio za marathon kwa saa moja dakika 59 na sekunde 40 katika shindano la Ineos Jumamosi nchini Austria Vienna, Shirikisho la Riadha Duniani (IAAF), halitambui rekodi hiyo.

**Kwa mujibu wa sheria za IAAF, ili mbio zozote ziweze kutambulika ni lazima zifikie vigezo ama kanuni zake, jambo ambalo mbio hizo alizoshiriki Kipchoge hazikukidhi vigezo na masharti ya wenye dhamana hao na mashindano yote ya kufukuza upepo.**

**Vigezo hivyo ni;** Kwanza mbio hizo lazima ziwe zimeandaliwa na IAAF ama Shirikisho la Raidha la nchini ambapo riadha hizo zinaandaliwa.

**2.** Wanariadha wanaodhibiti kasi hawawezi kuingia katika mbio hizo kwa zamu na kutoka kama ilivyokuwa katika shindano hilo.

**3.** Lazima wanariadha wafanyiwe vipimo vya matumizi ya dawa za kusisimua mwili.

**4.** Vinywaji vinavyotumika kwa wanariadha vinapaswa kutoka kwa vituo rasmi na si kupewa mwanariadha na wasimamizi wake.

**5.** Ni sharti kuwapo zaidi ya washindani watatu katika mbio hizo.

**6.** Mwanariadha hafai kudhibitiwa kasi na gari lililopo mbele yake.

**7.** Njia itakayotumika ni sharti ifanyiwe ukaguzi na kupimwa na maofisa wa IAAF.

Wakati wa jaribio la kwanza la mbio hizo za marathoni huko Monza nchini Italia miaka miwili iliyopita, Kipchoge alipatiwa vinywaji huku wadhibiti mbio hizo wakibadilishwa mara kwa mara, hatua iliokiuka masharti ya IAAF.

Aidha, Jumamosi alipewa vinywaji kila baada ya kilomita tano na hivyo basi kukiuka sheria hizo za IAAF.

Mwanariadha huyo mwenye umri wa miaka 34, tayari anashikilia rekodi ya dunia kwa upande wa wanaume katika umbali huo akiwa na muda wa saa mbili dakika moja na sekunde 39, ambao aliweka katika mbio za Berlin Septemba 16, mwaka jana.

Kwa mujibu wa AFP, barabara hiyo ilikuwa imeandaliwa hali ya kwamba ingemchukua Kipchoge sekunde 4.5 zaidi kulingana na uchanganuzi wa wataalamu wa michezo katika Chuo Kikuu cha Vienna na kwamba kwa jumla aliweza kushuka mita 26 na kupanda mita 12.

Mbio hizo za marathon zimekuwa na ushindani mkali katika kipindi cha miaka 16 iliopita kati ya wanariadha wa Kenya na wenzao wa Ethiopia.




Mshindi wa Bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Richard Weston Ramsi akionyesha mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. 3,158,501/- baada ya kukabidhiwa kufuatia kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Dodoma City, Kagera kukiwakisha leo Dom

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Dodoma City FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza inatarajia kukikaribisha Kagera Sugar kutoka Bukoba katika mechi ya kirafiki itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Dodoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema tayari kikosi chake kilishafika Dodoma tangu juzi jioni na lengo la mchezo huo ni kuendelea kujiimarisha kwa lengo la kufanya vema kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Maxime alisema katika mchezo huo anatarajia kutumia wachezaji ambao hawakupata nafasi katika mechi zilizopita, ili kuona viwango vyao na hatimaye kuanza kuwatumia kwenye michezo inayofuata.

"Tuko Dodoma tangu jana (juzi), tutacheza mechi moja ya kirafiki, itatusaidia kuchangamsha miili ya vijana baada ya ligi kusimama, halafu Jumatano tunaanza safari ya kuelekea Mbeya, huko tutakuwa na mechi mbili za ligi," alisema Maxime.

Kagera Sugar itashuka dimbani kuivaa Mbeya City Jumamosi Oktoba 19, mwaka huu na baadaye itawakabili Tanzania Prisons, mechi zote zitachezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Katika msimamo wa ligi hiyo inayoongozwa na Simba, Kagera Sugar wana pointi tisa na wako kwenye nafasi ya tatu baada ya kushuka uwanjani mara tano.

# Michezo

Jumanne Oktoba 15, 2019

Nipashe




Lacazette kurejesha utatu wao UKURASA 30

LA KUSAWAZISHA...




Gareth Bale akiifungia Wales bao la kusawazisha wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Croatia kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 iliyopigwa Cardiff usiku wa kuamkia jana. **PICHA: MTANDAO**

# Simba sasa yamaliza ushujaa wa Mashujaa

●●● Shiboub na Ndemla wahitimisha kazi, Aussems akiendeleza rekodi ya kutopoteza msimu huu huku...

**Na Mwandishi Wetu**

PASI ndefu ya Hamisi Ndemla iliyomkuta Sharaf Shiboub na kuitendea haki kwa kuzamisha mpira nyavuni katika dakika ya 56, ilitosha kabisa kwa Simba kumaliza ushujaa wa Mashujaa katika Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma jana.

**Katika mechi hiyo ya kirafiki, Simba ilikuwa ikihitaji ushindi kwa namna yoyote ili kufuta hasira zake za kutolewa na Mashujaa katika michuano ya Kombe la Shirikisho maarufu FA Cup msimu uliopita baada ya kuchapwa mabao 3-2.**

Mashujaa inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) msimu uliopita iliitoa Simba katika michuano hiyo, ikifuata nyayo ya timu nyingine inayomilikiwa na jeshi hilo, Green Warriors ambayo kabla ya msimu huo iliwatoa Wekundu wa Msimbazi hao kwa mikwaju ya penalti 4-3 kufuatia sare ya bao 1-1.

Kwa ushindi huo wa jana, kikosi hicho cha Mbelgeji Patrick Aussems kimeendelea kulinda rekodi yake ya kutopoteza mchezo wowote wa kimashindano na mechi za kirafiki msimu huu ikiwa ni baada ya Jumamosi iliyopita kuichapa Bandari FC ya Kenya kwenye mechi kali iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Wakati huu wa mapumziko ya kupisha Kalenda ya Fifa, Simba imepanga kucheza mechi tatu za kirafiki kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Azam FC itakayopigwa Uwanja wa Taifa Oktoba 23, mwaka huu, hivyo itakamilisha ratiba hiyo kesho kwa kuvaana na Aigle Noir ya Burundi katika uwanja huo wa Lake Tanganyika.

Katika mechi ya jana, licha ya Simba kukabiliwa na changamoto ya ubovu wa uwanja, ilijitahidi kumiliki mpira lakini wachezaji walishindwa kuonyesha 'udambwidambwi' wao wa kuchezea mpira pamoja na pasi mpenyenzo hivyo mara nyingi kulazimika kutumia mipira ya juu.

Baada ya bao hilo la Shiboub, dakika ya 65 kama Ndemla angekuwa makini angeweza kuiandikia Simba bao la pili kufuatia kuachia mashine kali ya shuti lakini likapaa juu ya lango huku dakika ya 53, Rashid Juma alijaribu shuti lakini likawa chakula cha kipa.

Hata hivyo, dakika ya 85, Mashujaa walionana vema nje ya eneo la hatari la Simba, lakini walishindwa kuitumia nafasi hiyo baada ya Manula kuonyesha umahiri wake langoni kwa kucheza shuti lililoelekezwa langoni mwao.

Katika mechi hiyo ya jana Simba iliwaanzisha, Aishi Manula, Athuman Mtamilwa, Joseph Peter, Yusuph Mlipili, Kennedy Juma, Said Ndemla, Rashid Juma, Maulid Limbe, Dickson Mhilu, Ibrahim Ajibu na Francis Kahata.

Huku waliotokea benchi wakiwa ni Salum Shaban, Gerson Fraga, Sharaf Shiboub, Andrew Michael na Wilker Da Silva.

# Molinga afanya makubwa Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Yanga kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), David Molinga "Falcao" ameendelea kuwa katika kiwango kizuri kwa kuifungia timu yake mabao mawili ndani ya dakika nne katika ushindi wa 4-2 ilioupata dhidi ya Friends Rangers jana asubuhi.

Hata hivyo, Molinga na Mustafa Suleiman, bado hawajapata leseni za kuanza kuitumikia timu hiyo katika mashindano ya kimataifa kutoka Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

Katika mchezo huo wa kirafiki uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Chuo cha Polisi, Kurasini jijini Dar es Salaam bila ya kushuhudiwa na mashabiki, Yanga ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa mabao 4-0.

Bao la kwanza la Yanga katika mchezo huo lilifungwa na Maybin Kalengo wakati Molinga alifunga la pili na la tatu, ndani ya dakika nne huku Pappy Tshishimbi akipachika la nne katika mchezo huo ambao kikosi hicho kiliongozwa na Kocha Msaidizi, Noel Mwandila.

Kipindi cha pili kilipoanza, Friends Rangers yenye makazi yake Magomeni jijini na inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, iliamka na kufanikiwa kupata mabao mawili ya kufutia machozi.

Wawakilishi hao pekee wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano ya kimataifa, watashuka tena dimbani kesho kuwakabili Pan Africans, ikiwa ni mchezo mwingine wa kujiandaa kuelekea mechi yao ya mchujo kuwania kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Pyramids ya Misri.

Baada ya mchezo huo, Oktoba 20 kikosi cha Yanga kitasafiri kuelekea Mwanza kuwafuata Mbao FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Oktoba 22 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba kabla ya kuikaribisha Pyramids Oktoba 27, mwaka huu katika uwanja huo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >